BAJUNI

# Mashairi A Kibajuni


**Wahariri**

**Kimani Njogu**
**Omar Lali**
**Omar Maulana**



TWAWEZA COMMUNICATIONS
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE
Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road, Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nd̲a Twaweza Communications
Chapisho la Kwand̲a 2024

ISBN: 978-9966-128-22-5

Picha ya Jalada: Ken Saitore

Kitabu cha *Mashairi a Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha ut̲amaduni wa Vabajuni. Nradi hii hut̲ekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na Department for Digital, Culture, Media and Sport.

In partnership with

BRITISH COUNCIL

Department for Culture, Media & Sport

# Yaliyomo


Shukurani .... VII
Wahariri .... VIII
Utangulizi .... IX

**Nlango a Kwanḏa: Mahusiano**
Nvuli na Nkewe .... 2
Mahavule na Jamii .... 3
Huniuma .... 10
Hakinichambai .... 11
Mbona hunichia dhiki? .... 12
Ndoa ni Yambo Aula .... 13
Mume Anapoingia .... 14
Nke Wangu .... 15
Mwanaharamu .... 16
Upi Alo Bora? .... 17
Chunda Hili Chunda Gani? .... 18
Huu si Mwana ni Baa .... 19
Yuru .... 20
Posa .... 21
Usiche .... 22
Rafiki Angu Umari .... 23
Sheṯi Kushirikiana .... 24
Tajiri na Maskini .... 24
Amani .... 25
Mausiyano .... 26
Amani .... 26
Umoya ni nguvu na upendo wa daima .... 27
Maelewano .... 28
Shere Lindaecha Ṯabu .... 29
Kuifurahisha .... 29
Masaibu .... 30
Uchudhie Wangu Moyo .... 31
Miftahi .... 32
Umoya .... 32
Mwando va mashindano .... 33
Maisha A Kila Siku .... 34

**Nlango a Pili: Maweedha**

Vunga ........ 36
Vadhani Vakiwaiyu ........ 37
Dunia si mbaya ........ 48
Maweedha Muyashike ........ 49
Mwanangu Ishi kwa Wema ........ 50
Maweedha kwa Dhijana ........ 51
Vanangu Munisikidhe ........ 52
Maadili ........ 52
Maweedha kwa Barobaro na Havule ........ 53
Maadili ........ 54
Maweedha Kwa Waja ........ 55
Hishima ........ 55
Wasia ........ 56
Jiṯahidi Ushindre ........ 57
Duniya ........ 58
Heri kuliko kama ........ 58
Maweedha ........ 59

**Nlango a Chachu: Kadhi dha Vabajuni**

Ukulima ........ 62
Uṯonyi ........ 63
Jahadhi ........ 64
Nṯegemea Cha Ndue ........ 65
Kadhi dha Vabajuni ........ 66
Kadhi Dhechu Vabajuni ........ 67
Kadhi A Vabajuni ........ 67
Usafiri wa Kibajuni ........ 68
Kadhi Dha Vabajuni ........ 69
Jamii na kadhi ........ 70
Kadhi A Kibajuni ........ 71

**Nlango a Iṉe: Mapendi**

Mahaba ........ 74
Hunitaki Kisa Nini? ........ 75
Eo Hakuna Mapendi ........ 76
Mapendi ........ 77
Chenye Kulenga Hufuma ........ 78
Dhiki Dha Mapendi ........ 79
Nyonda ........ 79
Mapendi ........ 80
Nidhamu dha mapendi ........ 81

**Nlango a T̠anu: T̠udhingatie Ilimu**


Ilimu ... 84
It̠afut̠eni Ilimu ... 85
Ilimu Kwa Vabajuni ... 86
Ilimu ... 87
Ilimu ni Muangadha ... 87
Ilimu ... 88
Ilimu Kwa Vabajuni ... 89
Ilimu ... 90
Ilimu Muhimu ... 91
Faida Ake Ilimu ... 92


**Nlango a Sit̠a: T̠abiya dha Kiuchu**


Uchu Ukikuponyoka ... 94
Ndudhangu ... 95
Bajuni ni Vadilifu ... 96
Uchu ... 96
Dhingat̠ia Mwanadamu ... 97
T̠abiya ... 98
Uchu Kichu cha Maana ... 99


**Nlango a Saba: Dini**


Duwa ... 102
Chambua Mola Mmoya ... 103
Dini ... 104
Maisha ... 105
Uisilamu ... 106
Dini ni Uadilifu ... 107
Dini ... 108
Dini yambo la aula, chufuache vaumini ... 109
Muongodho Dini ... 110


**Nlango a Nane: Historiya**


Ni Kadari Ake Mola ... 112
Alopicha alipicha lakini huakumbuka ... 113
Machukio ... 114
Hist̠oria a Mbajuni ... 115
Hakuvalipa Kichu ... 116
Yaliowapat̠a Vabajuni ... 116
Hist̠oriya ... 117
Hadithi ya Kibajuni ... 118
Bajuni ... 119

Hisṯoriya........ 120
Mbajuni........ 121
Ṯarihi A Kibajuni........ 122

**Nlango a Ṯisa: Uṯamaduni**
Mabarobaro na Jamii........ 124
Chuhifadhini Ṯuraṯhi........ 129
Chuṯayapo Maadili........ 130
Ṯanabuhi........ 131
Dhama Dhechu........ 132
A Kwapi Maina Echu?........ 133
Uganga........ 134
Maledhi A Kibajuni........ 135
Dhama Hidho........ 136
Jamii........ 137
Kiswahili........ 138
Harusi dha Vabajuni........ 139

**Nlango a Kumi: Madhingira**
Kulindra Madhingira........ 142
Kuhifadhi Madhingira ni Ada........ 143
Madhingira........ 143
Kulindra Madhingira........ 144

**Nlango a Kumi na Moja: Maisha a Ugenini**
Maisha a Ugenini........ 148
Maisha Ugenini........ 149

**Nlango a Kumi na Mbili: Ushirikishwaji**
Nyukani Vana Nyukani........ 152
Hupachikanae furaha?........ 153
Kuveeye mbona huvaye?........ 155
Kauli A Mafundisho........ 157
Mwanasimba........ 158
Fumbo........ 159
Risala Nda Veṉe Pwani........ 160
Hii Shungwaya ni Kwechu Huṯawalie Vageni?........ 161
Sivone Dhombo Kupicha Ungama Ulini Mui........ 162
Kufukuliwa mafucha........ 163
Chuamke Vabajuni........ 164

## Shukurani

Kiṯabu hichi dha ***Mashairi a Kibajuni*** ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Chwatoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuanḏika na kuchapisha kiṯabu hichi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṯabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a mashairi a luga ao. Chwavashukuru vaandisi va mashairi etu na vale vote vanavoimba mashairi a luga etu kwa ushirikiano wavo na vaanḏishi kachika haṯua dhoṯe na kumalidha kuanḏika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia twavashukuru vale voṯe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni.

**Diwani A Kibajuni**

1. Sina budi kushukuru<br>Kwa alochuumba Manani<br>Na pia kunshukuru<br>Ndugu echu Asumani<br>Mwengine nankushukuru<br>Ni Purofesa Kimani<br>Kwa juhudi ao kuru<br>Kuichapisha DIWANI

2. Kuna na kina Umari<br>Juhudi kuifanyidha<br>Kwa kadhi yao ndhuri<br>Vote n’nawapongedha<br>Nafisa kwa uhodari<br>Kadhi aliimalidha<br>Kurakibisha dosari<br>Dhote dhiloitokedha

3. Pongedhi ni kwa valochunga<br>A DIWANI mashairi<br>Dhina, midhani kutunga<br>Kibajuni kishamiri<br>Vameandika ya Vunga<br>Na mangi kwa uhodari<br>Na o’te valiyapanga<br>Kuchupa isi Madhuri

4. Asumani na Kimani<br>Duwa chunaikariri<br>Mikono echu itani<br>Kuvaombeya Jabari<br>Afaulu a DIWANI<br>Awape a’lo Madhuri<br>Mufaulu duniani<br>Kwa afiya na umuri

5. Kuiyandika DIWANI<br>Indakuva enu ari<br>Lahaja a kibajuni<br>Itadhidi kunawiri<br>Itakuva dhitabuni<br>Kwa luga a ushairi<br>Isomwe kote dhuoni<br>Fahari a mbajuni

6. Mememalidha huvaaga<br>Kuvaaga si hiyari<br>Kuondoka kutovaga<br>Ni makosa si udhuri<br>Umari imi huvaga<br>N’ndamalidha shairi<br>Mvagaji akivaga<br>Hunena haya kwaheri

## Wahariri

**Omar Lali** ni Katibu Mkuu wa Shungwaya Welfare Association. Amewahi kufanya kazi na Taasisi ya Maendeleo ya Mitaala ya Kenya na kufundisha katika shule mbalimbali. Alihudumu kama Mjumbe wa Baraza la Kaunti ya Lamu, akiwakilisha wodi ya Kiunga.

**Omar Maulana** ni mwalimu mstaafu wa lugha na fasihi ya Kiswahili. Baada ya kuhitimu kutoka chuo cha walimu cha Kisii alisomesha Shule ya Upili ya Witu na Lamu Boys. Amekuwa akishiriki mambo mbalimbali ya uongozi katika Kaunti ya Lamu.

**Kimani Njogu** ni msomi na mtafiti wa lugha, fasihi na utamaduni. Kwa miaka mingi alifundisha katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Kwa hivi sasa, ni Mkurugenzi wa Shirika la Twaweza Communications Center, Nairobi.

## Utangulizi

Kitabu hiki cha *Mashairi a Kibajuni* ni sehemu ya mradi wa kulinda na kuimarisha turathi za Kibajuni unaoendeshwa na Shirika la Twaweza Communications pamoja na Shungwaya Welfare Association na Swahili Resource Centre kupitia Mfuko wa British Council Cultural Protection Fund (CPF). Ili kukusanya mashairi haya, viongozi wa mradi walitoa tangazo kwa washairi wa Kibajuni waaandike mashairi kuhusu mada mbali mbali. Baada ya kupokea mashairi kutoka kwa watungaji, mashairi hayo yalipigwa msasa na warsha ya kusoma mashairi hayo ikaandaliwa kisiwani Lamu mnamo Julai 2023. Washairi waliohudhuria warsha wakapata fursa ya kusoma mashairi yao kwa pamoja . Mashairi mengine yalighaniwa na kuingizwa kwenye tovuti ya mradi; www. Bajuniculturalheritage.org

Nchini Kenya, Kibajuni (*Kitikuu*) kinatumiwa zaidi kaskazini ya mwambao wa pwani ya Kenya kuanzia Kilifi hadi miji ya kusini mwa Somalia ya Ras Kiyamboni hadi Kismayu. Kwa jumla tunaweza kusema kwamba Kibajuni kinazumgumzwa Kiunga, Mwambore, Ishakani, Simambae, Rubu, Matironi, Mvundeni, Mkokoni, Shanga, Rasini, Faza, Tchundwa, Myabogi, Mbwamwali, Kizingitini, Ndau, Mtangawanda, Shuwei na Kiwaiyu. Nchini Somalia Kibajuni kinatumiwa katika eneo la Kismayu.

Wabajuni wamekuwa wakitunga mashairi tangu jadi. Kama ilivyo katika jamii zote duniani, ushairi hujibainisha kama sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato, na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilizaji. Maneno ya mashairi huteuliwa kimaksudi ili yalete taswira maalumu akilini mwa msomaji au msikilizaji. Maneno hayo pia hupangwa ili yatoe mdundo fulani wakati shairi linapoimbwa, linaposemwa, linapoghaniwa, au linaposomwa. Ushairi hulenga moyo kwa sababu hueleza jambo na kutuingiza katika hisia fulani. Ushairi unaweza kumfanya mtu ahisi uchungu au furaha, hasira au ridhaa; waweza kumburudisha mtu hadi moyo wake utulie; ama kumhamasisha mtu achukue hatua fulani ya kubadilisha hali, kama yafanyavyo mashairi mengi ya ukombozi.

Tungo za kimapokezi za Wabajuni ni pamoja na **vave, randa, na kimai.** Vave huimbwa wakati wa ukulima na kusaidiana kukata mwitu, kufyeka,

kuchoma magugu, kupanda, na kuvuna. Ni utungo wa kushajiishana, kupana nguvu na moyo, ilimradi watu wafanye kazi kwa kushirikiana. Randa huimbwa baada ya kazi ya kuchoma magugu kukamilika na watu kurejea nyumbani. **Kimai** ni utungo unaohusu mambo ya bahari na usafiri itokeapo ya kwamba mtu au watu wamepotea baharini. Ni njia ya kusawiliana na yule aliyepotea baharini. Tungo hizi za kimapokezi zimechangia pakubwa katika kuimarisha ushairio wa Wabajuni.

*Mashairi a Kibajuni* ni kitabu cha kipekee na cha mara ya kwanza kuchapishwa kikiangazia mashairi ya Kibajuni moja kwa moja. Kinyume na vitabu vingine vya mashairi, kimeandikwa kwa kutumia lahaja ya Kibajuni na bila ya usanifishaji. Usanifishaji wa maandishi ya Kibajuni bado haujamilika na kwa hivyo matumizi ya sauti za **ṉ**, **ṯ,** **ḏ,** **kh** na kadhalika bado hayajafikia maafikiano. Katika baadhi ya mashairi, msomaji ataona **ṉ**, **ṯ,** na **ḏ,** zikiendelezwa kama **n’, t’ na d’**. Baadhi ya waandishi wanzingatia mpumuo wa /**k**/ unaopatikana katika Kibajuni na kutumia tahajia ya /**kh**/. Tofauti hizi za tahajia zinabainisha umuhimu wa kusanifisha maandishi ya Kibajuni ili kuleta wiano katika maandishi. Juhudi zilizoanzishwa na mradi huu ni za awali na zapasa kuimarishwa. Kwa mfano, katika kitabu cha Chusomeni Kibajuni (Gredi 1, 2, 3) kilichotolewa na mradi huu kimetumia **ṉ**, **ṯ,** na **ḏ** ili kubainisha tofauti ya Kibajuni na Kiswahili sanifu.

Mashairi yana mchango mkubwa katika maisha ya Wabajuni na yamekuwa yakikaririwa katika sherehe tafauti. Mara nyingi mashairi haya huwa ni ya ngonjera au malumbano ambapo washairi huwa na kipaji cha kutunga papo hapo bila kuandika na huwa ni kujibizana. Kwa mfano, katika ngoma ya Msondo, ambayo kuna mchanganyiko wa wanawake na wanaume, huwa kuna ushindani mkali wa kishairi na hushangiliwa na wasikilizaji wao.

Kama itakavyodhihirika katika kitabu hiki, utungaji wa mashairi ya Kibajuni umebobea zaidi katika tathilitha (mishoro mitatu kwa ubeti) na tarbia (mishororo minne kwa ubeti) na si kawaida kuona mtungaji akitumia mbinu nyingine za ushairi. Sifa nyingine zinazoweza kubainika ni:

- Tathlitha unusu (mishororo mitatu na kipande)
- Matumizi ya mizani na vina

- Katika mishororo yote ya ubeti mmoja, kina cha kati chaweza kuwa kimoja, na cha mwisho kimoja.
- Kina cha kati chaweza kuwa kimoja lakini cha pili cha mshororo wa mwisho kikabadilika.
- Shairi laweza kuwa la **pindu**, ambapo mizani ya mwisho au neno la mwisho la mshororo mmoja au kipande cha mwisho (utao) chaweza kuwa kianzio cha mshororo unaofuata au ubeti unaofuata.
- Katika mtindo wa *uneni* alioutumia Mohamed Kombo mizani huenda isilingane kwa sababu lengo la mshairi ni 'kunena' mashairi kwa mdundo. Mashairi hapo yametungwa kimazungumzo.

Sifa ya Kibajuni ni kuwa Wabajuni wanajifahiri na lahaja yao na wakienda maeneo mengine si rahisi kubadilisha lugha yao.

Tunatarajia kuwa utafurahia Mashairi a Kibajuni!

***Kimani Njogu***
***Omar Lali***
***Omar Maulana***

Januari, 2024.

# Nlango a Kwanḓa: Mahusiano

## Nvuli na Nkewe

*Abdalla Ali*

1. Uwe nilikuambiya
   Ukaiaṯa  shariya
   Imi ukanimbiriya
   Indakuva wayuṯiya
   Ṯabu dhindakudhidiya.

2. Uṯabakiya uyusi
   Ulinifanya siisi
   Kavona siku halisi
   Ukafura kama bisi
   Kwangu ukanena basi
   Kamwandama ibilisi.

3. Kila kichu kaṯukuwa
   Kwa simu si kwa baruwa
   Na koma kunsumbuwa
   Una alo kuṯukuwa
   Mara uwe mechambuwa.

4. Ulilikacha shauri
   Ikakudhidi kiburi
   Ukiambiwa subiri
   Hukuivona haṯari
   Na kwa sasa ndahiyari
   Uliiaṯa bandari.

5. Mbona waṯaka kurudi
   Ni yambo la makusudi
   Yamekupacha dhaidi
   Ukaipeka baidi
   Ulivona ṯafaidi
   Kwako siyava hasidi.

6. Lipi  nilokufanyiya
   Maringo ukaichiya
   Imi ukanisusiya
   Indakufunda duniya
   Ndakwisha kuichikiya.

7. Kaṯu hukunivulidha
   Langu imi ukaidha
   Ukampacha nahudha
   Ṯayari vandakuidha
   Kwako  kundachanda gidha
   Huna wa kukunyamadha.

8. Kukwambiya subiriya
   Imi  ukanikimbiya
   Buree ukaniṯukiya
   Huṯaki kunisikiya
   Dhishindomi ukangiya.

9. Ndio kwangu ukagura
   Hunivudhi kula mara
   Imekushinda subira
   Kamfanya ndio bora
   Umeivona hasara.

10. Ukaifanya hasira
    Maudhiko kila mara
    Kwa dhishindo ukagura
    Ukava kama bendara
    Ukaanda kunikera
    Ukaifanya ni bora.

11. Huku umekosa nini?
    Ukaṯaka kunihini
    Hoko uliposamini
    Kaniveka machesoni
    Kumbe hukuṯamakani
    Sasa karibu ṉumbani.

## Mahavule na Jamii

*Mohamed M. Kombo*

1. Huand'a kwa ina lake
Mola wechu atukuke
Alonvumba mawananke
Kidhadhi kihifadhike

2. Hunswalia wechu nchume
Alo nena ahishimiwe mame
Mara ch'achu kuliko mume
Na kuntukudha nisikome

3. Kachika historia akiislamu
Chusikose eo kuvafahamu
Vanavake chunavo vahishimu
Kwa imani na wavo ukarimu

4. Wa kwand'a ni Nana Hadhija
Alo mwamini nchume bila huja
Kwa imani lake hakunena ngoja
Hofu a atakao kuya akaituja

5. Ndrie wa kwand'a d'uniani
Uwisilamu alo uwamini
Bila kuveka shaka moyoni
Wala utajiri kunveka kidhani

6. Shahid'i wa kwand'a ni Nana Sumeya
Alonena hoo ni nchume wahaki alokuya
Akaambiwa tavuwawa ama abad'ili niya
Akakachaa kwa Mungu wake akaekeya

7. Ph'epo a-Mungu ali ahid'iwa
Kwa uchume kuuchambuwa
Na kulee kukubali kuvuwawa
Apache ujahilini kuikombowa

8. Wa kwand'a kachika kaumu afiraona
Iye na nchume Musa kukubaliana
Alonena nd'a Mungu haa shaka hakuna
Ni Nana Asiya chufahamuni vaongwana

9. Wa kwand’a kuwamini vend’ani
Wa kwand’a kufa shahid’i vaumini
Wa kwand’a kuupinga ufiraoni
Ni vanavake haa chusisahauni

10. Kachika utukufu havakubaki n’ima
Kachika uwongofu pia valisimama
Valikalia mbee mbee kachika mema
Kama atukuwavo mimba ako mama

11. Hidhi sifa njema isi huivunia
Vanavake vema valo chuatia
Takani hii mifano kubarikia
Sifa dha mwananke kubakia

12. Kwenye d’ini mumetukudhwa
Majumbani kubalini kutund’wa
Maledhini mupache kuongodhwa
Mukikuwa musinene hamukufundrwa

13. Ivekeeni hishima pache muitukudhe
Muve vaja vema jamii muiyongodhe
Avavonao kuvahishimu asipudhe
Na kwen’e upochofu asivaekedhe

14. Sababu akunena haa ni hakika
Kuva d’unia echu ind’aharibika
Hakuna hata imoya len’e mpaka
Kwa malimwengu chund’aghurika

15. Mach’iviini ndrudha huiyanika
Ng’ondra vapache kudhanyika
Samaki havatakikani kulika
Valonona sasa hudharaulika

16. Sid’unia a mila nyendro na tabia
Ni wakati wa ushetwani kubarikia
Hishima na sitara hadhina maridhia
Uvundro na ulanisi dhind’achuvamia

17. Eo kuva bora ni kudhia
Kuva d’ufu ni kusuluhia
Haa ndrio and’ao chuyia
Kuchuharibia echu d’unia

18. Vavadharauvo vanavake nvalanisi
Vasoyiva sitara na uchu havauyisi
Vaso nahaya wala aibu maibilisi
Holiud’i huliana n’ama maduyusi

19. Hutauliwa vanavake kama samaki
Kwa ina lafesheni hachuvoni dhiki
Haa ni madharau chusiashabiki
Kuvakosesha dhaubinad’amu haki

20. Kwa soda mahavule musiiyumbuwe
Kwa kh’uku na chips musidharauliwe
Fesheni na ch’ivii dhisivachafuwe
Kwa a-Mola wenyu ndrio muikuwe

21. Uchu wechu uchungeni
Mubakie nao sitarani
Musitake kungia aibuni
Kwa kunkudha shetwani

22. Chiki choki isivahad’ae
Wala a aibu musiachwae
Akimbieni musipumbae
Akuvachafuwa mamboe

23. Kwa vuso kitabu musihad’aike
Uhavule ukakosa udhuri wake
Ngiani kwa akili musighurike
Kwa mavidio aulanisi muepuke

24. Siveni dhishadhi dhaisi nveledhe
Ngiani pache mila echu muikudhe
Tamad’uni ndrio mudhitukudhe
Na d’ini echu muichangadhe

25. Kwa wasapu kuichambuwa
Ni muhimu sikoseni kuelewa
Nchu kwa hishima huikuwa
Ndripo apachapo kuhishimiwa

26. Na kwa instagiramu
Musikose kufahamu
Leroro huva igumu
Halali kava haramu

27. Mahavule ivekeeni hishima
Musitauliwe kama makoma
A apekao sokoni nkulima
Kudhanywa ndrio hatima

28. Aitukudhao ndrie hutukuka
Aidharauwo hudharaulika
Huu ni ukweli uso shaka
Aiyumbuwao huumbuka

29. Mungu alinchaguwa mwananke
Ave mama wa ulimwengu wake
Haa nimapend'i a-Mola afahamike
Kumpa mwananke utukufu atukuke

30. Nswahafuni suratu nnisai Mia
Kusoma vaisilamu alichuchumia
Hakuna suratu rijali navambia
Nikutukudhwa in'i mund'asikia?

31. Akikosa mwananke kuitukudha
A Mungu wake ndrio akaapudha
Basi ulimwengu ayive tauvodha
Maisha duniani kilo kuwalidha

32. Mahavule yivani ndrin'i mama vakesho
Mufanyao nimaand'isi kwen'e mbasho
Mwayiva m'bibo hudhawa na kh'orosho
Ujana ungava mocho huva ivu mwisho

33. Ṯabani ilo mifano mema
Akina wechu Nana Fatima
Ababa na mama kuand’ama
Nakuvajali vachu vadhima

34. Ilimu kalitafudheni
Lad’unia nala d’ini
Na n’ima sibakieni
Jamii ichambueni

35. Havule ni vuso wajamii vend’ani
Ni nuru akidhadhi hili lieleweni
Ndrie nocha audhuri n’umbani
Akihishimu vadhee huchia imani

36. Havule ndrie hukipa kidhadhi sifa
Akiitukudha kwa tabia na maarifa
Akaichambuwa kayidha akashifa
Asikubali yeda kwendra kunchofa

37. Havule aivekeyao hadhi
Akavatukudha vadhadhi
Anvonao kuva ni mpudhi
Ni n’nyama kama mbudhi

38. Havule huhishimika
Kwa ad’abu akiiveka
Vadhadhi vakiridhika
Kwa Mola hutukuka

39. Havule ambae ni n’dhuri
Hauwaniki wake udhuri
Huihishimu kwa kuisitiri
Ndrio udhuri wake fahari

40. N’dhuri huvonekana
Haivonyeshi ni lana
Nialo gali kupachikana
D’angironi kukosekana

41. Ichundra lipend’walo nchini
Ni lilee lilioko kiremberembeni
Kila alivonao ruhuni hulitamani
Chund’aivudha sababu nnini?

42. Ni kuva sirahisi, lilipo kupachikana
Udhuri wake kamili, sitarani hulivona
Kulitaka, niumee mbava muongwana
Ndrio kulisikilia, kitand’uni lilipo fana

43. Huu ndrio udhuri, wa havule alo iveka
Hii ndrio sifa, audhuri wen’e kusifika
Halina udhuri, ichundra lilo anguka
Mana huliwa, hata na iboye kilitaka

44. Mwananke ni mame,alonidhaa kaniea
Mwananke mmwanangu ubora huntakia
Mwananke ni vake vana valo nidhalia
Mwananke ni ndruangu ad’abu humuusia

45. Mwananke ni n’yukuwa wangu Aliya
Ruhuni mwangu muanga ulo chuliya
Ulimwengu mwema humuombeya
Akikuwa apache wema kuufurahiya

46. Ndrio haa mahavule kavambia
Utukufu mwananke kuntakia
Nledhi wajamii kachika d’unia
Atukuwao mimba nyedhi tisia

47. Mwananke ni nuru mwangu moyoni
Mame kipend’i na n’ngine hafanani
Kuntakia utukufu hukumbuka hisani
Ndrio kuvambia mahavule ihishimuni

48. Mwananke ndrie alo niecha d’uniani
Kwa maamrisho a-Mola Rahamani
Uko th’ini asati nlango wa ph’eponi
Ndrio kuvambia mahavule ihishimuni

49. Awembamba na unene si muhimu
Kuva na afiya nd'uri ndrilo tamu
Sitara na ad'abu dhivaladhimu
Ndrio uchu wenyu kuufahamu

50. Musifanywe dhid'ed'e kutedhewa
Musikubali mivili enyu kukosewa
Kwa ndi'ia dhadharau kuchumiwa
Mipaka aubinad'amu kuharibiwa

51. Mwananke ndrie mama wa maledhi
Amilikio maishani mwake in'e ngadhi
Mimba, kudhaa, kufundra, ndrie n'yudhi
Kuwea ali ntauwa Mola mwenye edhi

52. Kwangu ni muwangadha
Wangu mame huntukudha
Ni mangi maishani kiavadha
Mambo ambao aliniyudha

53. Havule kwa hishima iveke
Ndrio ahishimike mwananke
Ulimwengu pache atukuke
Ruhuni mwechu chufurahike

54. Alikuva ntwiifu havule
Mame imi Mwanabule
Aloyiva a nusu na tele
Akunielea imi nkale

55. Havule alikuva na hishima
Nahida mwanangu mwema
A-Mungu alikiri kuand'ama
Nd'ake radhi wangu nema

56. Ukiyaa nkundre, tavuna kundre
Ukiyaa nchendre, tavuna ch'endre
Choo kichafu, hukitawali mend'e
Kilicho safika nchafu na sendre

57. Mahavule imi huvausia
Nneneeo kuadhingatia
Isivahad’ae nno d’unia
Hishima mukaivund’ia.

## Huniuma

*Mohamed M. Kombo*

1. Huniuma huniuma, nilo nao huniuma
Siugonjwa wahuma, ntabibu nichadhama
Alondrani hunichoma, moyoni hunichafuna
Sinipe kh’aumwa kama, d’awa ake huna

2. Uwe wangu ntabibu, nitibu nami nitibike
Ugonjwa huniadhibu, kichandani siniveke
Kunandokea adhabu, niechea d’awa ake

3. Hukuomba nitibu, maradhi nilio nao
Siaate kuniadhibu, kuniumidha ndruo
unao uwe tabibu, d’awa ake atakao

4. Ch’embe sitajaribu, wayiva sid’awa ake
Naakwelee muhibu, nigani utabibu wake
Niwadha ewe tabibu, kichandrani siniate

5. Simidhi simayani, wala ch’embe dhad’ukani
Pia hosipichalini, hauwadhiki ulo ndrani
Ntabibu kwahisani,d’awa niechea nami

6. Niechea dhabibu, pamoya namakudhumani
Dhipungue dharubu, kh’idhiveka midomoni
Kisha unipe tabibu, d’awa akupodha ndrani

7. Nilo nadho dharubu, hunidhid’isha ntango
Kama sikucha aibu, ningaliugonga nlango
Niechea d’awa tabibu, niuchapike ushingo.

## Hakinichambai

*Mohamed M. Kombo*

1. Yapokuva vaongwana, moyo wangu hunirai
   Ili nive mwema tena, hili yambo musitumai
   Kilicho niuma yana, eo hakinichambai

2. Alo moyoni taanena, katu haa sinyamai
   Sindruo mungadhalikana, akuvonyao urui
   Kilicho niuma yana, eo hakinichambai

3. Sibarikii kulipana, hauna faid'a uwad'ui
   Lakini lakuyivana, kwa hili siichomoi
   Kilicho niuma yana, eo hakinichambai

4. Mambo kunyamaliana, nyoyo haadhungui
   Nibora kwambiana, aand'ame nkondro mai
   Kilicho niuma yana, eo hakinichambai

5. Kwa vadhee navana, ujumbe hauchagui
   Ukifanya akudhuriana, funguni haakutoi
   Kilicho niuma yana, eo hakinichambai

6. Uwadhi nimeuvona, sasa nami siisumbui
   Mifano kila namuna, akina havachambui
   Kilicho niuma yana, eo hakinichambai

7. Tamati hapa th'asona, nasikie goi goi
   Undrugu hauna maana, ubarikiyao urui
   Kilicho niuma yana, eo hakinichambai.

## Mbona hunichia dhiki?

*Mohamed M. Kombo*

1. Wanitaka hutakiki-mbona huweleweki
Wanipenda hupendeki-nnini hufunuki
Kama nikunichia dhiki-basi hili sitaki

2. Wataka kuva nami-kiva nawe hunaraha
Likukeralo husemi- likimbidhalo furaha
Maudhiko hunatia imi-moyoni kana jaraha

3. Ukinikosa hunitafudha-kinivona huna haja
Kh’ikaribia hunifukudha-kh’iva mbali nihuja
Lililoko basi neledha-sinifanyie dhioja

4. Kisafiri hufanya mayond’i-kh’iveko taka nandroke
Hukuvuwa angu mapend’i-pia hukuchia nvuke
Hidhi dhote ph’ingamand’i-niupi nsimamo wake?

5. Kh’ikwicha kwichwa hutaki-kh’inyamaa nimachacha
Kh’ikuenga pia hufurahiki-kuto kuengwa nidhicha
Mara huvamocho hud’ariki-ama kuvakisu kukh’acha

6. Tamati hichi sikikomo-yapo kuva hukoma
Hunid’anganya dhipimo-inganielea kupima
Nambia niyive kisomo-chako ulipo kisoma.

## Ndoa ni Yambo Aula

***Yusuf Kassim***

1. Nimepachwa na jadhiba, shairi kulihuṯubu,
Nikueledhe misiba, ujane unavosibu,
Ndoa mwando ni mahaba, vachu vanavohisabu,
Ndoa ni yambo aula, ujane ni kichu duni.

2. Ndoa ni kichu aula, kama miṯhili dhahabu,
kuipacha ni fadhila, na baraka na ṯhawabu,
Na kuikosa madhila, wankidhibu Wahabu,
Ndoa ni yambo aula, ujane ni kichu duni.

3. Japokuva sina pesa, siwedhi kuikidhibu,
Na moyo niṯauasa, kuchenda la kuharibu,
Ndoa kwa nchu halasa, kuva nao ni wajibu,
Ndoa ni yambo aula, ujane ni kichu duni.

4. Jenga jengo la fahari, kuchadhe dhive dhahabu,
Na milango a johari, kwa Lulu kuidhekebu,
Bila ya nke si ndhuri, nyumba uṯaiharibu,
Ndoa ni jambo aula, ujane ni kichu duni.

5. Ndoa kichu cha heshima, kila chunapohisabu,
Ndani ake ako mema, na faida ya ajabu,
Ndoa ni kichu cha nema, lipi la kuṯaajabu,
Ndoa ni jambo aula, ujane ni kichu duni.

6. Hachuvi vachu kamili, bila kumucha Wahabu,
Na kuiva la halali, na ambalo huharibu,
chufapo kachika kweli, pepo kwechu ikaribu,
Ndoa ni yambo aula, ujane ni kichu duni.

7. Si ooṯe kuṯauva, ni pande dhoṯe kuhibu,
Mwananke kuoleva, ni siṯaha na adabu,
Na mwanamume kuova, hukamilisha wajibu,
Ndoa ni yambo aula, ujane ni kichu duni.

8. Mola valinde dhigoli, pamoya na vanawali,
Vave kama va awali, kama dhama dha rasuli,
Nimemalidha kauli, hapa nafunga kufuli,
Ndoa ni yambo aula, ujane ni kichu duni.

## Mume Anapoingia

***Quswai Sufiyani***

1. Awali nachangulia, kumuhimidi manani
   Na swala kunswalia, kipendhi ake amini
   Mola kinipa afua, machache ṯaabaini
   Mume anapoingia, nke ako nlangoni

2. Nke ako nlangoni, ṯayari kumpokea
   Mayi ako nkononi, kwa hishima kimwechea
   Na maneno a uṯani, kwa henedhi kimwambia
   Na mayi a mocho chooni, ṯayari undamwekea

3. Ṯayari undamwekea, kisha nae amwandame
   Mayi akimwaia, ainame achuchame
   Mume kiyafurahia, asinene asiṯame
   Leso kimfukidhia, na mangine chusiseme

4. Na mangine chusiseme, chuṯaivuka mipaka
   Chunenapo a kinyume, vangine vaṯaudhika
   Ni hakika vanaume, valiwakiheshimika
   Nyendo hidhi dhisikome, bado dhinahiṯajika

5. Valiwakiheshimika, navo vake kuwajali
   Haki dha nke hakika, valihishimu kwa kweli
   Havakuwahi kufoka, kwa sauṯi a ukali
   Vakinena na kuṯeka, pendi lao la asali

6. Pendi lao la asali, kwa dhaṯi vakipendana
   Familia dhoṯe mbili, dhikadhidi kushikana
   Nasi chwaomba Jalali, dhama dhirudie ṯena
   Maisha mekuwa dhili, ndoa dha kuchukanana

## Nke Wangu

*Omar M. Maulana*

1. Nilimpenda kwa dhaṯi, nke huu navambiya
Nikaiva simuwaṯi, kwa njema ake ṯabiya
Nikaapa Jabaruṯi, imi siṯombiriya

2. Nilimpenda kwa kweli, maṯo akanipofuwa
Kava sivoni muhali, popoṯe kinṯukuwa
Kichu hakikuwa gali, akiṯaka hununuwa

3. Nilimpenda bayana, hilo sichi kuchobowa
Bado kimvona mwana, haṯa umuri kukuwa
Kwa kuiva nampenda, naye akaishauwa

4. Nilimpenda moyoni,na ruhuni kamveka
Kama iye simvoni, chakula hakikushuka
Kichanda sikuṯamani, kama hakukichandika

5. Nilimpenda nrembo, nke huu wa hishima
Nikampa kila pambo, kudhidisha ṯakirima
Anivudhapo na yambo, midomo hunichechema

6. Nilimpenda hakika, mwana alinisawadha
Shahidi Mola Rabuka, kila saa kimuwadha
Kila mui venye duka, kinunuwa sikusadha

7. Nilimpenda kipendi, kwake kadhidi mahaba
Kula asichokipendi, sikufanya haṯa haba
Kisafiri ni mayondi, huwa sili nikashiba

8. Nilimpenda kwa ari, kwa wivu kiniumidha
Kwa loloṯe ni ṯayari, yoyoṯe kummalidha
Lawama nikahiyari, na ya vachu kuyapudha

9. Nilimpenda sauṯi, na shingo ake ngamiya
Hana mwendo wa maṯiṯi, ṯausi hufananiya
Vakimuona umaṯi, maṯo hunkodoleya

10. Nilimpenda midomo, midhuri a kuneneya
Kwa shughuli hana somo, hafanani na mmoya
Ndiye pweke changu omo, ṯedhi na ngama pamoya

11. Nilompenda sinaye, mahasidi ndanivuwa
Ṉndaepukana naye, ṉdakimbiya wa muruwa
Licha kumvona iye, haṯa ina meṯukuwa

12. Yarabbi nipa subira, subira ya manabiya
Unisiṯiri siṯara, Siṯara kuvumiliya
Kuvumiliya harara, a pendo nilodhoweya.

## Mwanaharamu

***Omar M. Maulana***

1. Mwanaharamu si mwana, kila nchu hunnena
Hawamuaṯi kusona, ndimini hunchafuna

2. Mbona huyafanya hiya, na mwana hana haṯiya
Kuya kachika duniya, iye hakusaidiya

3. Valiafiki vavili, kwa dhao mbili akili
Kuyachenda ya baṯwili, ya dhina kuyakabili

4. Valingiya faragani, kiṯoṯo au mwichuni
Au vakava chumbani, hiyo mbeu kuichiya

5. Siku dhikawa ni nyedhi, na haipachikani hedhi
Kuṯembea kwa henedhi, ya dhishindo hayawedhi

6. Mimba ikadhaa dume, mwana huliya na mame
Kudhaa bila a mume, Iṯakuvae? nchume!!!

7. Vanavake vamuini, vakimuona ndiyani
Hunena ni nchu duni, mwanachisi wa fulani

8. Akifanya la makosa, au akipeka posa
Paka awe na mapesa, ndio mambo huyapisa

9. Ya nchu duni dalili, huimbwa iye dhalili
Kijaa kila mahali, hukiṯoa baradhuli

10. Kosa lake iye lipi?, haki yake hamumupi
Kumvoneya ni kupi?, masikini ende kwapi?

11. Ina la ishe Andala, na babu yake ni Dala
Akiuliza suala, hambiwa chuwa iyala.

12. Mwanaharamu haramu, kurisi kwake ni sumu
Ina vandamdhulumu, hafai kwenye kaumu.

## Upi Alo Bora?

***Omar M. Maulana***

1. Nilimveka farasi, nama alo maridhiya
Bei ake si rahisi, gali nno ṯavambiya
Kwa mwendo wake wa kasi,mbali kiiṯembeleya
Hakunivonya nuhusi, nṯiifu va ṯabiya

2. Nikanunua ipunda, kadhi kunisaidiya
Kula kiṯaka kupanda, ubishi hunifanyiya
Ṯabiya ake ni inda, mashudhi kunibikiya
Na aamuwapo kudinda masheke ṯanirushiya

3. Madhidhini nalikwenda, mwana ṉgombe kwangaliya
Kavaaṯa valokonda, igalimu kalipiya
Kila siku kaipinda, wisha kunnunuliya
Changu idhiwa kupanda, sinunui kopo moya

4. Kenda kanunuwa mbudhi, mwanangu kamuwecheya
Dhichendo dha kuniudhi, akava hunifanyiya
Huya kuninyeya chudhi, nlangoni pakungiya
Idhiwa lake siwedhi, kwa kiṯusi kudhidiya

5. Hondoo nikajaribu, nama mwema kudhwahiya
Nilimpenda ajabu, una nno madhoweya
Mara bila ya sababu, kiṯwa huya kakuchiya
Kiva kwako ni bawabu, majini havaṯongiya

6. Kuku naye kamveka, kut̲aka kumwangaliya
Kupara ndake huluka, hilo sikulit̲ukiya
Ingi lake hulipika, vali nikachoveleya
Na usiku akivika, ni swala indawadiya

7. Huyu bit̲a kumuecha, mapema niliyut̲iya
Kwenye chocho t̲ampacha, uchafuni undangiya
Hana fujo si machacha, kwa uchafu medhidiya
Siyamuona kuchecha, dhicha hadhikumweleya

8. Imbwa akava wa mwisho, kut̲aka kumwangaliya
Si nama wa malisho, nilacho hunt̲upiya
Numbani una uchisho,mwidhi hapachi kungiya
Hat̲a nikirudi kesho, hakuna cha kupot̲eya

## Chunda Hili Chunda Gani?

*Omar M. Maulana*

1. Ina lake kulichaya, vangi huwa vana haya
Vala hakuna ubaya, chunda hili chunda gani?

2. Halimei mahon̲deni, vala haliko nchini
Na halidhanywi sokoni, chunda hili chunda gani?

3. Dukani ukit̲afudha, vachu vat̲akuvudha
Uwe umerukwa mbedha? chunda hili chunda gani?

4. Guniyani halichiwi, vala halihisabiwi
Na bila hili hayawi, chunda hili chunda gani?

5. Mane ni kwa echu dini, dhaidi huva dhambini
Ule kwa kulit̲amani, chunda hili chunda gani?

6. Chunda lingava it̲amu, si la munu chwafahamu
Sukari hamuna humu, chunda hili chunda gani?

7. Lindaumbua mashehe,chunda hili la sherehe
Valao husit̲arehe, chunda hili chunda gani?

8. Kila hufanya pumudhi, kishiba mwisho siwedhi
Huchapika kama dudhi, chunda hili chunda gani?

9. Kula kwake kwa dhishindo, sawa kubika nsondo
Ukishiba keṯi kando, chunda hili chunda gani?

10. Haramu a chunda hili, makosa kula vavili
Halavanywi nusu mbili, chunda hili chunda gani?

11. Hapa nipo kikomoni, nimewavudha wendani
Nipani nami undani, chunda hili chunda gani?

## Huu si Mwana ni Baa

***Omar M. Maulana***

1. Ni shani a kila mja, a kudhaa duniyani,
Huva kwake ni faraja, moyo kupacha amani,
Na vakwe kukosa huja, muyukuwa kuṯamani,
Ila kwangu ni dhihoja, Huyuṯi medhaliyani.

2. Furaha kubwa moyoni, numbani ilichungiya,
Kumdhaa Asumani, duniyani aḵangiya,
Kava na maṯumaini, a njema ake ṯabiya
Kanama ni sheṯwani, Kudhaa huiyuṯiya.

3. Nilikesa kubembedha,Asumani asiliye,
Kiimba kunliwadha, Asumani achuliye,
Nyimbo dhoṯe sikusadha, Asumani bwana ndiye,
Eo vachu hunivudha, mwana huu ukeiye?

4. Si mwana ni afiriṯi, kwa maneno na dhichendo
Maneno ake maviṯi, hunuka kama uvundo,
Anenalo ni baruṯi, hualika kwa dhishindo,
Nangalidhaa binṯi, aso na mingi mipindo.

5. Hakuekeki akiba, nivekacho hukijepa,
Michaani ni misiba, huvala paka mifupa,
Kuku wamekuva haba, mbudhi voṯe mivajepa,
Sio angu maṯilaba, hidhi hasara kulipa.

6. Dhishembee saa dhoṯe, hadhikosi nkononi,
   Vala hamuchi ooṯe, jela ni kwake numbani,
   Akikupacha popoṯe, ṯakupoka hadharani,
   Haambiliki loloṯe, mwana huu mwana gani?

7. Andakuva majinuni, kwa uraibu kuvucha,
   Kuṯwa uko igogoni,nyuche ṯele humpicha,
   Hachambui duniyani, bangi dhake akipacha,
   Mwana umo mashakani, Si nadhi huu ni mbacha.

8. Nakuomba ya Jabari, muongodhe huu mwana,
   Awaṯe chake kiburi, haya asifanye ṯena,
   Aepukane na shari, naye ave kama vana,
   Duniya isimghuri, nami nipache kusona.

## Yuru

***Omar M. Maulana***

1. Mii indaharibika, chukubalini
   Vamwichuni vameṯoka, vako miini
   Valivakicha kuṯoka, va masiṯoni

2. Valikuva hucha vachu, yaulidheni
   Yuru kimuona nchu, mbio mwichuni
   Sasa vandakuya kwechu, chuamkeni

3. Yuru ṯachupoka muwi, chuuṯamani
   Chulikuwa hachuyuwi, Echu samani
   Kalama wechu adui, umo nyini

4. Yuru hula dhiwaladi, hachumvoni?
   Mbudhi va kina Hamadi, voṯe dhidhini
   Na hondoo voṯe va  Badi, na Handani

5. Yuru huu hula kuku, giredi wani
   Changu aye kwechu huku, yachungudheni
   Hali ṯena panabuku, hanṯamani

6. Undat̲aganya sihaba, hamuyavoni?
Kumedhawa kina mamba, majabiyani
Mbeu dhimekuwa shaba, kayavudheni

7. Yuru mechuchia hofu, isi nyoyoni
Huzichafuna manofu, yafahamuni
Hakuvekeki sarafu, hazichafuni?

8. Mwanyiva huu yuru, umo n̲yini
Afanyao huchudhuru, muyabaini
Chusinene haidhuru, badilikani

## Posa

***Omar M. Maulana***

1. Nalipoipeka posa, sikut̲arajia kosa,
La habiba kunkosa, kwani pesa sikukosa

2. Babu, ishe vakat̲oka, mwendo uso wa haraka
Ili maneno kupeka, harusi kunit̲akiya

3. Chumekuya vat̲ukufu, kwa moyo vaukundufu
Chwat̲aka kuvaarifu, a harusi kuvambiya

4. Mwana vechu mechuchuma, kuya kwenyu kwa hishima
Kuvapa habari njema, posa yechu kupokeya

5. Mwana huu mwan̲yiva, kwa ilimu undaiva
Na si nt̲onyi wa kuva, nshahara hupokeya

6. Undajenga numba ake, unao mahali pake
Mwana wenyu anveke, vala hamut̲ayut̲iya

7. Vakajibu kwa dharau, mbona mundaisahau
Si inyi kina Famau, Halima kuchuvakiya?

8. Hachulingani kwa sura, si wa kisiwa mbwa bara
Chut̲avodhaye mipura, hachut̲aki chwawambiya

9. Vako t̲ele valosoma, na hat̲a imi hut̲oma
Mwana vechu huichuma, kila mwedhi hupokeya

10. Hiya sasa uko kwapi? Mwenechu huket̲i kwapi?
Nanene sasa simpi, sabiki ndachanguliya

11. Nyaka t̲halat̲hini sasa, na umuri undakwisa
Hayavakwa undat̲usa, hakuna vakumwendeya.

12. Bure walichudhulumu, pendo kulichiya sumu
Mwanavo huwalaumu, ndowa kumuharibiya.

## Usiche

***Omar M. Maulana***

1. Usiche kunena alio a sawa, a sawa kunena usiche ni sawa
Ni sawa maneno alo na usawa, alo na usawa asiche kunena

2. Usiche kunena alo a muruwa, alo na muruwa kunena ni sawa
Kunena ni sawa kujenga muruwa, kujenga muruwa usiche kunena

3. Usiche kunena vachu vat̲ayiva, vachu vat̲ayiva kwa vene kuyiva
Kwa vene kuyiva mamboye huyiva, mamboye kuyiva usiche kunena

4. Usiche kunena alo na mwangadha, alo na mwangadha hachut̲ayaidha
Hachut̲ayaidha akuchuongodha, akuchuongodha usiche kunena

5. Usiche kunena akuchufundisha, akuchufundisha kuchuilimisha
Kuchuilimisha akunufaisha, akunufaisha usiche kunena

6. Usiche kunena akuwakomesha, akuwakomesha ao at̲akwisha
Ao at̲akwisha kuchuhangaisha, kuchuhangaisha usiche kunena

## Rafiki Angu Umari

*Omar M. Maulana*

1. Nndangia uvandani, kuwayudha ikhuwani
   Rafiki alo moyoni, Sifa dhake nibaini

2. Na Umari halingani, yoyoṯe kwene midhani
   Umari ni namba wani, vangine havafanani

3. Umari una imani, si jauri asilani
   Avapenda majirani, Na hukirimu vageni

4. Mikono ake iṯani, Kukuhini kaṯwaani
   Kivanacho ni yakini, Aṯakupa kwa hisani

5. Akiwapo furahani, huṯeka hana kifani
   Apachapo miṯihani, huva hachambulikani

6. Akikuvona ndiyani, ṯakuṯapia mwendani
   Aive muhali gani, Somoe na fadhiluni

7. Sinsifu ni yakini, hana umbo la undani
   Hukwambiya la moyoni, moyo upache amani

8. Ni swahibu wa yakini, imi ndamuamini
   Sina shaka asilani, kukuudhi haṯamani

9. Habari ilo ṉyini, kuwa hufuga majini
   Hilo imi siamini, ni udhushi michaani.

10. Kuva henda ulevini, halingii akilini
    Hapepesuki ndiyani, henda kwa kuimakini

11. La kuichwa kisirani, hilo haṯa silivoni
    Ni njama dha mafaṯani kunchiya haṯiyani

12. Ya Ilahi ya Dayyani, humuombea mwendani
    Umari awe peponi, kwa rehema dha manani

13. Awe iye siṯarani, na vachu vake numbani
    Uvaveke kivulini, na Muhammadi Amini

## SHEṮI KUSHIRIKIANA

*Swaleh Omar Mohamed*

1. Sheṯi kushirikiana, mushikamane pamoya
   Kisha kuhishimiana, kwa mahaba kuwaeya
   Ndipo mambo aṯafana, na mangi kuvaṉokeya.

2. Mungu akivapa vana, muvaee kwa imani
   Mangi kusaidiana, kwa kiṯe na ihsani
   Hondoka alokwandama, mukaishi kwa makini.

3. Pindi munapokosana, ingiapo ṯafauṯi
   Huna budi kupachana, bila kuyudha umaṯi
   Ṯalaka mukipanana, muṯabaki na kuyuṯi.

4. Adabu iṯavapasa, kwa vana kuvafundisha
   Vachambuwe la makosa, vawedhe kurekebisha
   Ivapo muṯapukusa, muṯayafuja maisha.

5. Mambo musifanye siri, paka muaminiane
   Loloṯe lene kujiri, uwadhi uvonekane
   Hamuṯopacha usiri, hamuna budi mufane.

6. Ṯamaṯi kupokedhana, vana vema kuvapemba
   Kwa usiku na nṯana, nimbo njema kudhiimba
   Mambo adhidi kufana, mahaba kuva sambamba.

## TAJIRI NA MASKINI

*Swaleh Omar Mohamed*

| | | |
|---|---|---|
| Ṯajiri: | kamwenge umwiche<br>aye ale mache | nchu aso chake<br>na miva chanoni. |
| Ṯajiri: | mkacha hayisi<br>akanda kulasi | kula na nkasi<br>hulia kiṯwani. |
| Masikini: | ungaya kunicha<br>ninwee mafucha | nail nimekucha<br>ṯele kikombeni. |

| | | |
|---|---|---|
| Masikini: | nkacha ni noka<br>kwa vake ukacha | ndrudhe humwepuka<br>na umasikini. |
| Masikini: | nkacha ni kidha<br>angaishikidha | endapo husodha<br>hachambulikani. |
| Masikini: | nkacha si muchu<br>angava sharifu | akusapo kichu<br>hana buruhani. |

## Amani

***Khalid Omar Kanjenje***

1. Enyi ndudhangu Bajuni, kunena nanyi naṯaka
   Muyachie akilini, niṯakayo kuṯanka
   Chudumisheni amani, chupaṯe kusiṯirika.

2. Amani kichu muhimu, kwa wadhee na kwa vana
   Chuṯukueni jukumu, na suṯe kuhimidhana
   Malengo echu yaṯimu, kwa uwedho warabana.

3. Kiwa hachuna amani, ni shida ziṯachungia
   Hachuṯokeṯi numbani, kwa makini kuchulia
   Chuṯakuwa dhishindoni, bila ya kufikiria.

4. Amani mimi na wewe, ndio wa kuidumisha
   Kwa makini na chuchue, ukweli nawajulisha
   Shidani na chujiṯoe, yawe madhuri maisha.

5. Amani kichu awali, chukiwa nayo miini
   Vanawake na wavuli, suṯe chushikamaneni
   Kabisa chusikubali, nchu kuvunda amani.

6. Ṯamaṯi chudumisheni, amani kwechu muhimu
   Vala chusiichieni, kwene dhiṯa mahashumu
   Suṯe chushikamaneni, malengo yechu yaṯimu.

## Mausiyano

***Mzee Athman Shee***

1. Huadhimiya safari, baharini kuingiya
   Kuṯafudha ṯaisiri, a mikondro a duniya
   Avuke kwa ushuwari, kwa endrapo kupakiya.

2. Huiṯafudha ingwe, nakodhimo akuchiya
   Kwa siri alengwe, mwenye swiha na afiya
   Michengani afungwe, aye kuvaecheya.

3. Huvinda mangi masaa, na masiku enye kidha
   Ṯena bila kupumbaa, ndiya akidhiongodha
   Huṯoka pasi na ṯaa, alomaṯi kumuekedha.

4. Hunshika wakueya, nama wakuridhiya
   Numbani kavaecheya, kanga asokimbiya
   Wa maingi kuvachiya, na vana wakuvaeya.

5. Hundhegeya ndhuri, umbile la kuvuchiya
   Mwene ngaro wahariri, sifa dhilidhoṯimiya
   Ndripo hukacha shauri, dhamira kuifikiya.

6. Huṯokedha muangadha, nuru njema ikangiya
   Vahenga vakaeledha, valiyo a kusudiya
   Midirara kuovedha, baraka dhikadhukiya.

## Amani

***Mzee Athman Shee***

1. Eo naṯaka ṯamka, kuvausiya vendani
   Kuna yambo la hakika, chuvekani akilini
   Lulu ikichumbirika, si marudio shadhani.

2. Nfano nimeubika, muelewe ikhiwani
   Ni yambo la uhakika, aṯaka chuve makini
   Lulu ikichumbirika, si marudio shadhani.

3. Hunena na vachu vangu, valo kwechu Bajunini
Venye damu a kwaangu, i<u>t</u>okawo mifupani
Lulu enye damu angu, haikurudi shadhani.

4. Ni lulu ilisofika, inaong'ara kidhani
Ina sifa dha hakika, dhiso fi<u>t</u>ika ma<u>t</u>oni
Hadhari ikimbirika, si marudio shadhani.

5. Ina samani hakika, na mangi ma<u>t</u>umaini
Ni vangi chunai<u>t</u>aka, hui<u>t</u>afudha michoni
Chukikosa kuishika, si marudio shadhani.

6. Lulu muliyoipacha, sifa dhenee miyini
Afuweni chumepacha, chumeona <u>t</u>umaini
Apichao kiokocha, si marudio shadhani.

## Umoya ni nguvu na upendo wa daima

***Fahad Mahadhi Kombo***

1. Haukuveko umimi, vachu va mui mmoya
Haikusikiwa yomi, nsiba kimfikiya
Huya vavili kwa kumi, ili kunsaidiya.

2. Li<u>t</u>okeapo la kwava, vachu valikiivana
Usiku ulivokuva, na hali za vao vana
Wakifanya kwa kuyiva, undugu si kufanana.

3. N<u>t</u>ikachi kuliliwa, kichoveo <u>n</u>umba ndhima
Na jirani kupekewa, uchupu vasile sima
Ha<u>t</u>a kichache elewa, hukudha <u>t</u>abia njema.

4. Baada dhavo shuhi, siku ndhima ivani
Kifunga dho<u>t</u>e amali, <u>t</u>avapacha dhikaoni
Huambidhana kauli, au hu<u>t</u>edha bavoni.

5. Mmoya akiamuwa, ku<u>t</u>aka kujenga ake
<u>N</u>umba hio i<u>t</u>akuwa, vajenge rafiki dhake
Vae kumpa afuwa, hadi agurie kwake.

6. Kuni vaṯankachia, alo na harusi ake
Mayi vaṯanchilia, kwa shangwe dhavo majike
Kikango vaṯachangia, nchu kwa uwedho wake.

## Maelewano

***Fahad Mahadhi Kombo***

1. Vaishipo kwa umoya, rijali navo nisai
Kwa mapendi huchuliya, kwa pendo lenye uhai
Huishi pasi udhiya, Vakachulia na mui.

2. Vanaume ni nsada, kwa nduzavo vanavake
Rabi ondoa husuda, maovu asivafike
Dhendelee hidhi ada, siku dhoṯe vasichoke.

3. Hishima avo mabinṯi, medhibiṯiwa sihaba
Hafanyiwi usheraṯi, na vahuni vasohiba
Huva avo mahabaṯi, hupawa hadi hushiba.

4. Hushadidi urafiki, pasipo na mbovu nia
Vakaishi bila chuki, kwa nyedhi na nyaka pia
Uṯadhani ni ashiki, pale ukiivonea.

5. Mipaka a vanaume, iwadhi kwa vanavake
Sivo vale pakashume, kula dhisidho dha kwake
Hava ndivo vafalume, hulinda pasiomoke.

6. Uṯangamano huanda, kwa kuandaliwa posa
Yambo dhuri la kupenda, la ndoa bila hamasa
Nvuli hupawa mwenda, aishi naye kipusa.

## Shere Lindaecha Ṯabu

*Zuwena Ahmed Mohamed*

1. Kuna ṯabia dha vachu, huchufanya ṯaabani
   Huveledha vene kwechu, ṯena bila samahani
   Munenapo na ndrudhechu, mambo a shere aṯani

2. Husifika sana kwechu, nalipodhawa Rasini
   Havanisadiki vachu, vangi havaniamini
   Kila kivambia kichu, huva havakiṯamini

3. Si ladhima kila kichu, chupange shere jamani
   Kheri ṯapasa usichu, au nendra makuchini
   Lakini shere kwa vachu, chuaṯe vene Rasini

4. Sineni ni kila nchu, va kukuyiva ni nyani?
   Mara huechewa dhichu, ndridho hidhi ukadhani
   Hwambiwa ulie chuchu, nave buru huivoni

5. Uovu wa hichi kichu, cha urongo jamanini.
   Husadikiwi na vachu, haṯa kivambia nini.
   Hwichwa la shere ijichu, yapo hunena yakini

6. Ṯakoma hapa mwenechu, kalamu ṯaveka ṯini
   Hela nawe fanya uchu, ndrudhako usivakhini
   Likomeke shere kwechu, vageni vachuamini

## Kuifurahisha

*Zuwena Ahmed Mohamed*

1. Furahi hukudhiviwa, vala kuifurahisha
   Lakini madhangaṯiwa, ni bora ṯakuyivisha
   Ulioharamishiwa, sendre kuikurubisha
   Siandame nshawasha, va alielaaniwa

2. Hakuchudhiki Moliwa, bali mechuneemesha
   Mangi chumejaaliwa, madhuri mechuegesha
   Kwa chuloharamishiwa, kifanya huchukondresha
   Usiku huchukesesha, na ruhu dhikashukiwa

3. A hoko chwalovekewa, ni ṯamu isiokwisha
Ueledhwapo elewa, uande kuṯayarisha
Dha duniya mehadawa, dhina mwisho vake hwisha
Peponi ndrio maisha, hadhishi hudhidishiwa

4. Kivumbe kifanikiwa, kushukuru hudhidisha.
Na lau akisibiwa, subira kuṯosichisha.
Mara aṯachachukiwa, faraja kwake kubisha.
Mola hunfurahisha, na kwingi kafanikiwa.

5. Sheṯwani kichusumbuwa, ruhu kichuṯamanisha.
Mikono angu ṯanyuwa, kwako kuikurubisha.
Asubuhi kininyuwa, na usiku kinifisha.
Siku uhai ukisha, palipo pema kuchiwa.

6. Ṯamaṯi hapa ṯachuwa, shairi lipache kwisha.
Wadhi nimeafunuwa, mambo sikuabakisha.
Mwenewe ṯapambanuwa, uaandame ukisha.
Kisa huifurahisha, siiṯakie baluwa.

## Masaibu

*Zuwena Ahmed Mohamed*

1. Ghafula haelewani, abawa na nke wake.
La kuchendra halivoni, ina dhiki ruhu ake.
Hana raha asilani, wala uchulivu kwake.

2. Unvonapo ndiani, abawa hunena pweke.
Na haṯa nsikichini, hachulii na ndrudhake.
Imenchandra hudhuni, medhoofu mwili wake.

3. Linikeree moyoni, mpaka nendee kwake.
Nami niyive kiini, a hidhi balaa dhake.
Nke kanveka ṯini, ili suluhu iṯoke.

4. Kamba hayisi ni nini, hoo pia nke wake.
Na hana mimba hanani, hachuyisi chando chake.
Kwamba havaelevani, mebakiya na upweke.

5. Ndriposa kakeṯi ṯini, kachungudha mambo ake.
   Huveka michandraoni, picha dha kishuna chake.
   Ni hasadi kwa yakini, indanngilia kwake.

6. Ndrudhangu nachuombeni, achengee mambo ake.
   Kisha chudhingaṯieni, chuifundre kichu kwake.
   Hasadi nachudhicheni, na mambo echu anoke.

## Uchudhie Wangu Moyo

***Zuwena Ahmed Mohamed***

1. Kwene urongo na kweli, hulichudha langu bongo.
   Nsimamo sibadili, kipofu ḵamwicha ṯongo.
   Pene madhimbi makali, ndripo ulipo nlango.

2. Bahari ivapo ḵali, imi sifanyi nṯango.
   Huomba Mola sahali, niṯimidhe langu lengo.
   Kwake ngeudha hali, nja hafanyi mashingo.

3. Kupacha ḵwake Jalali, si sharuṯi nlolongo.
   Ridhiki ilo halali, hukupa pasi nchango.
   Kwake ukiṯawakali, hukuyadhia kikango.

4. Vangapi haṯa sikuli, havakuvona ṉjengo.
   Vana raha kweli kweli, kama nyusi dha kifungo.
   Na alosoma hayali, hayauvona mpango?

5. Kukosa sio kufeli, ridhiki ni nviringo.
   Kupacha sio kunali, hidho pumba dha vuongo.
   Shukuru kwa kula hali, uiṉoe ako shingo.

6. Mwisho wa shairi hili, nilochunga kwa mpango.
   Niya usiibadili, uuvonapo nlango.
   Wa moya havai mbili, pia si kama igango.

## Miftahi

***Hassan Msham Mahmoud***

1. Ya faṯahi ya radhaki, Mola na kuchambaliya
   Nichilia ṯaufiki, niwedhe kuendeleya
   Mwene haki mpe haki, kwa baraka dha Nabiya

2. Nichambaavo Jalali, ṯaka kukuṯaradhiya
   Kwa baraka dha Rasuli, Mola niṯakabaliya
   Chwandolee mashakili, na balaya dha duniya

3. Mola vangu jabaruṯi, iṯani nimeinyuwa
   Wala sina hasanaṯi, kuwedha kukuongowa
   Chupe nasi harakaṯi, kwa baraka dha Rasuwa

4. Niko nlangoni kwako, nakubishia dayani
   Kwa ṯwaa na sikiṯiko, unichie kabulini
   Chwandolee maudhiko, kwa baraka dha amini

5. Mola uwe ni ṯajiri, usie na madharau
   Vapenda kuifakhiri, na ahadi husau chupe
   Maisha huwa madhuri, kwa dhema dha ulamau

6. Hapa niko ukingoni, nakhiṯimisha maombi
   Chungo hini ya Hassani, nakoma mbee siimbi
   Nakuomba Rahamani, chuepuse na dhiṯimbi

## Umoya

***Hassan Msham Mahmoud***

1. Naanda kuvaedheya, kwa maneno anenao
   Mwando wa muchu kudhiya, ni kuidha ambiwao
   Ṯaaṯhiri dha umoya, hudhaa maendeleo

2. Ndudhangu navaambiya, kwa hamumu na ṯhabaṯi
   Haina mwen'e duniya, chuvadhe sana mauṯi
   Mahala peṉe umoya, huṯimbuka hasanaṯi

3. Chuvasome Manabiya, valivo na utatuvu
Kwa ibada na twabiya, valikuva vaekevu
Chukiva vachu vamoya, mii itapacha nguvu

4. Vachu valochanguliya, valiketi kwa muruwa
Sana vakisaidiya, tena bila kubaguwa
Chukishikana pamoya, hachuwedhi kutedhewa

5. Sura ninenavo hiya, shakili limenishika
Nanyi vene kusikiya, andani kubadilika
Chukiukudha umoya, chutadhidi kufunuka

6. Mwisho hunu nauchaya, basi kuvaburudisha
Ikiva nimekoseya, siidhi kurekebisha
Walakini la umoya, huchengenedha maisha

## Mwando va mashindano

*Hassan Msham Mahmoud*

1. Nalianda kushindana, kwene mashindano mingi
Nikafanyiwa hiyana, ikava kama sichungi
Eo nashindana tena, kwa dhifusi na dhigingi

2. Na mwando va mashindano, sikufanyiwa usawa
Nilitujiwa maneno, valokosa kuchambuwa
Naliambiwa sindano, haitibu bila dawa

3. Mwando va mashindanoni, vashindani valikiri
Valinena Kibajuni, amechunga kihodari
Walakini vatahini, valinipoka nambari

4. Japo nashindana eo, nashindania ilimu
Nivone mipangilio, ya vachu vataalamu
Naveka maadhimio, malengo angu yatimu

5. Mashindano kula mara, nikishindana sishindi
Hudhidi kuva na ghera, vala daraja sipandi
Kubadili mbinu bora, nami nipache ushindi

6. Mwisho kushindana kwangu, nimeinyua iṯani
Kumuomba Bwana Mungu, anipe naloṯamani
Kwa sababu valimwengu, hawana ṯena imani.

## Maisha A Kila Siku

*Jamila Ali Haji*

1. Mamboe husikiṯisha, ukichia akilini
Chuaishio maisha, heri a kae dhamani
Nyakaṯi dha kula wisha, na chondo dha ufuoni

2. Kula chondo na miṯimbi, vadhee validhoveya
Na bodo wavo wa wimbi, na miṯasi a Kambaya
Eo hula dha madhambi, dha kuchudhuru afiya

3. Valo vakiula wisha, na mayi a madhivani
Havakuva na presha, wala sukari mwilini
Va eo na vakisasa, hali dhavo ṯaabani

4. Hava valavo dha sasa, vaangisievo hamu
Huṯilifika mapesa, kwa ndisa dhilidho ṯamu
Maudhiko huvachesa, apimwao hana damu

5. Kwavo mekuva maudhi, kwa ugumu wa maisha
Ameshiṯadi maradhi, dhivumbe huhangaisha
Huvoni la kukuridhi, moyo kuusahilisha

6. Na vana vandachuvua, mabongo aṯawaliwa
Dhilevi huvasumbua, ivo vene huivuwa
Rabi ṯachubadilia, achupe enye usawa

# Nlango a Pili: Maweedha

## VUNGA

*Abdalla Ali*

1. Undachumalidha vunga
Hasara dhindachudhonga
Vana usiku hudhinga
Ivo kujepa hupanga
Huyala kwenye ntanga
Ruhu dhechu huchutanga

2. Kuna na hiyo tumbaku
Dhitwa dhavo kama kuku
Si ntana si usiku
Chunakuomba Maliku
Chukenda huku na huku

3. Madawa yana balaa
Halele na mogokaa
Chumekosa pakukaa
Huchafuna kila saa
Vana vechu ni dhishaa

4. Dhibugidhi nadho piya
Pweke yavo husindiya
Ukivavona taliya
Sindano dhakudungiya
Na chumuombe Jaliya
Huvona vote hungiya
Na tayari kuichiya

5. Chundadhiveka rahani
Ili chuvatoe ndani
Bwana Mungu mbwaulani
Chundakuva masikini
Umeyaa michaani
Mola wechu chuawini

6. Madawa haya ni sumu
Vadoda paka makamu
Dhimepunguwa nidhamu
Hudhisuwa dhavo damu
Vandakuva kama gamu

7. Uloingiya miini
Hakuna tena amani
Mayaa na mapipani
Hata haya havavoni
Vangine dhibaradhani
Lakufanya hachuvoni

8. Husokotwa hadharani
Mache tele ndomoni
Havachoki asilani
Uchuveke nusurani
Vana chuvahurumieni

9. Haya vanaochumiya
Mifukoni vakichiya
Dharubu dhindachungiya
Hasara ndachudhidiya
Kwa madawa kuchumiya

10. Hudhiyadha ndomoni
Hoko kwavo masikani
Kwa janga hili jamani
Vakichiya misipani
Achuchie nusurani
Vana dhisu nkononi
Havajali masikini

11. Dhahabu na numba dhechu
Kukombowa vana vechu
Vunga huu ulo kwechu
Ndakwisha imani yechu
Huliwa na kila nchu
Vachuliye valovechu

12. Hili nanena kwa dhati
Kila saa na wakati
Vashikalo havaati
Usiku na ntikachi
Kuvasumbuwa umati.

## Vadhani Vakiwaiyu

***Mohamed M. Kombo***

1. Kiwaiyu nalipo nyukia
   Maisha nalo ashuhud'ia
   Ali ninjema kwechu d'unia
   Malimwengu chukiafurahia

2. Ubinad'amu ulikuveko
   Undrugu haukuva maudhiko
   Uswahibu haukuvund'a miko
   Utamad'uni ulipawa mashiko

3. Vachu vechu valipend'ana
   Kwa mangi n'yini valisaid'iana
   Kwa harusi nakifo havakuatana
   Kwa raha nasumbuko valiyivana

4. Chwalidhungukwa na nema, kila aina
   Ntia, marukatwa, na kh'afu chukavuna
   Dhiboma vatonyi havakudhanyiana
   N'ama dhakasa nanguva chukiavanyiana

5. Chukivind'a kh'ungu vakipachikana
   Ajaliwao fungu chukikumbukana
   Dhikuni, mai,mocho chukipanana
   Kwa ruhu safi kinyongo hakuna

6. Chukipanana ch'eche dhabishee
   Pia wimbi, buru, kundre na mavee
   Machikichi na machanga aenedhee
   Eo dhote hidhi hakuna dhipotedhee

7. Chombo chali chikendra safari
   Hakulipa ipeni kila alokuva nsafiri
   Mana alind'echu isi vote bahari
   Na chombo ch'andruechu n'dhuri

8. Hachukuva matajiri vapesa
   Wala van'umba dhakisasa
   Lakini maisha haakuchuchesa
   Kuva ruhu chwalidhichakasa

9. Langu imi ndruo lalikuva lako
Lako halikuva lako pweke ako
Yapo haakukosekana maudhiko
Kuyivana halikuva sumbuko

10. Harusi ndrudhangu ali nd'an'yi n'dhima
Haukulipwa upishi wala kutedha ngoma
Chukialikana kwa furaha na kuterema
Chukitangamana vana na vachu vadhima.

11. Akiwaa mmoya wechu n'yini
Akiwadhwa nasi vote kijijini
Ven'e kupeka mai na kh'uni
Ntabibu malipo hakutamani

12. Afapo nchu n'yini, kikh'etiwa machanga
Vangine vakipeka kichoveo, vangine vunga
Vakipikiwa ven'e nsiba, vasipache kutanga
Ama chakula kuechewa, ruhuma kudhijenga

13. Maiti hadhikwi, majirani vaongojewe
Apekwe mwana Chandrani, vaambiwe
Endre na kitangani, va Nkokoni vaviliwe
Kendre chombo, Nd'au vasisahauliwe

14. Mwana akikosa ad'abu vaongwana
Akikemewa nanchu n'dhima alonvona
Vadhadhi van'yi vote vakiaminiana
Na hishima kwa umoya vakivekeana

15. Nchu akijenga n'umba vend'ani
Akisaid'iwa na vote valo n'yini
Wiki mbili achachu hungia ndrani
Haukuva na udhicho umasikini

16. Mama akishikwa na utungu, chukiichana
Vaume kwa vake, ndrani naind'e kud'irikana
Kupokewa n'geni wechu, akidhawa mwana
Mbwechu isi pia, kwafuraha chukiambiana

17. Haa aliendrelea kwa muda nrefu
Miyi echu ote ilikuva mitukufu
Hakuna kwavo alo kukashifu
Chwendrapo chukiva dhiraufu

18. Mpaka n'gavanyiko ulipo kuya
Kwa mikono mivili chukaupokeya
Undrugu na umoya dhikapoteya
Chukabaki huliya mwana huliya

19. Usaliwa na mayuto mwana huliya
Angafucha ushingo humwambiya
Mayuto ni n'yukuu bankuu alinambiya
Unacho chembe, moyoni kimen'ngiya

20. Unacho chembe unacho
Ndrudhangu simachocho
Ndruo hukuchilia mocho
N'umba ivake usibaki uficho

21. Musinivudhe imi kuveeye
Kh'inena alivo musinitukiye
Ni imani chulimbiridhiye
N'ongo ruhu idhitawaliye

22. Nyoyo dhalipo kosa imani
Uchu nao ulitolewa samani
Kakosa kuchambuliwa hisani
Akapawa nguvu a ushetwani

23. Uwaminifu ukakosekana
Hachukemeani tena vana
Kin'dara wako chutavuana
Mana wangu siwako tena

24. Kujepa ikava nikuerevuka
Widhi ukapacha kusifika
Kunyang'anya kakubalika
Ndripo mambo kubad'ilika

25. Ukweli chukacha kutamuka
Urongo kwechu ukakubalika
Utukivu ndripo chukautaka
Ch'uki nao ipaa kalichia tuka

26. Vana siasa vakachuchechesha
Machifu akili vakachudhungusha
Kujepeana akava echu maisha
Ushetwani baraka kadhirambisha

27. Chuangalini eo kwechu chulivo
Uhasid'i ndrio uchuchidhie muevo
Umeenedha dhichundru dha mbuvo
N'oki nchengedha asali hana bavo

28. Mwanad'amu nialo chumia akili
Madhuri en'e faid'a akaakubali
Nishetwani apend'eleyao batili
Maovu na Kuvund'a kufanya asijali

29. Sumbwi na sulisuli,vali vaenedhee
Nguru na Ph'andru dhama dhilee
Mbona Kiwaiyu hachukutokea mbee
Na baraka dhali kwechu dhienee?

30. Hachukujenga majumba
Hachukubuni mashamba
Chwalibakiwa na mafumba
Magomeni kuhisabu namba

31. Haa ndrudhangu chuadhingatieni
Palipo haribika chuchengedheni
Imani na upend'o chudhichwaeni
Uwaminifu nakueleana chutakeni

32. Ugonjwa hutibiwa ukiyivikana
Palee ntabibu nvilini akiuvona
Ndrio imi haa nnenao kuanena
Kuitibu chupache kusaid'iana

33. Mana isi Vakiwaiyu nvagonjwa
Vakutuviwa d’awa nakuchanjwa
Aakh’iyao ichonge husongwa
Aand’amao nd’ia hutevengwa

34. Eo hachutakiani tena mema
Humfanyia kiito apachao nema
Huand’amana kwa dhitimbi d’aima
Hachubagui vana kwa vachu vadhima

35. Th’anena alioko munene huchukana
Kama hidhi nyendro hachutadhiviana
Yivani chutakuva samaki chutalana
Kiwaiyu kwechu ichutawale lana

36. Jamani chuchendrao kwechu n’yini
N’nyani mmoya wechu aso kaavoni?
Huombana mikopo chusilipane d’eni
Kwa kukosa haya chukaifanya vaneni

37. Sikuva imi kwechu nikutukie
Hunena alioko chuwafikirie
Kwa udhicho chuadhingatie
Mana avao aibu anichidhie

38. Nchu hatukii kwavo
Kuve kuovu kuvavo
Mana kh’wavo kulivo
Kwa vachu sikwavo

39. Nchu kwavo haiyidhi
Yapo aveko akumuudhi
Wala sababu hatafudhi
Kukuyidha ni upudhi

40. Nchu kupend’a kwavo hachoki
Hata kama nkweli hakukaliki
Yambo la kuitukia halikubaliki
Kiondra nvilini hakiambuki

41. Kwechu ni kwechu chwakupend’a
Yapo kuketi kimaisha huchushindra
Hachuengi kwa mbali kukivund’a
Chuate kudhiokowa dhechu nyond’a

42. Nikipend’i chechu Jazra
Nyoyoni katu haitagura
Kwa faid’a na kwa hasara
Kuilindra niechu dharura

43. Nimuhibu wechu Nd’odhi
Nyoyoni katu haivodhi
Ungachutukidha upudhi
Kuilindra kwechu nifaradhi

44. Lakini yambo imoya chulifahamuni
Tena hili chulichieni sana akilini
Afapo kivumbe nvili huvoa kaburini
Ruhu endrapo ayivao Mmanani

45. Vachu huovowana vakikubaliana
Vakikosa kuelewana huwatana
Harusi nisherehe vaongwana
Talaka ni nsiba chund’aelewana?

46. Najamii hukund’uka vakipend’ana
Hukund’ika ivapo vatatukiana
Huva na nguvu umoya kipachikana
Huva dhaifu ivapo vatatengana

47. Chuiyengeni chulivo venechu
Isi sidhiboye ndrudhangu nvachu
Uko chwalokuva nao wechu uchu?
Und’akosa samani kwaajili adhichu

48. Kama isi kwa isi hachusikidhani
Hachujaliani mema hachutakiani
Hachupend’ani hachuhishimiani
Ad’ui akiya tandhivia n’nyani?

49. Chwalikuva ni simba hoko dhamani
Eo niph’aka hukimbia kuisita kidhani
Vaongwana chwaloyivikana Bajunini
Eo mila akichwana ndrio huisamini

50. Uchwana sirangi sikabila
Si Nsanyi, M’boni wala N’gala
Sikidhadhi siukoo wala wala
Vadhee valinena nikuata mila

51. Chuchungudheni chuishivo
Chuengeni kwechu eo chulivo
Si Kiwaiyu tu mambo akeevo
Bajunini chwalivo kuva eo sivo

52. Kisha huketi chukalia
Maisha and’achuemea
Sababu chund’aifikiria?
Haikusitamana chambua

53. Mifano iko tele haikukosekana
Wala isi sitongo kukosa kuivona
Chusikasirikianeni chukivonyana
Chubad’ilikeni ndrilo la maana

54. Mashamba a minadhi ako
Na amibibo pia alikuveko
Nd’a marika gani hii mikh’o
Echu niipi rika langu na lako?

55. Hushindrana dhitimbi na ch’uki
Kutukiana, kutongeana na unafiki
Kudharauana sindrugu simarafiki
Kisha nkweli dhiki hachudhitaki?

56. Musinene n’dhungu uyie kuvachukana
Ama kuva nind’akuva nakiburi huivona
Udhunguni hupokwa wangu uwongwana
Hudharauliwa kisha kh’aichwa nchwana

57. Hakuna wakukuchambuwa
Kama huichambui abawa
Ndriwe hadhi ako taichafuwa
Na ndriwe utaiyata kuvowa

58. Umbula hakuna atakae kukuhishimu
Kama samani ako uwe huifahamu
Ukaata kuuchambuwa ubinad'amu
Ukaand'ama dhilo mbovu hukumu

59. M'bajuni kikuu huikuwa kwavo
Ndrivo vaongwana vanenavo
Ni nshipini kiyivikanapo kiovo
Nkisimani lichambuliwapo idovo

60. Ph'embe humea kitwani
Kh'acho humea maguuni
Kisinga humea kishurini
Ndrudhangu chusisahauni

61. Imi Mad'isomo Kiwaiyu nalidhawa
Ndripo kwechu niwedhapo kuikuwa
Kukiharibika maudhiko hunivuwa
Kukichengea ruhu angu huchuwa

62. Sivambii in'i nnenao,imi kh'aitowa
Nimo nkaoni kama ubuva na kivuwa
Nd'echu isivote jukumu kulitukuwa
Aulimini husukia machumboni abawa

63. Niishi niishivo udhunguni
Sivi n'dhungu hili fahamuni
Ndrio hudhid'i kuva M'bajuni
Mana naichambuwa imi n'nyani

64. Kwechu kisiwani kund'aharibika
Chukiata kunena haataandroka
Maovu n'yini and'ao kusanyika
Dhidhadhi pia dhind'akh'achika

65. Ndrio ndrudhangu mukavona
Aandrokao harud'i n'ima tena
Chund'aivudha nnini mabwana?
Huvavudha nan'i pia kina nana

66. Salaalah Muhamadi wasallimu
Chund'akuvae isi vanad'amu?
Niikundru vakavaka madhimu
Chuleni haki dhavachu ntamu!

67. Ndrugu na ndrugu hutukiana
Na maovu vakasumbikidhana
Kwa ajili anini,chund'avulidhana?
Kukosekene imani nakupend'ana

68. Hun'yiva ndruo ikuyiapo shid'a
Palee sasa utakapo kwake nsad'a
Kama huna haja kunkumbuka nilabud'a
Huvavudha haa nimaisha vanwa soda?

69. Ndrugu vakiyivana huchuudhi
Vakipend'ana isi haichupend'edhi
Vakishirikiana hutukia ph'apadhi
Huu mmwendro gani hachuivudhi?

70. Vangine vatanena sisi vote jamani
Chupend'ao huu ulioko ushetwani
Lakini uwe ndruwangu nihatuwa gani
Utukudhieo kuupinga huu uhuni?

71. Alioko kipund'uni vumbi nladhima
Kama huneni kukanya alioko akakoma
Hupudha ukauwata kuendrelea ujoma
Basi yiva uwe nikiboye chanchama

72. Ukinvona ndruo hufanya nawe katamani
Kuntukia nakunfanyia uhasid'i niud'uni
Kikuchia sikitiko ukafanya hudhuni
Kuva huna uwedho,basi chufanye nini?

73. Chuichaneni chudhungumudheni
Mavadho bora naakili chupananeni
Chupange masikini nsad'a chumpeni
Dhiandroke dhinyongo na hudhuni

74. Haa kuva niladhima umoya upachikane
Chuve vaaminifu navakweli chuwaminiane
Ruhu ndrani dhichakasike, ndrio n'yi ufane
Dhandroke dhitimbi,uhasid'i ukosekane

75. Nd'ia dhiko tele dhakuchusaid'ia
Chutadhivona, ubinafusi chukiudhivia
Pia utengano nafasi chukiukachalia
Basi palipo na nia, haikosekani nd'ia

76. Chukiva na nia moya
Chukava nasafi niya
Mambo atachengeya
Madhuri kuchuiya

77. Ivapo chutasikidhana
Kwa umoya kuelewana
Uwaminifu ukapachikana
Mangi kuva tawedhekana

78. Dhikipend'edha huruma
Namadharau nao akakoma
Ukafukudhwa n'yini unyama
Dhitarud'i tena kwechu nema

79. Ukichambuliwa ubinad'amu
Nakila haki anchu ikava sumu
D'ini a Mungu ikava hakimu
Ataandroka ote madhulumu

80. Ukweli chukiambiana
Chukaata nyuso kuchana
Alo nkosa haki akaivona
Utukivu utakosekana

81. Kinyongo kitaondroka
Aisitiyeo wadhii atafunuka
Kusameheana chutataka
Ndrio n'yini dhiye baraka

82. Nguvo ikingia ongo hufuliwa
Kwa jiki na sabuni husuguliwa
Mapaku na uchafu kutolewa
Ndrio kupend'edha ikivawa

83. Mana uchafu hutukidha
Na ongo nguvo huvodha
Ndrio haa basi kh'aveledha
Usafi upache kupend'edha

84. Mbwa moyo unadhifu ulo bora
Nikupao wanguvo nimfano Jazra
Ongo na mapaku ni widhi na ukora
Havi mwerevu apend'eleyao ujura

85. Nchu hakachai mwicho Bulo
Bali hukachaa aambiwalo
Akapinga iyovu afanyiwalo
Akaunga lema aechewalo

86. Langu ineno lind'akoma hapa
Mund'aokuva miteva na mipapa
Basi nilani musibakishe mfupa
Kama nneneo faid'a haakuvapa

87. Lakini lamwisho huvambia
Haa maneno yivani atabakia
Dhitabuni atakuva historia
Dhidhadhi dhiyadho kuasikia

88. Imi navapend'a nno ndrudhangu
Ayivao nafusini mwangu ni Mungu
Kiwaiyu ndrio ulimwengu wangu
Nan'i vakiwaiyu vote mbangu.

## Dunia si mbaya

*Mohamed M. Kombo*

1. Haloo rafiki-d'unia simbaya
Ingava hutaki- haa kuwasikiya
M'baya ndriwe-dhichuko hufanya
Vaja kukutaya-d'unia simbaya

2. Chunyukeni-chuateni makusud'i
Hachuvoni-sasa kilo kind'adhid'i
Chusisahauni-kuva yana haiṯarud'i
Navambia ndrudha-simbaya d'unia

3. Ukichendra-asokuva namaana
Ṯakuchandra-maovu kila namuna
Mwisho tendra-usumbufu kuuvona
Hukwambia ndruwa-simbaya d'unia

4. Ngoja nikweledhe-d'unia simbaya
Nikweledhe tena-upache kusikiya
M'baya ndriwe-dhichuko hufanya
Vaja kukutaya-d'unia simbaya

5. Fikiria-upime dhako dhichendro
Dhingatia-maovu ana magendro
Hii d'unia-simahali adhishindro
Hukwambia ndruwa-simbaya d'unia

6. Uchendrao-dhingatia kivumbe
Upend'ao-asikudhuru Yumbe
Maso ashikao-hunkacha wembe
Hukwambia ndruwa-simbaya d'unia

7. Nisikidha sana-d'unia simbaya
Nisikidha tena-hili hukwambiya
M'baya ndriwe-dhichuko hufanya
Vaja kukutaya-d'unia simbaya

8. Ulimacho-ndrio ako mavuno
Vuwa mato-uwivone mifano
Bila mocho-hapikiki ph'ono
Hukwambia ndruwa-simbaya d'unia

9. Kila yambo-huya nasababu
Sidhiungo-siph’epo dhamaibu
Kuva lengo-nikukuvelea wajibu
Hukwambia ndruwa-simbaya d’unia

10. Haloo rafiki-d’unia simbaya
Ungavona dhiki-d’unia simbaya
M’baya ndriwe-dhichuko hufanya
Vaja kukutaya-d’unia simbaya.

## Maweedha Muyashike

***Quswai Sufiyani***

1. Eo nataka kunena, maneno ya tankini
Kuwausia dhijana, na mahavule wendani
Naomba kufuachana, hadi mwisho kikomoni
Ya sawa kufundishana, a dini a dunia

2. Kihavule alo bora, hutunga ake hishima
Kailadhimu sitara, kaifanya ni ladhima
Asiiate papara, mwiso vatu takusema
Ulinde na ubikira, afurahi vako mama

3. Nguo dhiwe dha sitara, dha adabu na hishima
Na yambo la kudhurura, ndio mwando wa kuduma
Mwari hapendwi kwa sura, vala kwa ake neema
Hupendwa tabia bora, mwene mila na hishima

4. Hata na inyi dhijana, yapaswa muihishimu
Kula unayenvona, ushasimamisha damu
Mulao na kuchafuna, chungeni musile sumu
Dhiwaandame na lana, na kwa mola majukumu

5. Kwa makini tafakari, haya nilovaambia
Yafaa kutahadhari, ni ndhunguko dunia
Va vatu ukihasiri, miguu huchekechea
Vala hili sio siri, chumewahi shuhudia

6. Siṯoi ṯena kauli, keṯini muṯafakari
Kwa haa angu kalili, muyashike kwa udhuri
Mungaionda asali, mwisho ṯaonda shubiri
Va mwendio unjali, uive kunsiṯiri

## Mwanangu Ishi kwa Wema

***Famau Ali Famau***

1. Awali Mola Karima, inale nachangulidha
Madhicho yalochwegema, ilahi ndiwe muwedha
Chuondoshee nakama, baraka kudhisogedha.

2. Mwanangu ishi kwa wema, kwa ndudho uṯapendedha
Usipende uhasama, wa dhicha kuzichokodha
Uṯaipacha lawama, na mbee huṯoongodha.

3. Hishimu baba na mama, na familia kukudha
Pia na vachu vadhima, usive ṯavaṯukidha
Uṯaipacha neema, na wema hauṯoodha.

4. Shaṯi uve mwana mwema, uṯangamane na ndudho
Ukarimu ni ladhima, vendiyo kuvafanyidha
Wala usirudi nyuma, kwa vachu uṯaṯukidha.

5. Ibada ake Karima, aula kuliṯimidha
Bwana Mola ni Rahima, ni bora kunṯukudha
Oṯe maadili mema, wafaa kuyaṯimidha.

6. Ṯamaṯi imi hukoma, beṯi siṯa nafupidha
Una maadili mema, na ukarimu faidha
Mekujalia karima, kiombwa huwedhi idha.

## Maweedha kwa Dhijana

***Famau Ali Famau***

1. Nashukuru Maulana, kunipa nafasi hini
   Maweedha a maana, nivawedhee a dini
   Awali ndrinyi dhijana, mahavule pia ndani.

2. Kwanda dini ya Rabana, nayo muishikeni
   Kufunga kuswali sana, kwa shime chuyafanyeni
   Mwisho hili vaungwana, ni kushukia peponi.

3. Chungeni sana dhijana, nawausia chungeni
   Ṯabia dhiso maana, bure musidhingieni
   Kwa Bwana Mola ni lana, kufanya aso maana.

4. “Legibiṯi” mbovu sana, mepichishwa udhunguni
   Jinsia kuowana, wamoya ni usheṯwani
   Halagao vakafanya, hufukudhia mapeni.

5. Uraibu si ungwana, pia ulevi si shani
   Amechukanya Rabana, kwenye ake Quruani
   Chwafaa kuepukana, chuepushe sheiṯwani.

6. Uhalifu uso mana, naomba chusifanyeni
   Ṯabia dhenye laana, naomba chudhiwaṯeni
   Chuegeshe kwa Rabana, achuingidhe peponi.

7. Kadiṯama vavulana, mawedha angu shikeni
   Pamoya na mahavule, wasia wangu fwacheni
   Chushikeni dini sana, sheṯwani simwandameni.

## Vanangu Munisikidhe

***Swaleh Omar Mohamed***

1. Huvapa vangu wasia, vanangu munisikidhe
   Isivaghuri dunia, a anasa muyapudhe
   Masomo kudhingaṯia, nafasi musipoṯedhe.

2. Muachie akilini, pasi moya kumbiria
   Mungiapo darasani, valimu kuvasikia
   Masomo muasamini, mupasi bila udhia.

3. Vadhee muvahishimu, ndipo muṯafanikiwa
   Auṯovu wa nidhamu, yiva nikuvundikiwa
   Musende kudhila sumu, a madawa a kulewa.

4. Mapendi musiyaṯake, a mapema si madhuri
   Muṯakuya mucheseke, mungie kwene haṯari
   Birashi mushighurike, vanangu muṯafakari.

5. Na mambo a kuvuana, kwa sababu aupudhi
   Kwa dhipanga kuchiana, haṯa kwene kirumbidhi
   Ni bora chukikanyana, nyoyo dhechu dhive radhi.

6. Ṯama mangi sibaini, huṯosa naloṯanka
   Vasia vangu shikani, muṯakuya nikumbuka
   Chuime na ṯamaduni, umma wechu kuṯukuka.

## Maadili

***Khalid Omar Kanjenje***

1. Maadili kwa Bajuni, vachu vakuheshimika
   Kuṯoka hoko dhamani, vamechulia hakika
   Na havana kasirani, nvachu va muafaka.

2. Ni vachu vene nidhamu, Vabajuni kiwambia
   Ṯena vene kuheshimu, vakuru vadodi pia
   Havapendi kulaumu, shida dhinapoṯokea.

3. Mila havakuipudha, na uṯamaduni pia
Na dasiṯuri henedha, kwa jamii kwendelea
Ndio huvapa mwangadha, mazuri kuwapikia.

4. Huvaheshimu wadhadhi, mama na baba yakini
Nahuvapa kubwa hadhi, popoṯe kwavo numbani
Kabisa hava vaudhi, huvachia akilini.

5. Nahuhishimu vageni, pindi vanapovailia
Hakika kwavo ṉumbani, sana huvakongowea
Ni sifa ya wabajuni, na ni maadili pia.

6. Beṯi siṯa ni haṯima, ya mwisho angu kauli
Machache niliyosema, mueke kwene akili
Haya ni oṯe daima, ya Bajuni maadili.

## Maweedha kwa Barobaro na Havule

*Khalid Omar Kanjenje*

1. Vanangu nisikidhani, ṯaka kuwapa wasia
Muyachie akilini, niṯakayo kuvambia
Ni muhimu ndudhanguni, chusiye kuangamia.

2. Barobaro na havule, vekani kichi mukeṯi
Nivambie alo mbele, ilo kuru mikakachi
Chusiweni kama vale, wene kunena laiṯi.

3. Havule kujiheshimu, ni yambo lene murua
Na barobaro muhimu, kuyaveka mambo sawa
Chusiye kuilaumu, kwa mambo asiokuwa.

4. Ichudhe eṉu havule, ndia siandame sana
Siifanye kama wale, vasokuwa na maana
Ukaya kubika kele, na jamii kukunena.

5. Barobaro nawe chuwa, uvaṯe akudhodhana
Uichudhe sawasawa, vachu vasie kunena
Mwana huu husumbuwa, vakaya kukupa lana.

6. Hapa sasa wasalamu, mwisho va wangu wasiya
   Maneno nalo nudhumu, nadhani mundasikiya
   Vanangu kuna muhimu, kushikamana pamoya.

## Maadili

***Mzee Athman Shee***

1. Vayudhi vamashairi, dhingaṯiani uneni
   Mukeṯi muṯafakari, chulonao maishani
   Dhing'arapo dha hariri, ni maadili numbani.

2. Madili apoṯeapo, uchu hauna samani
   Huva sawa na upepo, uvumiapo angani
   Huva hauna ulipo, kuva hauvenekani.

3. Madili si marembo, kununuliwa dukani
   Ni unasao ulimbo, upikwavo numbani
   Ni ubavo wa ng'ambo, unaodumu mayini.

4. Maadili ni michembo, a fedha kari ashani
   Iyechao dhuri vumbo, la uchu na la samani
   Hauvonekani wimbo, na kele barabarani.

5. Maadili ndiyo ngudho, husimama familia
   Huṯamani valo nadho, kwa njema dhavo ṯabia
   Madili nikichechedho, harufu a kuenea.

6. Ndidho hujenga hishima, ya fahari duniani
   Hudhiondrosha lawama, dha kunenwa mandiani
   Huva ni ichundra lema, huṯumainiwa nyoyoni.

## Maweedha Kwa Waja

***Mzee Athman Shee***

1. Naanda kwa sifa dhake, mwene uwedho Kahari
   Mwene sifa peke ake, mwene ezi na kiburi
   Yachupasa waja wake, ch̲urudi kwake Ghaffari.

2. Bini adamu kiumbe, churudi kwa Mola Lat̲wifu
   Kwa nguvu usiigambe, kwa nno ukaisifu
   Hufa na dhake pembe, dhit̲ongao kwa urefu.

3. Dunia ni nt̲a a chembe, hukuchofa hukivoni
   Ina t̲amu ya wembembe, mara hisha ndomoni
   Rudi kwa Mola kivumbe, usiya chiwa mwandani.

4. Dunia chombo kipana, e nduwangu nisikiya
   Hukuhora ukivona, huyawedha sikiliya
   Rudi kwa Mola Rabana, ufuwache njema ndiya.

5. Naanda angu nudhuma, ndudha kuvahadisia
   Ya akaye na a nima, vale valo changuliya
   Kwa ghera valosimama, mambo ndiyo kuchuliya.

6. Nikumbukapo duniya, moyo shaka huningiya
   Hubadili angu niya, imi kwechu kurudiya
   Kivaenga vamesiya, vale chulovadhoweya.

## Hishima

***Fahad Mahadhi Kombo***

1. Maadili ndiyo ngao, Vabajuni met̲hamini
   Vamefunda vana vao, vayachie akilini
   T̲ena vapigia mwao, changu kwavo udodini.

2. Ni mwiko kwa mwananke, kut̲embea hadharani
   Kuvonesha sura dhake, hilo kwavo huva soni
   T̲akemewa na ndudhake, akome kuva shet̲wani.

3. Hakeṯi mwana awali, kabula ndhee wake
Ṯena angoje kibali, ama apelekwe dhake
Kufanya hiya hunali, hukudha hishima ake.

4. Aṯokapo mwanamwali, huṯoka iye na nduwe
Akenda kula mahali, bila kuchiwa idowe
Ṯarudi kwavo sahali, adabu asikosewe.

5. Kwa upande wa mavadhi, limeshajiishwa sana
Asikivae kijindhi, kiṯakacho kumbana
Vaṯampora mijidhi, mwana alo nsichana.

6. Akoseapo kijana, jukumu la kunkanya
Jirani awedha sana, la usawa kumvonya
Ṯena kwa kuridhiana, ndio sifa a Vagunya.

## Wasia

***Fahad Mahadhi Kombo***

1. Nisikidha ewe mwana, haṯa nawe mwanamwali
Mambo amechacha sana, haswa a kidijichali
Usipoṯaka bayana, uive hwanda kufeli.

2. Munadhipenda wasapu, fesibuku chikichoki
Huifanya ni vashapua, ya vadhee hamuṯaki
Na mwaipenda sharapu, kuvambia malukuki.

3. Usasa mevaharibu, miṯindo mundakoroga,
Dhimedorora adabu, kwa kuṯukudha ushoga
Mambo enyu a ajabu, heri vaundao sega.

4. Epuka mihadaraṯi, nao uhanisi pia
Usikubali shuruṯi, dha kumuasi Jalia
Uṯakufa na laiṯi, maovu kiashashia.

5. Dhijana vakikuicha, vurugu kuliandisha
Sikio lijaze ncha, uyakumbuke maisha
Huna uṯachopacha, maafa kisababisha.

6. Akhiri naweka ṯini, kalamu nimeichuwa
Siendekedhe uhuni, dha vaṯu kudhinyakuwa
Uende dhibaruani, hio maisha kuyuwa.

## Jiṯahidi Ushindre

*Zuwena Ahmed Mohamed*

1. Lau ingevekwa ngadhi, ridhiki kuiṯapiya.
Vangalipandra vayudhi, kwendra kuchuharibiya.
Na nchu asokawedhi, kupandra angeumiya.
Ni shani ake Mwenyedhi, kwa alivochupangiya.

2. Hadhidishi hapungudhi, nja kwa kuṯoridhiya.
Humuhadaa pumudhi, kuva ṯalindra duniya.
Mola hana pingamidhi, aṯakavo huṯimiya.
Dhuka ukibika mbidhi, uwedho mbwake Jaliya.

3. Nja una ubagudhi, na kwingi kupendeleya.
Una wingi wa upudhi, haa oṯe huchweleya.
Mara ningi humuudhi, ako akikuendreya.
Hukereka kwa nṯudhi, kikuvona huchoveya.

4. Sheṯi uve nṯukudhi, hasidi hana imoya.
Uikadhe kuvaudhi, yapo vaṯakushoyoya.
Hela vafanye vapudhi, haṯa vakikuṯukiya.
Ushone kwa mwema udhi, dhishoneke nisikiya.

5. Moyo wako uve radhi, kachika hii duniya.
Asikupache maradhi, ndrani ndrani kuumiya.
Mambo aanike wadhi, moyoni wishe udhiya.
Siaṯe havo baadhi, wasiwasi kukuchiya.

6. Mwisho va vangu waadhi, nami hapa ṯachuliya.
Siishushe ako hadhi, kwa mambo a kusikiya.
Kawaida vaso kadhi, maovu hukudhuliya.
Chembelecho usṯadhi, havakuwedhi sikiya.

## Duniya

*Hassan Msham Mahmoud*

1. Chuiengavo duniya, maṯo echu hayavoni
   Na dhiṯwa dhimesindiya, kila nchu ṯaabani
   Afie mwene umoya, na ndue mwen'e imani

2. Chuisomavo duniya, hachuyaiva kusoma
   Chwashindana kukimbiya, na huku. chumesimama
   Afie mwene ṯabiya, na ndue mwene ruhuma

3. Duniya chuipekavo, hachuisi kuipeka
   Na japo chwavona ndivo, si verevu ni udhuka
   Andakufa mwen'e chuvo, na ndue mweṉe baraka

4. Duniya chwendavo nayo, hachwenendi kwa udhuri
   Huku chushishie choyo, na huku chuna auri
   Andakufa mweṉe moyo, na nduake mwene heri

5. Dhilioko duniani, dhoṯe dha sasa si kichu
   Si michi si hayavani, haṯa pamoya na vachu
   Afie nṯamaduni, na nduake mwen'e uchu

6. Mwisho va neno duniya, ni mwisho wa kuangadha
   Ṯoka mwando wa kadhwiya, na hamu ya kumalidha
   Afie mwene duniya, na nduake miujidha

## Heri kuliko kama

*Hassan Msham Mahmoud*

1. Vachu sasa duniani, hudhua kila madhuo
   Vako mbio dhishindoni, kuṯafuṯa vaṯakao
   Heri ipu la puani, kuliko la mashikio

2. Mii ichendee baa, kwa dhivavu na koroṯo
   Ikosekene waswaa, na mambo henda kushoṯo
   Heri kuwaa dhijaa, kuliko kuwaa maṯo

3. Vachu vave ni vaongo, huhadaa kula yambo
Ivo hubuni mipango, vavonekane michembo
Heri kuemewa nyongo, kama kuvavwa na chumbo

4. Kuvambia sina budi, si sifa angu uchoyo
Ṯoka dhamani dha jadi, suṯe huchupeka mbiyo
Heri kuwaa jasadi, kuliko kuwaa ma moyo

5. Nivumbisie na nguvu, dha kuṯokuva ndhivu
Na mori ya ushupavu, kiṯe na ukakamavu
Heri kuva nlemevu, kama kuva mpumbavu

6. Mwisho wa heri kuliko, na kiandamidhi kama
Udhwalimu ulioko, haupachi mwisho mwema
Heri mwene maudhiko, kuliko mwene ṯuhuma

## Maweedha

***Jamila Ali Haji***

1. Handa kushika kalamu, pefu mochoni kuchia
Kuvachungia nudhumu, vanangu kuvausia
Mwavanye ṯamu na sumu, na hadaa dha duniya

2. Ṯaka uvuche fikira, muupime ulimwengu
Ni hengerebu huvira, si wenyu inyi si wangu
Walivumbwa ni duara, una ṯamu na uṯungu

3. Huvausia kwa hama, dhisipoṯee akili
Ulimwengu changu dhama, mambo mavili mavili
Kwenye raha mukiṯuma, na ṯabu mudhihimili

4. Ṯena ivani makini, Mola wechu hana sari
Avapapo miṯihani, ifundeni kusubiri
Musiṯoke mipakani, subira huvucha heri

5. Idhidisheni adabu, kwa valo vakuru venu
Musive venye gadhabu, haṯa kwa hirimu dhenu
Mvumba havapi ṯabu, dhiṯanyoka ndia dhenu

6. Ivani vaaminifu, ndundhenu shikamanani
Muuepuke uchafu, ueneo miyini
Muṯavuka bila hofu, nyamba dhoṯe baharini

# Nlango a Chachu: Kadhi dha Vabajuni

## Ukulima

*Abdalla Ali*

1. Michi ṯakacha kwa dhaṯi
Asubuhi nṯikachi
Kisha niombe kwa dhaṯi
Hakuna cha achi achi
Kunde, fiwi kachi kachi

2. Kisha ṯaichia randa
Ndio kadhi imeanda
Sishuki ṯena ndapanda
Na nungwa nikivainda
Nijenge changu kibanda

3. Kisha ṯafanya ulingo
Nnana mwenye ṯevengo
Ni kadhi enye ushingo
Kadhi initodhee kijongo
Ni lichudhe langu bongo

4. Niṯailinda usiku
Ṯanende huku na huku
Imenidhidi shauku
Nisaidia Maliku
Ndudhangu kadhi ni huku
Vamekuva kama kuku

5. Ṯadhiaṯa dhikauke
Nivaiche vanavake
Ichaani nidhiveke
Kusudi nisisumbuke
Nipache nisiṯirike
Kwa ndudhangu nidhipeke

6. Kisha ṯadhilinda kunde
Huomba vasivunde
Na nchama niuponde
Machikichi niachunde
Na mayungu niyaṯunde
Imeng'ara yangu chonde

7. Kwa shembee ndabaini
Siṯoki niko mwichuni
Mola unipe auni
Mwaka huu ni hondeni
Na pojo ni uvavuni

8. Kijojo ṯavapikiya
Mui nndaumbiriya
Nichie yangu pondeya
Buru asiyeniliya
Kibandani nṯangiya

9. Imi iyu ṯaupanda
Kwa bidii kiulinda
Ni ladhima kuipinda
Kwa tavau kuvalinda
Haiwedhi kunishinda

10. Nikidhunguka hondeni
Ndia ya nungwa ni gani?
Kivona punga mbuvani
Na vaovu hayawani
Bishee mudhiengeni
Hava nnana jamani

11. Buru bishee pamoya
Hondeni kunivuniya
Bei kiiṯafudhiya
Chakula ṯaivekeya
Ndaa iṯanondokeya
Navo vapache chumiya

12. Pamoya pondea dhangu
Nilivone jasho langu
Na vale valio vangu
Kiyapanga kwa mafungu
Kwa kudura ake Mungu

## UṮONYI

*Abdalla Ali*

1. Uṯonyi wechu mbwa yuwa
Na malasha chwaṯukuwa
Vaovodhi venye kuwa
Majiweni kuliṯowa
Pono, ṯasi na dhiluwa
Na machava kuvavuwa
huya venye kununuwa

2. Majarifa kadhalika
Rambadhani chwamshika
Na pwedhi yake hakika
Mambasani chwayapeka
Na ng'onda vakikauka
Kwa ingi chwafaidika

3. Nambo piya chwamṯowa
Na sana huchusumbuwa
Anawedha kuchuvuwa
Na supu kuchokosewa
Dhipandeni akichiwa
Mara nyingi huokewa

4. Vanavake madondoni
Na ibori nkononi
Na vangine ni imboni
Dhali dhinao samani
Mama dhechu mayemani

5. Kuna vaṯonyi va kamba
Ni vangi vakivasomba
Kwa udhuri kuvapamba
Na Mungu vakimuomba
Chwalivarisi vajomba

6. Kadhi ilo na balaa
Kwenda kuṯafudha kaa
Ni ipi yakukufaa?
Bora isipiche saa
Kusudi iishe ndaa

7. Kuṯoka hoko dhamani
Chukichega nlangoni
Voṯe hushuka maini
Hobe jama livucheni
Kwenye ṯapo vako ndani
Kuvachiya mashambini
Kuvapeka Mambasani

8. Chwenda kuchega michoni
Na mbingusi uko ndani
Yanao nyingi samani
Kuyadhanya kwa yakini
Hupacha mangi mapeni
Sifa huchiya chomboni

9. Hupimiwa midhanini
Kiambacha ijiweni
Anao gamu mwilini
Chule na bodo numbani
Akianikwa yuvani
Na kwa mofa chunleni

10. Na kaure kudhichunda
Majiweni kuyapanda
Na kururu kuvaponda
Na vadhungu vakipenda
Siku dhoṯe kuipinda

11. Maini vakidhamiya
Shambini vakivachiya
Na nanga kuvachiliya
Baraka kuvadhidiya
Isi voṯe bahariya

12. Na ṯena inao dhiki
Mahala hakupichiki
Miini hakukeṯiki
Imekudhidi hamaki
Upache ndhuri ridhiki.

## Jahadhi

*Abdalla Ali*

1. Hapa sasa naṯamuka
Uchako chunauveka
Kuna muli kwa hakika
Alama hudhiandika
Mbavo chunadhodhiṯaka
Shoka kwanda hulishika

2. Huyachiya maṯaruma
Mongochi ulosimama
Mijari chwaichidhama
Ifundo ukilandama
Mashuwani kuna ngama
Chombo kisiye kudhama

3. Joshi nenda kaivuche
Njari muupakache
Nlangoni chusicheche
Madhimbi yasichupache
Chulochega chukavuche

4. Ngololo akishangia
Chundu aṯachuṯolea
Ndipo fundi huandia
Kalafaṯi kuichia
Na sifa chombo kuchia
Hasumbuki baharia

5. Na changa chwaliṯindia
Nanga mbee huichiya
Farumu huivekeya
Hurudi kaiṯungiya
Kachikachi hulichiya
Amuri kaingojeya

6. Mashuwa huchiwa rangi
Iṯakapo kwenda ṯingi
Ndani dhilidho ni nyingi
Kudhiṯafuṯa shilingi
Kisha hupakiwa longi
Na mafucha kwa miṯungi

7. Inyi voṯe sikidhani
Chwaunyosha nṯangani
Na ṯurusi kibaini
Fundi sive lawamani
Nda nsaji kwa yakini
Mashuwa chuchengedheni

8. Koṯe koṯe uvavuni
Na dasiṯuri mulini
Indafungwa farumani
Na shariṯi iko ndani
Na upo chuushikeni
Mayi ndani chuṯoeni

9. Nahudha huchuambiya
Na damani nao piya
Kwa inde chwaṯaka ndiya
Chombo chikachuvundiya
Bila kupacha udhiya

10. Kwa hakika ubavoni
Mayi angie ngamani
Hukalafaṯi jamani
Pale pale iduvuni
Kikavu chenye samani
Kukesa kuṯwa ngamani

11. Kuichachiya mulini
Na kukadha farumani
chushukeni kwa makini
Ikipwewa nṯṯangani
Mai nikaushe ndani
Nende kachuwe numbani

12. Ikapendedha maini
Huvona raha moyoni
Ngurudi chuidhibeni
Kwenye mashuwa pandani
Na nyavu chupandisheni
Mashini nachufungeni.

## Nṯegemea Cha Ndue

*Yusuf Kassim*

1. Kadhi ni kuru ibada, kila nchu ni wajibu,
Cha halali si nsada, kuṯafuṯa kwa aibu,
Na maṯajiri hukuda, siye kupacha dharubu,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

2. Kadhi dhechu Vabajuni, namba moya ni bahari,
Pili ni kukacha kuni, kwa vamama mahodari,
Na dhiki hachudhivoni, chumehiyari kadari,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

3. Chachu shongoro maṯumbi, huchuchesa kilimoni
Hasa kulipo Na vumbi, yembe halishuki ṯini,
mwisho ukinya huṯambi, paka urudi numbani,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

4. Nne kukacha mikoko, udhanye upache pesa,
Hupambana na dhiboko, moyoni hukuachusa,
Hakuna sharia ako, kumvua si ruhusa,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

5. Si bahari si mwichuni, dha halali hadhiliki,
Nachi akifa hondeni, uwe ako ni bunduki,
Kasa akia numbani, ni milioni na laki,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

6. Kila nnyuka Kiunga, amekuva kwa bahari,
Eo mayuva kufunga, hamuivoni haṯari,
Yuwa ndio echu kinga, haṯa kuliko mapori,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

7. Maina angu kamili, Yusufu Bini Ayubu,
Yusufu ni la asili, Ayubu ni vangu babu,
Malenga wa kiswahili, pamoya na kiarabu,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

8. Mola chulinde rijali, pamoya na mahavule,
Vale vasio kayali, usindidhi vape bure,
Hapa nafunga kufuli, nami nende nikayale,
Nṯegemea cha ndue, mwisho hufa masikini.

## Kadhi dha Vabajuni

***Famau Ali Famau***

1. Mola mṯerehemedhi, chwashukuru Rahamani
   Aloavanya uyudhi, kwa ṯaifa la bajuni
   Anafanya kubwa kadhi, mbajuni suluṯwani.

2. Ukulima ndio kadhi, dhisiwani na barani
   Malimo ya siku hidhii, haṯa yale ya dhamani
   Kuna na mbinu dhindudhi, bajuni kiva hondeni.

3. Ufundi wa majahadhi, na madau baharini
   Bajuni hakwenda kodhi, hidhiunda kwa makini
   Mdhungu hayo hawedhi, haṯa hesho hamkini.

4. Mbajuni ni muhundhi, va dhuma dha kivandani
   Chuma kwake hakiwedhi, kumwechea kisirani
   Asili ake uyudhi, ana akili kiṯwani.

5. Kwa uṯonyi humuwedhi, mbajuni ake fani
   Iye nṯonyi wa nyedhi, nyaka nyingi baharini
   Huvuwa papa mapwedhi, na pwedha voṯe nyambani.

6. Vabajuni ni vakwedhi, va kupanda minadhini
   Panda mirefu minadhi, madafu kuangueni
   Pia wao ni vajendhi, boloki na michi ndani.

7. Mbajuni simba kadhi, kwa bidii ya kadhini
   Na hufanya kwa ujudhi, nkono vake va shani
   Dhungu huṯowa maṯodhi, bajuni si nshindani.

8. Ṯamaṯi kadhi ni kadhi, heko sawa vabajuni
   Mambo mangi memaidhi, kacha michi makokoni
   Na mangi enye uyudhi, huyafanya suluṯwani.

## Kadhi Dhechu Vabajuni

***Swaleh Omar Mohamed***

1. Bajuni ni vaungwana, sivachu vakuṯavia
   Kadhi dhavo ndamaana, mavuno huivunia
   Kwa mangi kushikamana, veneve huikomboa.

2. Chukenenda baharini, si yoyoṯe kuchwandama
   Ni mijisi kwa miṯani, kwa mayuwa na mayema
   Na mishipi na kambani, kwa uṯonyi ṯuko wima.

3. Chwendapo kwa ukulima, hulima kisawasawa
   Kaṯu hachuaṯwi nima, na bara chwalichambuwa
   Huvuna chukiṯerema, na dhakula dhikiliwa.

4. Kwa mafundi akuunda, majahadhi na mashua
   Hakuna vakuchushinda, uyudhi undabobea
   Kwa bajuni uṯapenda, vainde huchuchambua.

5. Kwa mafundi vakushona, ajabu ṯaivonea
   Mishono kila aina, upendao kuṯaua
   Avake na vavulana, a miguvo na kofia.

6. Na mafundi a kujenga, mangi siṯoaṯamka
   Kwa mijumba a kupunga, madhuri akusifika
   Ni velevu va kupanga, bajuni uṯachuchoka.

## Kadhi A Vabajuni

***Khalid Omar Kanjenje***

1. Hapa naṯaka radidi, machache naṯaka nena
   Haya angu makusudi, ili nivape bayana
   Kwa kadhi waiṯahidi, Bajuni kila aina.

2. A userumala kadhi, haṯa pia ukulima
   Bajuni wana ujudhi, la ukweli chukisema
   Wala hawana ajidhi, pia hawarudi ṉima.

3. Kuna kadhi a kuṯoma, ya nshipi na kwa nyavu
Na haṯa pia mayema, vafanya kwa uchulivu
Mayarifa na mayuwa, hudhifanya si kwa nguvu

4. Na makuchi kuyafuma, ni a vanavake kadhi
Vaifanya himahima, kwa kuchumia uyudhi
Wala havarudi ṉima, ndio kadhi changu endhi.

5. Na usuchu kuṯapasa, ni kadhi dhao dhidhere
Waifanya bila kosa, kwa upana na kwa mare
Ili wapache mapesa, kaṯu hawakeṯi bure.

6. Hapa nindaishilia, nimefika kikomoni
Nadhani mumesikia, niloyanena vendani
Wallahi ṯwajivunia, kadhi dhechu vabajuni.

## Usafiri wa Kibajuni

***Mzee Athman Shee***

1. Nadhumu kuvuwa nanga, bahari kuiṯapiya
Nilichekwe langu changa, nyambani kuivukiya
Usiudharau nlinga, limango ni asiliya.

2. Valichiundra limango, kwa kalibu na vumbo
Na dhingi dhamirengo, eo huviliwa dhombo
Kuṯimidhiya malengo, kuikudhiya michembo.

3. Valianda na limango, ridhiki kuṯafudhiya
Kasia kudhua dhongo, neema kudhiṯapiya
Vakipicha milango, kwa salama vakingiya.

4. Vakiipanda bahari, kwa chungo kuvaechea
Kiva sulubu haṯari, nyamba kuvagurumiya
Vakidhifuchia hari, ridhiki nguvo dhikikaukiya.

5. Vakiivuka kwa kidha, na nocha ndriyo ramani
Nyamba wakidhiongodha, kidha keusi maṯoni
Nayuva likichomodha, chombo huvuka dirani.

6. Valiendra kwa miedhi, pepodha kubadilika
Vakionyesha uyudhi, bahari wakidhivuka
Milango ikiwa wadhi, na siku dhakufunguka.

## Kadhi Dha Vabajuni

***Mzee Athman Shee***

1. Mwanda Bisumillahi, kwima kumuomba anga
Huomba avape rahi, madhicho kuaṯenga
Yavadhonge maṯilahi, vavuke bila kugonga.

2. Huichugacha kungiya, gongo kulikumbachia
Hiṯima huvasomeya, baraka huvashukiya
Kesho vaipache ndiya, navo mwambani kungia.

3. La muando ni muongo, hisabu dhikiṯimiya
Huṯoka na lavo lengo, gongo kuvuadhiya
Huingia pasi kinyongo, vakamuomba jaliya.

4. Huṯolewa vakalonde, kukunduwa la upia
Hurudi nasi chwenende, harusi kuyalikia
Chuule kama chendre, amuri dhikiṯokea.

5. Huenendra kwandiya, washauri va baraka
Kuangusa wakueveva, gamu iliyofungika
Avafunguliye mbava, chungu chakuandika.

6. Huṯoka nisikohohe, ndiya kuiyandamiya
Nende nimuhadahe, na pamba pamba kungiya
Nkononi nina kwahe, mbayo kuisukuliya.

## Jamii na kadhi

*Fahad Mahadhi Kombo*

1. Haikuveko ajidhi, kamwe na ugoigoi
Valichumia uyudhi, kuyakidhi masilai
Havakudharau kadhi, lengo kuu la uhai.

2. Kwa ufundi namba wani, va kila nyanda hungia
Vangiapo michamboni, kula kichu huchengea
Ni hodari vabajuni, mangi valiifundia.

3. Hukuundia jahadhi, pasi chekinolojia
Akaichengedha ṯedhi, na omo ilo sawia
Huṯembedhwa kwa uyudhi, bahari kudhichasua.

4. Valikilima machanga, machikichi yakimea
Nchama nao mpunga, simu simu karafia
Korosho vakidhigonga, kwa pishi moya kwa mia.

5. Vangiapo makokoni, michi ṯakuangusia
Boriṯi ficho na kuni, dha mekoni kupikia
Pau dhigingi ṉhumbani, paa lako kuekea.

6. Vashi valivo veledi, ndhuri hukujengea
Ilo ndhuri na gudi, na ndani ukiishia
Mbajuni changu jadi, hodari kuifanyia.

## Kadhi A Kibajuni

*Jamila Ali Haji*

1. Kinyuka nilioavona, huku kwechu bajunini
Vana kwa vachu vadhima, kadhi valodhiamini
Ni kulima na kuṯoma, na kungiya makokoni

2. Huanda kwa kuṯefudha, mwichu ndhuri ni upi
Mkonde akafuadha, kwa masadaka mwichuni
Hapo kuchema huwedha, akapisa nchamani

3. Mkonde kisha kuyaa, huṯindikia hondeni
Akalima kwa masaa, na kupanda ulingoni
Mwisho dhipundu huyaa, dhikachiwa dhipembeni

4. Kadhi ngine mashuhuri, bajunini ni kuṯoma
Kisha huya maṯajiri, na dhombo kuya kupima
Lakini sasa bandari, inndachurudisha nima

5. Vanavake vakinyuka, hunyukia makuchini
Vakirudi huwavika, vakangia na mekoni
Vakisha kula huṯoka, huekea miyaani

6. Na vangine jadi lavo, ni kwenenda makokoni
Na kuu silaha dhavo, msumenyo nkononi
Hujengaa numba dhavo, na kudhanyia vageni

7. Henda vakikacha michi, vakiya nao numbani
Vakachapo maboriṯi, hupekwa ughaibuni
Sasa hakuna pamichi, ukishikwa henda ndani

# Nlango a Iṉe: Mapendi

## Mahaba

*Abdalla Ali*

1. Ṯakupenda upendeke
Nakuṯaka uridhike
Nduo nisiadhirike
Umeshinda vanavake

2. Mahaba yaso nfano
Lini ṯapacha usono?
Daima sivi nnono
Nawe nishika nkono
Mekuva kama sindano

3. Ruka ndege wa mabava
Na salamu wadhiiva
Wambie mekwisha kuva
Chakula changu mabava
Na vakenda la kuava

4. Sina haṯa la kunena
Si usiku si nṯana
Undanivua kimwana
Ni ndhuri wa maana
Nakuapia  Rabana

5. Nikiyala hukuocha
Raha hapo kaipacha
Mara pa ikikucha
Ndipo hapo yakachacha

6. Ndoo mwana ndoo mwana
Shahidi wangu Rabbana
Ndani ya swala hunena
viva nakupenda sana
Mai hayashuki ṯena
Na shai  nikiivona

7. Havule uṯanivua
Iva kwako naumia
Uwe dhakuṯaua
Kachika hini dunia
Hela nawe nichambua
Nami nipache chulia

8. Menichia dharubuni
Nami nive  furahani
Damu ndakwisha mvilini
Mwenginewe simvoni

9. Na baruwa nkononi
Nda Faṯuma na Lahani
Imi niko ṯabaani
Chengine sikiṯamani
Kwako niko maradhini

10. Haṯa siṯaki chakula
Ni dhiki imi kuyala
Lini ṯakupacha Lela
Sivoni yako badala
Kwako sumu niṯaila

11. Kichandani huniiya
Moyo wangu huchuliya
Gafula ndani mengia
Ndwee dhikanidhidiya

12. Ama ṯakuṯapiliya
Lela kikufikiriya
Nikimuomba Jaliya
Hakuna wa kuṯokeya

## Hunitaki Kisa Nini?

*Yusuf Kassim*

1. Penḏi nḏia ya adhabu, sina budi kuipicha,
Ṯena ichendee ṯabu, nami siwedhi kuaṯa,
Eo huomba jawabu, ni lini niṯakupacha,
Huniṯaki kisa nini, sababu niichambue?

2. Kula kikufikiria, moyo hunichunduvaa,
Na sauṯi kisikia, akilini hulemaa,
Vuso na maungo pia, maṯoni nimekuvaa,
Huniṯaki kisa nini, sababu niichambue?

3. Haṯa kama uko mbali, si mbali na moyo wangu,
Nimekupa na kibali, ukeṯi moyoni mwangu,
Mapenḏi ako a kweli, agonge nafusi angu,
Huniṯaki kisa nini, sababu niichambue?

4. Maṯodhi alo dhahiri, huṯoka maṯoni mwangu,
Kuva mbali si hiyari, ukiva mpenḏi wangu,
Nakupenḏa sio siri, kuṯoka moyoni mwangu,
Huniṯaki kisa Nini, sababu niichambue?

5. Vaovu usivajali, nive wako uve wangu,
Haṯa kapacha ajali, sihofu uhai wangu,
Hukupenda kwelikweli, shahidi ni Mola wangu,
Huniṯaki kisa nini, sababu niichambue?

6. Pendi pia ni safari, a haṯari na salama,
Kuna wakaṯi shuari, na ifuṯedhi kuvuma,
Voṯe chuve vasafiri, kamwe chusirudi nima,
Huniṯaki kisa Nini, sababu niichambue?

7. Mwishoni ndasikilia, sikusadha akunena,
Usiniaṯe kulia, huruma nami nivona,
Sina kwa kukimbilia, kwako ni mwisho a kona,
Huniṯaki kisa Nini, sababu niichambue?

## Eo Hakuna Mapendi

***Quswai Sufiyani***

1. Naanda langu shairi, kuṯoa angu bayana
Niipange misiṯari, kisha nichie na dhina
Ingawaje si hodari, nimejaribu naona
Eo hakuna mapendi, imebaki hadaana

2. Imebakia asari, mapendi hakuna ṯena
Nke, mume vajeuri, machusi kuṯoleana
Wafanyiane miari, na kama vao hakuna
Eo hakuna mapendi, imebaki hadaana

3. Dha chumbani dhao siri, dhachangazwa kila kona
Mabaya pia madhuri, huva sio siri ṯena
Hadhira huva ṯayari, wameyua valonena
Eo hakuna mapendi, imebaki hadaana

4. Madireva a malori, kula wanaemuona
Hunena huu ndhuri, na namba vakapanana
Haṯa havo asikari, siṯaki ao kunena
Eo hakuna mapendi, imebaki hadaana

5. Sheṯwani asichughuri, chukamuudhi Rabana
Chusipandisheni mori, kuṯaka kuonyeshana
Chukosapo nachukiri, ahidi huchendi ṯena
Eo hakuna mapendi, imebaki hadaana

6. Mwisho chuucheni nari, meuveka Subuhana
Kula asoṯenda dhuri, dharubu aṯadhivona
Japo angu hamukiri, sina ṯena la kunena
Eo hakuna mapendi, imebaki hadaana

## Mapendi

*Famau Ali Famau*

1. Nema kuṯoka kwa Mungu, ni binadamu kupenda
Vadhadhi na ndugu dhangu, na majirani va mama
Rafiki na nke vangu, kupendana ndio sawa.

2. Huba huṯoka kwa Mungu, Ilahi Mola Rabana
Ampaye haṯa ṯungu, ridhiki bila hiyana
Mapendi siya ndhungu, sivema kuhadaana.

3. Mawada a valimwengu, amechupa Maulana
Kupendana valimwengu, chumekaririwa sana
Chupendane nke wangu, chusifuache fiṯina.

4. Mapendi yambo la Mungu, meamuru Maulana
Chupendane valimwengu, kwa wema na ihisana
Chusichiane maṯungu, chukava chuṯaṯengana.

5. Chumpende haṯa ṯungu, na dhiumbe dha aina
Suṯe kwenye ulimwengu, chusive chuṯavuana
Mwisho wa dhicha ni pingu, dhicha hadhina maana.

6. Mapendi ṯaguo langu, kupenda ni kiungwana
Kwanda nampenda Mungu, mame na nke na vana
Navo voṯe valimwengu, haki nawapenda sana.

7. Ṯamaṯi mapendi angu, yangasukwasukwa sana
Imi na mpendi wangu, kwa sasa raha hachuna
Chwamuomba sana Mungu, achurudishie ṯena.

## Chenye Kulenga Hufuma

*Swaleh Omar Mohamed*

1. Chene kulenga hufuma, makini kikachuliya
Ene kuyaa hufuma, na mambo huendeleya
Ene kuvaka hudhima, pia mapendi husiya
haya mambo huṯokeya.

2. Kipakivacho huyaa, kikavuka kwa salama
Nnyonge huva shujaa, huya kwa yiu kiema
Kwene kidha huva ṯaa, na mapendi husimama
haya ni mambo hukoma.

3. Mwene kupanda hushuka, wa yiu nngoje ṯini
Uchelevapo ṯafika, uwegese bandarini
Ndhuka huerevuka, mapendi henda mwishoni
yakakoma ukingoni.

4. Chene kuchekwa huchuwa, na chakwenda husimama
Afundwaye huchambuwa, alokubali kusoma
Mwene sifa husifiwa, mapendi nao hukoma
haashikiwi ladhima.

5. Kinolewacho hupacha, kikaṯinda kwa ajabu
Ushikapo uṯaaṯa, ugonjwa hupaṯa ṯibu
Na siku nadho hupicha, na mapendi huchusibu
yakakoma kwa ghadhabu.

6. Livushalo huva gogo, na lendalo huishiya
Na maneno si ndhigo, nke hupendwa ṯabiya
Na dhiyadhi si muhogo, mapendi ana udhiya
hupendana yakasiya.

## Dhiki Dha Mapendi

*MzeeAthman Shee*

1. Dhichukucha sumilani, uneni kunipulika
   Kinofu cha nvilini, menifanya kuṯemuka
   Huvambia kichangani, huendra chikaongika.

2. Haumalidhi maudhi, na dharubu dhandrani
   Hu udhonga simaidhi, huyuṯiya abadani
   Huenenda kwa ghaidhi, na biri dha mafaṯani.

3. Hufinikwa na gubari, na weusi wakidhani
   Hauvoni lenye shari, hukimbiliya nkoni
   Hupoṯedha la saburi, ukavama hasarani.

4. Dharubu ni usongapo, hauṯoki malengoni
   Hauchoki urangapo, hudhengeya afuweni
   Hufuma kuvona ndipo, kajenga maṯumaini.

5. Haufudhi ulengapo, huvuya vuya chochoni
   La faraja halipo, hauṯoki lavamani
   Uṯadhongwa na upepo, hulivoni la maṯoni.

6. Hupoṯedha ujagina, unyonge ukaridhiya
   Hudhihimili hiyana, maovu ukaridhiya
   Halivi lene kufana, husimama la udhiya.

## Nyonda

*Jamila Ali Haji*

1. Ṯaka kuṯoa pumudhi, nikweledhe la ruhuni
   Sili sina usindidhi, nina ṯabu nafusini
   Na wala sina maradhi, ni nyonda dhake fulani

2. Kwa nyonda dhake fulani, Huvona ṯaadhirika
   Kimvonesha havoni, hudhidi kuniepuka
   Ṯamwendea maguuni, pangine ṯasikiṯika

3. Ama kweli kwa hakika, Una dhiki apendao
Mwambieni si dhihaka maneno nianenao
Pangine ṯasikiṯika, anipe nami pumbao

4. Moyo una ṯabu nno, sina raha asilani
Sikubakisha sindano, na dawa dha madukani
Nandika nami nkono, ashuke mai kooni

5. Moyo wangu hwenda mbio, ndani ni kama kionda
Udhicho nilionao, haṯukui haṯa punda
Kula akuṯukieo, mwapidhe nakupenda

6. Lakini huba ni ṯamu, vavili mukipendana
Waswaa na ṯabasamu, kula mukidirikana
Ulimwengu huva sumu, mukosapo kuvonana

## Mapendi

***Fahad Mahadhi Kombo***

1. Mapendi yanashiṯadi, kwa mume na nke wake
Hulindwa kama waridi, kusudi lisinyauke
Likifukidhwa na udi, rihi mbovu lisinuke.

2. Nke ndani ya akidi, hunlinda mume wake
Baiṯini akirudi, kuṯoka kadhini kwake
Hupokewa kwa nyiradi, na nyimbo dhenye makeke.

3. Hadi ndani kwa siṯadi, mambo asiharibike
Kama uwa la nkadi, shombo hukimbidhwa dhake
Hulainishwa fuadi, a mume na nke wake.

4. Chakula kikivadia, hudhiwiwa asiṯoke
Ale kwa kufurahia, ashibe na kinshuke
Mapendi avo kuea, a daima vasichoke.

5. Mayi aliobaridi, hukoshwa hadi nvuke
Ili kusudi Hamadi, aṯoe uchofu wake
Alale bila inadi, la kuchoka mwili wake.

6. Familia maridadi, upendo koṯe ufike
   Vameusia valedi, wadhee vechu chushike
   Ṯupendane kwa kusudi, nyoyo dhisifadhaike.

## Nidhamu dha mapendi

***Famau Ali Famau***

1. Chwamshukuru Karimu, ndie wakuhimidiwa
   Alomvumba Adamu, akamvumba na Hawa
   Mahusiano muhimu, kichu kimoya vakawa.

2. Mahusiano ni ṯamu, hususa kwa vanandowa
   Haṯa vale maharimu, kuhusiana si sawa
   Ela mambo a haramu, kuafanya siyo powa.

3. Kupendana vanadamu, ameridhika Moliwa
   Voṯe huwa mahashumu, kuhusiana kindowa
   Udhinifu ndio sumu, hilo limeharamiwa.

4. Na urafiki ni ṯamu, haṯa kwa vasoovowa
   Kuhusiana kwa hamu, na vale vasoolewa
   Bora dhinaa haramu, dhisiwe dhiṯafanyiwa.

5. Biashara ni muhimu, michaji kuiṯeuwa
   Mahusiano adhimu, mema yanakubaliwa
   Undugu waisilamu, ndio chuliousiwa.

6. Kuhusiana wadhwamu, suṯe chumekubaliwa
   Na mashariṯi magumu, hakika chumeekewa
   Uhasharaṯi fahamu, ni wovu chumekemewa.

7. Ṯamaṯi angu kalamu, huṯosa nalochasuwa
   Mahusiano ṯimamu, kwa vachu voṯe ni sawa
   Ṯangamano la haramu, ndilo chulilodhiviwa.

# Nlango a Ṯanu: Ṯudhingatie Ilimu

## Ilimu

*Abdalla Ali*

1. Bajuni nachunyukeni
Vana chuvasomesheni
Isi voṯe chusomeni
Madhuri na chuvapeni
Vala halivi nishani

2. Chuaṯeni ya dhamani
Sukuli chuvapekeni
Kesho ave kaputeni
Na nahudha wa melini
Jamani nachunyukeni

3. Kisha chuveni na ari
Chufanyao si udhuri
Chupache madakiṯari
Navangine asikari

4. Isi chuveni na ghera
Nachusimame imara
Kuumalidha ukora
Hachuipachi hasara
Ṯachuiliya ṯijara

5. Vala haivi aibu
Yaṯaisha masaibu
Kidhungu na kiarabu
Chuṯapacha makaṯibu
Chuaṯeni  ya mababu

6. Chuvasomesheni vana
Dini vasome sana
Na udhuri vakinena
Ni yambo lenye maana
Chuvapeke paka China
Na chuveni vaungwana

7. Wakaṯi undawadiya
Ya akhera na duniya
Chusipache kuyuṯiya
Hii ni yechu shariya
Shaṯi ndani kulitia

8. Hoko chulipoandiya
Vakaisome shariya
Baluna kichupekeya
Sukani kichushikiya
Jogoo ndachuvikiya

9. Ṯayari kuiṯoleya
La ukweli ndavambiya
Maradhi kuchuṯibiya
Mipaka Kuchulindiya

10. Vachuive vachu voṯe
Chushikalo chusiaṯe
Vasome ilimu dhoṯe
Kaṯu wala chusiyuṯe
Chuṯakalo chulipache

11. Vana vechu vakisoma
Chuṯaipacha salama
Vapache kuṯakalama
Kwechu ikome garama
Vakisoma ndio mema

12. Vaume  na  vanavake
Na kidhungu vakishike
Bajuni chukasifike
Chusiyale nachunyuke
Ilimu vakaishike
Kwenye uchumwa chuṯoke.

## Iṯafuṯeni Ilimu

***Yusuf Kassim***

1. Chuisomeni ilimu, vana baba na vamama,
   Pindi ukiifahamu, uṯaipacha hishima,
   Na uṯakuva imamu, kwa uwedho wa karima,
   Iṯafuṯeni ilimu, apukuva kwenda China.

2. Ifundishe kuandika, haṯi ilio nḏuri,
   Loloṯe unaloṯaka, uṯalipacha kwa heri,
   Sikwambii kwa dhihaka, na uṯakuva amiri,
   Iṯafuṯeni ilimu, apukuva kwenda China.

3. Hini ilimu a dini, ameiveka Karima,
   Chuipende chusomeni, ilimu ya ṯaadhima,
   Chuṯaingia peponi, amali ikiva njema,
   Iṯafuṯeni ilimu, apukuva kwenda China.

4. Himarika ndugu angu, heri ikikuandama,
   Maarifa a vadhungu, sukuli uṯaposoma,
   Na heri iko kwa Mungu, ni wadhi sio hujuma,
   Iṯafuṯeni ilimu, apukuva kwenda China.

5. Ilimu ni ṯarubini, akuangalia mbali,
   Na ni gilasi maini, a kuṯafuṯia mali,
   Usiveke kishogoni, kamwe hilo sikubali,
   Iṯafuṯeni ilimu, apukuva kwenda China.

6. Nchu asie ilimu, dharau hainṯoki,
   Huchekwa ake nujumu, akava ni kama ṯaki,
   Akikamuliwa kamu, yaa ndilo lake paki,
   Iṯafuṯeni ilimu, apukuva kwenda China.

7. Ilimu kwa vabajuni, ni faradhi kwa hakika,
   Kwa kuifuacha dini, ukafiri kuepuka,
   Ilimu a duniani, na ahera kuishika,
   Iṯafuṯeni ilimu, apukuva kwenda China.

8. Kadikama wa ṯamaṯi, shairi laṯamaṯika,
   Nendao dhangu kukeṯi, yaani kupundhika,
   Musiyuṯi na laiṯi, ilimu mukaidhika,
   Iṯafuṯeni ilimu, japokuva kwenda china.

## Ilimu Kwa Vabajuni

***Quswai Sufiyani***

1. Naandha angu nudhuma, kwa ina lake manani
   Ṯuma swala kwa Hashima, na swahabadhe Amini
   Na dhuria wake wema, pamoya na waumini
   Ilimu kwa Vabajuni, ili ni shani hakika

2. Niandapo kuisoma, ilimu a wabajuni
   Usiaṯe kunandama, ukaikosa samani
   Waliṯukudha daima, kuṯokea uchochoni
   Ilimu kwa Vabajuni, ili ni shani hakika

3. Dhijana vachu vadhima, walikiyaa chuvoni
   Ilimu ililadhima, hususwa ya Quruani
   Valadhimishwa kusoma, bure huṯoi ipeni
   Ilimu kwa Vabajuni, ili ni shani hakika

4. Usṯadhi na valima, hishima ao engani
   Kunde, fiwi na nchama, ṯukidhipeka chuoni
   Ili ni ada ya numa, kuilipa ihisani
   Ilimu kwa Vabajuni, ili ni shani hakika

5. Havakukoma kusoma, chuvoni nsikichini
   Na valio vakulima, vakisoma mahondeni
   Ndio wakapacha nema, ilimu kuisamini
   Ilimu kwa Vabajuni, ili ni shani hakika

6. Ṯukifikisha haṯima, kuisoma Quruani
   Kwenda shule ni ladhima, chukiṯoka namba wani
   Nasi eo ni ladhima, ilimu kuisamini
   Ilimu kwa Vabajuni, ili ni shani hakika

## Ilimu

***Famau Ali Famau***

1. Vedhangu ninavayudha, kauli angu shikani
   Mola amechuhimidha, ilimu chuṯafuṯeni
   Ilimu ni muangadha, akhera na duniani.

2. Kuruani mehimidha, ni faradhi chusomeni
   Vanaume kuikadha, na va kike pia ndani
   Ilimu kuiṯafudha, ni ladhima haṯa Swini.

3. Mwene ndia kufulidha, a kuenda masomoni
   Humsahali muwedha, ndia a kwenda peponi
   Nami ndugu nahimidha, kwa bidii chusomeni.

4. Ilimu ni mwangadha, akhera na duniani
   Hukuṯoa kwenye kidha, ikakuṯia dirani
   Uinga unaṯukidha, binadamu chusomeni.

5. Illahi anavulidha, kwene ake kuruani
   Aivaye ṯosheledha, na asoiva yakini
   La, havako sawidha, mbora ni vasomeni.

6. Ṯamaṯi nimemalidha, beṯi siṯa mebaini
   Oṯe niliovayudha, yachieni akilini
   Ilimu ni muangadha, akhera na duniani.

## Ilimu ni Muangadha

***Swaleh Omar Mohamed***

1. Ilimu ni muangadha, ufunguo wa maisha
   Kwene ndia hukwekedha, mangi hukuelimisha
   Hukuṯowa kwene kidha, na cheo kukupandisha.

2. Ilimu ni manufaa, a dunia na ahera
   Maishani hukufaa, ikakupa na siṯara
   Piya hukupa shifaa, kwene kinga na busara.

3. Ilimu ni muamko, hukuṯowa uingani
Huecha mabadiliko, miyini na mashambani
Huegemwi na sumbuko, huva raha maishani.

4. Ilimu ndio nlango, wa kungiya na kuṯoka
Ukosapo huva ṯongo, samani ako hushuka
Wendapo huna npango, hukomi kudhalilika.

5. Ilimu ndio ni ngudho, iloshika ṯandu dhoṯe
Abadani machachidho, hayasibu kwa loloṯe
Hukupa na malivadho, kufurahi siku dhoṯe.

6. Ilimu kwechu ni ngadhi, akupanda na kushuka
Hukuchia kwene kadhi, vuso ukanawirika
Ukachamba wadhi wadhi, kwa raha kumakinika.

## ILIMU

***Khalid Omar Kanjenje***

1. Naṯaka kuṯakalamu, machache kuyabaini
Kwani yana umuhimu, chukichia akilini
Kwa upande wa ilimu, Bajuni ni namba wani.

2. Si kwa upande wa dini, na vala kwa a dunia
Kwa kweli isi Bajuni, nno chumeendelea
Ṯumekuwa namba wani, na bado chwaivunia.

3. Ni mashehe mbalimbali, ṯumevaṯoa Bajuni
Na walimu wa sukuli, vayee ṯele nchini
Na madakṯari kweli, wako masipichalini.

4. Chunao maprofesa, ambao vayulikana
Na pia vanasiasa, vaeṉee kila aina
Na uyudhi wa kisasa, Wabajuni ṯumefana.

5. Piya chuna mameneja, Vabajuni valosoma
Hufanya kadhi kwa haja, kwa imani na huruma
Voṯe chwawavisha koja, kwao ilimu daima.

6. Beṯi siṯa na fupisha, nimefika kikomoni
Haya nalovayulisha, nadhani mumebaini
Kwa ilimu chunaṯisha, ilimu ni namba wani.

## Ilimu Kwa Vabajuni

***Mzee Athman Shee***

1. Chulivuka na vahina, makwechu chulipoṯoka
Fani dha kila namna, havakuvuka mipaka
Valo nyiva rabana, mashehe valochayika.

2. Valochufunda ilimu, dha sayari na dha ṯiba
Umuhimu wa nidhamu, na dhakula dha ruṯuba
Nasi chukava na hamu, kunsoma Mola Raba.

3. Valichufundra imani, nyoyo dhikankubali
Chuiṯenge na sheṯani, na dhilla dhau dhalili
Chuifundre a samani, na ilimu mbalimbali.

4. Valichusomesha dini, awajibu na shariya
Dha swala misikichini, na mema kuifanyiya
Chuka n yiva manani, nasi chukanyenyekeya.

5. Chulidhisoma ibada, Mola kunilinganiya
Chupache yenye saada, duniyani na khiraya
Haṯa dha kukeṯi eda, dhoṯe valichupangiya.

6. Na hapa ninahaṯimu, mwisho nimesikiliya
Ni wajibu kufahamu, amri dhake Jaliya
Basi chusome ilimu, chudhiive njema ndiya.

# Ilimu

*Fahad Mahadhi Kombo*

1. Mola alimuamuru, yambo la kwanda nabiya
   Ili asinkufuru, asome alo na ndia
   Asifanye a kudhuru, mwisho akaiyuṯia.

2. Ilimu ilipokuya, dhamani valisusia
   Kusoma valikimbiya, haswa ile a dunia
   Vakadhani vandakuya, mila kuvaharibia.

3. Baada ya ṯafakuri, ṯanabuhi ikangia
   Vakakiṯoa kiburi, uinga kuufagia
   Ṯena vakachia ari, ilimu kukumbachia.

4. Imeshamiri ilimu, a dini na a dunia
   Kwa vabajuni kaumu, kwa kule kusuluhia
   Yasomewa kwa nidhamu, kushoṯo kuvuli pia.

5. Kila nyanda mehiṯimu, ṯena vamedhiuliya
   Nyadhifa pesi na ngumu, nyingi meinyakuliya
   Kwa uwedho wa karimu, uraisi ṯavaniya.

6. Uongodhi meikimu, viongodhi huṯauwa
   Kwa kuchumia elimu, pasi na a kubaguwa
   Ndhuri avo haṯamu, mambo amekuva sawa.

## Ilimu Muhimu

***S.A. Bin Abeid***

1. Ilimu ni uṯukufu
lau chuṯafikiriya
ni ṉingi ake sharafu
kachika hii duniya
aso ilimu ni dufu
popoṯe anapongiya

2. Ilimu ni njema jaha
lau chuṯadhingaṯiya
na ṯena ni ushujaha
kwa maringo huṯembeya
ndrio ngavo a silaha
a ncẖu kuponraniya

3. Ilimu ni ḵichu chema
maishani navambiya
chenye hadhi na hishima
na daraja aa aliya
fahari na ṯaadhima
kwa alie isomeya

4. Na sifa a mwanadamu
avapo kwene duniya
ni mwene nalo ilimu
chuvoni aloingiya
duniya humfahamu
kila anapoṯokeya

5. Na mweṉe kuipa ṯabu
akava aṯaṯembeya
ilimu kuiṯulubu
apache kuisomeya
ni faida na sawabu
ya ahira na duniya

6. Ilimu chuisomeni
vabajuni navambiya
kwa jidihada na shime
isi piya kwa umoya
chusive magume gume
uinga ḵichu kibaya

7. Vaume na vanawake
naṯaka kuwaambiya
ni wajibu chukumbuke
ilimu kuisomeya
na kwa hili chusichoke
suṯe chumefaridhiwa

8. Mangi siṯoyakariri
hapa nanga niṯachiya
ilimu nimehubiri
nani mumenisikiya
na chuchieni nadhari
chusiandame kudhiya

## Faida Ake Ilimu

*Jamila Ali Haji*

1. Kuna meko ni muhimu, vachu vachachu pamoya
   Mwanafundi na mwalimu, na ndhadhi nawe piya
   Mukishika majukumu, malengo aṯaṯimiya
   Faida ake ilimu, ndipo chuṯafurahiya

2. Huvanasihi vadhadhi, musichoke ipindeni
   Nani vema dhiongodhi, mavadho mema vapeni
   Majukumu a uedhi, vasiaaṯe ndiani
   Vachuee kwa mapendi, chufaulu maishani

3. Mdhadhi vucha haṯuwa, usikilie wendapo
   Na mwalimu chwaelewa, ni nsaada akivepo
   Pamoya nyoyo dhikiwa, chuṯapacha chuṯakapo
   Mmea ukilimiwa, ndipo mavuno ayapo

4. Inyi pia kihakika, muchuvonapo ndiani
   Hufaa kuwajibika, kuchuhuji kwa makini
   Mbona uwe hudhunguka, kwenyu una ṯabu gani?
   Maishani kipochoka, nyani wamo hasarani?

5. Manafasi huṯokea, a kadhi sirikalini
   Vana huidhungukia, huranga ṯu miyini
   Kulipa huchuemea, kwa kuva ni masikini
   Sasa mbona huṯedhea, bure hachuisamini?

6. Mikono chushikaneni, vana na vachu vadhima
   Maovu chukanyaneni, chukumbusaneni mema
   Nasi chubadilikeni, nyendo njema kuandama
   Chumwepukeni sheṯwani, kuva hana mwisho mwema

# Nlango a Siṯa: Ṯabiya dha Kiuchu

## Uchu Ukikuponyoka

***Quswai Sufiyani***

1. Vajamali, yani minawe kuchecha
   Na ngalili, hakikai kiso kacha
   Ni mivili, ipakanao mafucha

2. Hui nchu, uchu ukikuponyoka
   Nawe kachu, sipende kukasirika
   Mila echu, hufurahi na kuṯeka

3. Nchu bora, husaidia ndudhake
   Na hasira, hakubali dhimfike
   Na kukera, huva si ṯabia ake

4. Akipacha, neema dha mola vake
   Uṯakucha, hawedhi kula e pweke
   Na kuyuṯa, awaudhipo ndudhake

5. Eo nasi, chuwe na uchu jamala
   Chuikisi, chuepukeni a ila
   Pa harusi, usikimbilie kula

6. Samahani, ivapo nimekuchusa
   Nṯu duni, ayasamini mapesa
   Hana dini, uchu wake meukosa

7. Kadi ṯama, nimefika kikomoni
   Nilosema, yachieni akilini
   Himahima, uchu mbee chuwekani

## NDUDHANGU

*Omar M. Maulana*

1. Ruhu angu sina raha, kwa mambo yanipecheo
Nndaikosa furaha, kwa ndudha vanichendao
Vandadhidisha karaha, lindadhidi kero lao,
Ya Ilahi nakuomba, nepushia baa dhavo.

2. Havanilichi kuyala, usingidhi naṯamani,
Chakula imi nikila,sina amani chumboni,
Hunibikia salala, ili nive mashakani,
Ya Ilahi nakuomba, nilinda na ndimi dhavo.

3. Imi nikifanikiwa, hukachika chumbo dhao
Kiya kuharibikiwa, vao hufanya dhikao,
Naiva ni majaliwa, undapanga Mola vao,
Ya Ilahi nakuomba, niṯenga na dhicha dhavo

4. Vandaungana vavuli, na vanavake pamoya,
Sihiri ndavo amali, kwa vaganga hulipiya,
Hukila changu kivuli, maovu kunifanyiya,
Ya Ilahi nakuomba, dhisive sihiri dhavo.

5. Si nṯana si usiku, havachoki kwenda mbiyo,
Mara huku mara huku, huamini vambiwayo,
Kuwa imi vanishuku, haya ndiyo vanenayo,
Ya Ilahi nakuomba, dhidhibiṯi ndimi dhavo.

6. Havapendi kunivona, hunivona kama noka,
Kwavo kupacha kusona, ndimi duniya kuṯoka,
Hapo ndipo vaṯavuna, kila changu kukiṯaka,
Ya Ilahi nakuomba,dhiepushe njama dhavo.

7. Ni wajibu chupendane, isi vana va Shelali,
Na mema chuchendeane kwa wingi na kwa akali,
Na maovu chukanyane, vayukuu va Nyalali,
Ya Ilahi nakuomba, dhibadili nyendo dhavo.

## Bajuni ni Vadilifu

***Swaleh Omar Mohamed***

1. Bajuni ni vadilifu, kwa vadhee hadi vana
   Huchenda au fanifu, madhuri kuekedhana
   Vachu vangi huchusifu, kila chwendapo shindana.

2. Yambo a uṯamaduni, makwechu huendelea
   Kwa sharia na kanuni, sana kudhiandamia
   Kuṯoka hoko dhamani, nasi chundolipokea.

3. Mkuru mwiche abawa, ama abaya kwa ina
   Hunicha avu mpwawa, mume bwana mke nana
   Bibi, babu nyukuwa, maina kuviliana.

4. Huṯoovodhwa havule, kama hukusuluhiya
   Alianda choka kale, hadi sasa hendeleya
   Mipango ni ileile, vadhee valochwaṯiya.

5. Nke hufundwa kupika, mapisi kila aina
   Amijisi akupaka, na dhakula dha maana
   Na chumbani kadhalika, akankarimu bwana.

6. Ṯamaṯi vakisafiri, vakenda dha Arabuni
   Husafiri kwa bahari, kwa changa bila mashini
   Kwa dharuba na shuari, huegesa bandarini.

## Uchu

***Fahad Mahadhi Kombo***

1. Ni mpole mbajuni, na nkarimu kwa kweli
   Changu jadi na dhamani, namba wani kwa kujali
   Hana dharau yakini, hapendi mambo kufeli.

2. Haupendi udhalili, si kwake hadi kwa ndue
   Aṯafanya kila hali, yambo hilo aondoe
   Ṯena bila a kujali, garama dhoṯe aṯoe.

3. Anapokuya ṉgeni, humwekea ake hadhi
Hunchia akilini, ili asimbughudhi
Dhawadi hini na hini, hupawa kama faradhi.

4. Huyawaṯa mambo avo, ṉgeni asighurike
Na kuchuma vana vavo, mambo asiharibike
Hini ndio jadi avo, fadhila vadhianike.

5. Yambo linaponsibu, huva si la pweke ake
Ndugu dhake mahabubu, hamuaṯi awe pweke
Aṯasaidia babu, hadi vayukuu dhake.

6. Machangani harusini, voṯe vanajumuika
Ni vigumu kubaini, upi ndie muhusika
Meriṯhi ṯabia hini, kwa miaka na mikaka.

## Dhingaṯia Mwanadamu

***Zuwena Ahmed Mohamed***

1. Uipendao duniya, na kacha ake nunuwa.
Upache kuṯukuliya, kiwedha kuiṯukuwa.
Vangi vandaimbiriya, nami haikunichuwa.

2. Nami haikunichuwa, kwa sana kunihadaa.
Ikee kana mauwa, mara moya husinyaa.
Ndripo nami kaṯauwa, kaenga a kunifaa.

3. Kaenga a kunifaa, nisingie hasarani.
Siṯaki kuchundruvaa, kanshiriki sheṯwani.
Maana huchuhadaa, a haki hachuavoni.

4. A haki hachuavoni, kwa kupenda a haramu.
Huichia mashimoni, kwa dhisidhokuva ṯamu.
Dhiṯachuchia mochoni, Chusipochia fahamu.

5. Chusipochia fahamu, sana chukaghafilika.
Dhiṯaongedheka hamu, dha maovu kuaṯaka.
Basi kaṯiṯi ni ṯamu, Rabbi chupe muafaka

6. Rabbi chupe muafaka, chuapangao aṯimu.
Dhichuyie dha baraka, na neema kiladhimu.
Chuaishi a fanaka, maisha aso wadhimu.

## ṮABIYA

***Abdalla Ali***

1. Nda badilaka ṯabiya
Jirani wanṯukiya
Ukali kunṯoleya
Hujali kundhuliya
Uchafu kunsuliya
Chuive chundakoseya

2. Ṯabiya ndakuva mbovu
Umedhidi uṯukivu
Chumeshinda haṯa ndovu
Na machukano maovu
Nshendi na mpumbavu

3. Humfukudha ayao
Hunrudisha kwa mbio
Haa chufanyao sio
Chuṯabaki na kilio
Ndhee akudhaao
Na voṯe vakushindao

4. Ṯabia ndaharibika
Kwa shembee na mashoka
Na nduwo ukinshika
Na polisi kunpeka
Kwa huu nnaloṯaka
Aniiva kwa hakika

5. Vaume na vanavake
Kila nchu ana lake
Ndani heri usiṯoke
Nyamaa usiṯamuke
Ama kwako kampeke
Ya kale nachuyashike

6. Ṯabiya ndakuva duni
Hukeṯi voṯe ndiani
Havendi nsikichini
Jamani mpaka lini?
Mii echu iengeni
Chusiveni hayawani

7. Hachuvudhanyi habari
Kimechudhidi kiburi
Isi voṯe hachujeri
Kwa loloṯe nṯayari
Harufu sidho ndhuri
Hii sio dasiṯuri

8. Kachika hini duniya
Na balaa dhoṯe piya
Nguvu chunadhichumiya
Anyukao husikiya
Chuaṯeni ndavambiya

9. Hodi ukiisikiya
Bila ya kufikiriya
Na dhibadili ṯabiya
Chukenda kwake Jaliya
Akiya kunyukiya
Heshima kuvavekeya

10. Hili nachulikubali
Kuvuana hachujali
Chndakuva madhalili
Kama chuso na akili
Kwangu niakeṯi mbali
Imi ni simba rijali

11. Hachuna bora ṯabiya
Kachika hini duniya
Hukeṯi pweke kiliya
Karibu ukamwambiya
Ndivo uṯafanyahiya?
Mababu valochwaṯiya

12. Vana vandaharibika
Mashembee vandashika
Ni bure uṯasumbuka
Hachuna kubadilika
Sikiṯiko hukushika
Hachupendani hakika.

## Uchu Kichu cha Maana

***Zuwena Ahmed Mohamed***

1. Uchu kichu cha maana, ndruangu ukiushika
Ni yambo la kiungwana, popoṯe likifanyika
Kwa vema chukishikana, nasi chuṯaimarika

2. Sisamini kichu mwana, kushindra uchu hakika
Iṯahidi kukadhana, upache kusiṯirika
Na ndrudho muṯapendana, nyoyo dhiṯamakinika

3. Madhuri kudhaniana, ruhu dhiṯawaswiika
Pia kusaidiana, kupendana kadhalika
Na faraja kupanana, ndruo anapodhikika

4. Aṯani kujepeana, madhila aṯavafika
Haki mukichendreana, undrugu muṯaushika
Na pema kuekedhana, chuṯakapo chuṯafika

5. Chuvasaidie vana, wa ndruo mbwako hakika
Duniya ikivabana, nno vaṯababaika
Palipo bora havana, iyu echu kuvashika

6. Chuvahishimuni sana, vadhee hufurahika
Huchuombea Rabbana, na dua dhikasikika
Neema hushukidhana, kwa wema chukivashika

# Nlango a Saba: Dini

## Duwa

*Abdalla Ali*

1. Mola wangu ichikiya
Kwako nindakuiliya
Dhiki dhimechuemeya
Rabbi t̲achusahiliya
Hidhi t̲abu dha duniya
Hushwindi Mola Jaliya

2. Huomba huku chwaliya
Simama nasi Nabiya
Kula chulilokoseya
Dharubu ndachudhidiya
Ndiwe ut̲achudhimiya
Kwechu lilobakiya

3. Rabbi Mola chuawini
Asichushinde shwet̲wani
Chuko kwako nlangoni
Kula kilicho na shani
Uchupe Mola manani
Chusamehe Ramahani

4. Kwa jaha ake Amini
Chwangoja ako auni
Kula alo kichandani
Rabi mpe afueni
Duwa zechu chuombeni
Rabbi chuve sit̲arani

5. Chunakuomba kudusi
Muumba ulo mkwasi
Chuepushie ibilisi
Dhichudhe dhechu nafusi
Chusiyafanye maasi
Kuikosa firidausi

6. Huliya isi huliya
Chwaiva chumekoseya
Kwako chundakimbiliya
Isi hukusujudiya
Rabbi uishe udhiya
Udhime mocho Jaliya

7. Duwa dhangu nabaini
Nimebisha nlangoni
Dhimechudhidi dhifwani
Mbwachuafu Rahmani
Kwechu dhit̲akwisha lini?
Dhiwe kunfayakuni

8. Shida dhindachudhunguka
Chuepushie mashaka
Nsamaha chwaut̲aka
Moyoni mocho huvaka
Kula saa na dakika
Chut̲ubu kwako Rabuka

9. Vana na vadhee piya
Mochoni kut̲ochuchiya
Ndilo chwaomba Jaliya
Ilahi t̲achondosheya
Mwilini yenye udhiya
Isi chumekukoseya

10. Ilahi pokeya duwa
Ilahi chupe afuwa
Vagonjwa uvape dawa
Ndiwe ut̲achuokowa
Chupache kunusuriwa
Uchupe na t̲aquwa

11. Hachuchoki kukariri
    Isi uchujazi heri
    Nlani ewe kahari
    Chufanye yalo madhuri
    Yakukuridhi Jabari
    Chuchie na Muhuṯari

12. Na maṯodhi huchusuka
    Kwa madhila na mashaka
    Sichufukudhe hakika
    Rehema dhako chwaṯaka
    Chuchilie muafaka
    Peponi kupundhika.

## Chambua Mola Mmoya

***Yusuf Kassim***

1. Pindi aombapo nja, kumuomba Mola vake,
   Akava na kubwa haja, kwengine asiipeke,
   Akanena ni mmoya, Mola mwondosha upweke,
   Chambua Mola mmoya, hanṯupi n̠ja wake.

2. Ule alodhulumiwa, kafanywa asononeke,
   Malidhe akajepewa, hakidhe kupigwa ṯeke,
   Na n̠imbo akaimbiwa, dha kuṯoa ṯodhi lake,
   Chambua Mola mmoya, hanṯupi n̠ja wake.

3. Nja akanena heri, ninaye aliye pweke,
   Akenda nena kwa siri, yeye ṯu na mola wake,
   Mola hunena subiri, vala usihangaike,
   Chambua Mola mmoya, hanṯupi n̠ja wake.

4. Kama sio duniani, vaṯakapokwenda kwake,
   Siku hiyo kiyamani, vaṯaomba vaṯoroke,
   Ila haiwedhekani, ladhima vakababuke,
   Chambua Mola mmoya, hanṯupi n̠ja wake.

5. Usingie ubayani, vaaṯe vahangaike,
Nlilie sijidani, na vala usichambike,
Siku moya hadharani, aṯafanya vaumbuke,
Chambua Mola mmoya, hanṯupi ṉja wake.

## Dini

***Quswai Sufiyani***

1. Samahani sikidhani, muyapache a ifadi
Dini ake mbajuni, nda nchumi Muhamadi
Haṯa dhake ṯamaduni, dini hadhikukaidi
Dini waliisamini, vangi mekufa shahidi

2. Haṯa kwavo mahondeni, dini ao meshadidi
Vaendao baharini, wakidhiṯoa nyiradi
Usiku valo numbani, vakiswali ṯahajudi
Dini waliisamini, vangi mekufa shahidi

3. Hidhibu misikichini, ulikuva ni uradi
Kudhiswali rakaṯeni, numbani na masijidi
Kukiyawa darasani, wachu hawana idadi
Dini waliisamini, vangi mekufa shahidi

4. Walivameshika dini, kuvasifu imebidi
Waendapo harusini, hawafanyi ufisadi
Mahavule hawazini, wala hawaṯii udi
Dini waliisamini, vangi mekufa shahidi

5. Ingiapo Ramadhani, kwavo ibada hudhidi
Kuisoma Quruani, ṯena kwa kiṯajuidi
Swadaka kwa masikini, chende na mayi baridi
Dini waliisamini, vangi mekufa shahidi

6. Mwisho va wangu uneni, kunyamaa sina budi
Nilochaya apimeni, kukoma imenibidi
Hela nasi chwangojani, kurudi kwake wadudi
Dini waliisamini, vangi mekufa shahidi

## Maisha

*Famau Ali Famau*

1. Bismillahi isimu, Rabi nakulingania
Na chumwa wako Hashimu, faradhi kunswalia
Na swahaba akiramu, ṯabi ṯabiina pia.

2. Akidhawa mwanadamu, Mungu humuandikia
Mambo oṯe aladhimu, hakuna linosalia
Hadi kufika kudhimu, kaburini kuingia.

3. Kula ake ni muhimu, na ajali yaṯokea
Hujaliwa binadamu, maishani na Jalia
Chuendeme chuna hamu, mapesa hupapilia.

4. Ela maisha ya humu, Kenya amechuemea
Medhidi kuva magumu, na ruri alipongia
Vunga mekuva ni sumu, sukari kuidhidia.

4. Halali kuva haramu, kwa bei kuchudhidia
Mekadhika majukumu, dhina dhiki familia
Ṯajenga numba kwa ngumu, kwa chachu asilimia.

5. Churudini kwa karimu, dhambi dhechu kuṯubia
Maisha sasa magumu, ni mibachi huchungia
Siṯamani kunwa sumu, chikichi ṯaikachia.

6. Ṯamaṯi ni vanadamu, nyuṯe muloshuhudia
Mayi meingia sumu, na nocha menikabia
Nikiaṯa ni haramu, na kinwa niṯaifia.

## Uisilamu

*Famau Ali Famau*

1. Bisimilla alonena, kwenye ake Quruani
Kwamba ni kaṯiṯi sana, vashukurio hisani
Chunafaa kulingana, na aṯakavo Manani.

2. Ni Bwana Mola Rabana, kuabudiwa yakini
Dini dhingava shehena, vahindu na baniani
Dini ilo na maana, nchu kuva muumini.

3. Uisilamu hunena, kuchufunda ikhiwani
Duniani vaungwana, ni chumba cha nṯihani
Yachupasa kukadhana, kumuabudu manani.

4. Ngudho ni ṯano bayana, za dini a Rahamani
Shahada yaivikana, na swala ina ṯhamani
Dhaka, maka nenda sana, na kufunga ramadhani.

5. Yahimidha kupendana, dini ake Rahamani
Hisani kufanyiana, na kuvonyana imani
Kwa mema chukishikana, chuṯaingia peponi.

6. Sana kusalimiana, isilamu duniani
Na hali kuiviana, inde na nsikichini
Ṯhawabu ṯapacha sana, na chuṯangia peponi.

7. Ṯamaṯi ni kushikana, na kamba ake Manani
Kwa umoya kuengana, na kusaidianani
Kuaswi ni mbovu sana, mwovu ṯachiwa mochoni.

## Dini ni Uadilifu

***Swaleh Omar Mohamed***

1. Dini ni uadilifu, huchufunda mambo mema
   Huondowa ṯakilifu, vachu kuishi salama
   Huchufanya vanadhifu, kila chunaposimama.

2. Dini huchupa mongodho, kwene sawa kuchwekedha
   Hepukana na midhodho, huchwandolea bughudha
   Kwa mema chufanyanadho, huchuṯowa kwene kidha.

3. Dini huchwecha pamoya, vachu kushirikiana
   Madhicho kuchuemeya, kwa huruma hupanana
   Maovu huchwandokeya, chukadhidi kipendana.

4. Dini huchupa ilimu, haki kuisimamisha
   Mabongo akafahamu, a sawa kubainisha
   Dini akiislamu, ndio dini a maisha.

5. Dini kuhishimiana, kwa mashehe na valimu
   Vachu vadhima kwa vana, hufundishana kwa hamu
   Ndipo huya kupendana, kwa furaha na nidhamu.

6. Dini echu chwaipenda, maneno ṯaafupisha
   Mambo mema huchufunda, suṯe huchufaidisha
   Ndipo nasi huipinda, vangine kuelimisha.

## Dini

***Khalid Omar Kanjenje***

1. Chukiangalia dini, kwa Bajuni ni haswaa
Hachukudharau kwani, kwechu ina manufaa
Kwa kusoma Qur'ani, Bajuni wamechangaa.

2. Sifikihi sikwa sera, Bajuni wamebobea
Wamesimama imara, ahlaki wachumia
Ṯarehe kwavo ni bora, soma wamelidhowea.

3. Kwa hadisi dha nchumi, wandadhihifadhi sana
Kwa hakika dhao ndimi, husoma kula aina
Kaṯu kunena sikomi, ni mfano va maana.

4. Na hafidhi Kuruani, vao vameihifadhi
Isi voṯe Vabajuni, chumepacha kubwa hadhi
Wakenda mashindanoni, masomo ao huridhi.

5. Chuna bora maimamu, vene ilimu ya dini
Ṯena valio muhimu, na koṯe misikichini
Wamelangacha jukumu, kwavo wao waumini.

6. Hapa sasa nasimama, mangi siṯayabaini
Naweledha himahima, muyachie akilini
Kachu hachurudi numa, haswa kwa mambo a dini.

## Dini yambo la aula, chufuache vaumini

*Fahad Mahadhi Kombo*

1. Yambo la kuivunia, la pamoya Vabajuni
   Mola mevajaalia, kuva moya avo dini
   Ya suna dhake Nabia, na ale a Quruani.

2. Jamii ilosifika, si pwani hadi barani
   Kwa kule kuilimika, kuiyiva avo dini
   Sifa hii mesifika, kwa miaka miaṯeni.

3. La midhodho kivafika, huchachuliwa kwa semi
   Dhake Ilahi Rabuka, na hadiṯhi dha nchumi
   Suluhu kwavo hufika, bila kiṯhone moyoni.

4. Imamu ake nafasi, ni kuvu kweṉhe jamii
   Ni muhali kumuasi, huna budi kunṯii
   Mweṉhe huecha nuhusi, lake yambo hafikii.

5. Ingiapo Ramadhani, vanafunga vaumini
   Uṯavona dhisahani, magharibi kiadhini
   Dhipekwadho majirani, vafuṯuru majumbani.

## Muongodho Dini

*Zuwena Ahmed Mohamed*

1. Muongodho dini, kwa dhivumbe voṯe
   Ndechu vaumini, va ṯabaka dhoṯe
   Nachuishikeni, chufuache oṯe
   Chusiipudheni, si kana loloṯe

2. Ishike mwendani, kwa raha na kiṯe
   Uichie ndrani, wala siisiṯe
   Uve ibadani, kaṯu usiaṯe.
   Changu uchochoni, huabudu suṯe

3. Ni misikichini, isilamu voṯe
   Na makanisani, vakirisṯo nyuṯe
   Hwendra hekaluni, muhindi yoyoṯe
   Dini ni kanuni, shika sidhiaṯe

4. Hapa duniyani, Mola simuaṯe
   Iva muangani, maovu aaṯe
   Dini ni sukani, a kwendra popoṯe
   Basi ngia ndrani, sive koṯe koṯe

5. Siṯake uhuni, dini ikamache
   Iko dhiṯabuni, chako kifuache
   Sio dha kubuni, siifanye piche
   Ila maluuni, hafuachi oṯe

6. Niko kikomoni, wa shairi loṯe
   Achie maṯoni, haa siasiṯe
   Senendre mochoni, dini siiaṯe
   Nveke vusoni, Mungu simuaṯe

# Nlango a Nane: Historiya

## Ni Kadari Ake Mola

*Yusuf Kassim*

1. Naanda na Ishakani, ilio mwisho a Kenya,
   Mambo ake si mageni, kila nchu alivona,
   Valikimbia nyini, vakaaṯa a maana,
   Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

2. Pili ni mui Kiunga, mashifṯa valivachesa,
   Pamoya na kuvagonga, bila kuiva makosa,
   Kugura valiipanga, pakwenda havakukosa,
   Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

3. Dha ṯhamani kumbiriwa, majumba kubaki pweke,
   Na wisha nao ukava, ndio chakula cha peke,
   Uṯumi nao ukava, hakuna alo na chake,
   Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

4. Na widhi ukaṯokea, Kwa vachu kujepeana
   Dhahabu dhikapoṯea, na mali kila aina,
   Hasara iloṯokea, ṯhamani ake hakuna,
   Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

5. Mui wechu wa Mwambore, ni aridhi a ruṯuba
   Dhakula huchenda bure, kwa masholole sihaba,
   Na kuchunanga kaure, ndio Kwa vana kushiba,
   Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

6. Vachu na vana dhidodi, valichekwa nyara,
   Huya akapija hodi, nyani hunena “dhahara”,
   Karama ni mahasidi, vaṯaka kukugangura
   Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

7. Kuna vangine sichai, vakevo valivamiwa,
   Maṯoni vakishiṯai, ukaṯili vakipawa,
   Rubu nao kuva hoi, vengine vakapagawa,
   Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

8. Mii oṯe a Bajuni, kila nchu ana lake,
Yaṯaka sana makini, kueleza mambo ake,
Ṯena ive ni mpwani, wa hilo kabila lake,
Ni kadari ake mola, nja hawedhi kupinga.

9. Hapa sasa hukomea, mwisho wa shairi langu,
Kama nindavakosea, nisamehani ndudhangu,
Bado mi siyaṯimia, alokamili ni Mungu,
Ni kadari ake Mola, nja hawedhi kupinga.

## Alopicha alipicha lakini huakumbuka

***Fahad Madhi Kombo***

1. Bismillahi nda kwanda, kauli ya kuandiya
Uṯakalo kulichenda, Rabi hukubarikiya
Na hilo chwaliifunda, kwa suna dhake Nabiya.

2. Aliṯukuka Bajuni, barani na pwani pia
Alivemo Sulṯani, kesi kivahukumia
Gafula ndani iṯoni, kijaa kikavangia.

3. Ukangia ukorofi, aridhini wakachiya
Vakaaṯa malighafi, ruhu dhavo kukimbiya
Na kupaa kama sufi, kwa Shifuṯa kuvamiya.

4. Janibu validhovemo, Vabajuni asilia
Kukangiwa kwa yahomo, vakuṯoka Somalia
Kuharibu dhalovemo, kwa mabavu na afia.

5. Ndarandara kwalikuva, dhijiji dhikapoṯea
Sendeni vakavaṯova, Rubu, Nvundheni pia
Vakamidha kama ṯeva, Simambae navambia.

6. Ilikuva na madhuri, mangi a kuṯamania
Aṯokao kwa bahari, si yasi maema pia
Ukulima mashuhuri, dhoṯe dhikachekechea.

## Machukio

*Quswai Sufiyani*

1. Bismillahi Manani
Mikono angu iṯani
Dua angu kwa yakini
Rabi niṯakabalia

2. Mecheseka mbajuni
Kugura kwake numbani
Kaaṯa dhilo samani
Bila a kuṯarajia

3. Shungwaya na Mvundeni
Mwambore hadi Shakani
Zilidhechu masikani
Suṯe chukiivunia

4. Vakayaa mafaṯani
Kakosekana amani
Chukabakia vageni
Huku chulokimbilia

5. Sababu hachudhioni
Dhakuchuṯoa numbani
Aridhi dhene samani
Mebaki hisṯoria

6. Dhuluma dhiso kifani
Chulofanyiwa vendani
Hini si haki jamani
Hakuna va kuchechea

7. Ya illahi chuauni
Churudi kwechu numbani
Aridhi dhene samani
Ṯurudi kudhikalia

8. Kuifanya njama hini
Ni serekali yakini
Ṯayanena hadharani
Soṯe ṯulishuhudia

9. Nasi eo chwaṯamani
Kurudia masikani
Upiya chwende kubuni
Neema kuchuenea

10. Shifṯa valo mwichuni
Valokuya mahondeni
Kuchuponda hadharani
Mbona eo mepoṯea?

11. Sichufanye majununi
Mufanyao hachuvoni
Walakini chwaamini
Mola aṯachulipia

12. Heri nikome uneni
Nnadho ningi hudhuni
Kuṯoroshwa masikani
Yechu chuloidhoea

13. Na suṯe chunaamini
Haṯochuaṯa manani
Haṯa nyaka ṯisaini
Haki chuṯaipachia

## HisṮoria a Mbajuni

*Famau Ali Famau*

1. Kwa jina lake mwenyedhi, shairi naliandia
   Nieledhe kumbukidhi, mambo alivochukia
   Vabajuni a maudhi, mambo valiopichia.

2. Ni nyaka nyingi na nyedhi, kachika hisṯoria
   Paliṯokea vangodhi, Somaleni kuishia
   Ni va shungwaya vakadhi, vabajuni asilia.

3. Va arabuni makadhi, ndipo alipoṯokea
   Changu dha uchumwa endhi, au haṯa kabulia
   Kuvuana havawedhi, ngodhi vakakimbilia.

4. Mbajuni laadhidhi, falume aloṯimia
   Suluṯwani mwene endhi, shungwaya akaguria
   Vagalla vafumanizi, vakenda kuvavamia.

5. Si kwamba dhicha hawedhi, bajuni ni maridhia
   Akaikubali kadhi, shungwaya kuvaguria
   Kakadha dhake pumudhi, ufuo kuandamia.

6. Ni mrefu si upudhi, ufuo wa Somalia
   Kufuwacha kiuyudhi, vangine vakisalia
   Hadi vakaṯusa odhi, miini kusikilia.

7. Ṯamaṯi ni kwa dhishadhi, maguro yao sikia
   Vabajuni changu endhi, valikiishi shungwaya
   Vagala dhicha vishendhi, vakenda kuwavamia.

## Hakuvalipa Kichu

*Swaleh Omar Mohamed*

1. Ṯaanda kukibaini, kisa kuvasumulia
Valokiishi miyini, makini bila udhia
Havakuvadha mwishoni, shifuṯa kushambulia.

2. Mamboye husikiṯisha, bajuni kuvavonea
Kinena huvachonesha, hasara ilovangia
Hakupacha kugurisha, mali oṯe kupoṯea.

3. Kwali ni kuwi na Rubu, Mwambore na Mvundeni
Valikuchishwa dharubu, Simambae na Sendeni
Voṯe valipacha ṯabu, Kiunga na Ishakani.

4. Vali na vana dhidodi, na vangine machumboni
Risasi dhikishadidi, kikimbilia mwichuni
Kupoṯea hana budi, na vanavo dhivekoni.

5. Sababu chukivudhana, hachuyisi paka sasa
Unyonge umechubana, hachuvoni la makosa
Ṯavalipia Rabana, kwa madhicho kuvakusa.

5. Ṯamaṯi amaṯokeo, vakuṯemene ndrudhechu
Changu lijiri chukio, kuvonewa vachu vechu
Sirikali paka eo, haikuvalipa kichu.

## Yaliowapaṯa Vabajuni

*Khalid Omar Kanjenje*

1. Nyaka siṯini na chachu, shida ilichufikia
Kupacha uhuru wechu, Kenya kuiṯegemea
Ilipikwa miyi yechu, nawalo maharamia.

2. Ṯavayudha eni vachu, kwa makini ṯachasuwa
Yalinikumi na chachu, miyi aloshambuliwa
Valipokwa kula kichu, na ṉumba vakavasiwa.

3. Baadhi ṯaibaini, miiye alongiliwa
Ashuei Mvundeni, na Sendeni kuvamiwa
Kiunga na Ishakani, na Rubu wakaṯolewa.

4. Ilibidi kukimbia, kuvukia dhijijini
Vakabuniwa upia, kuishi kama vageni
Ni Shanga valishukia, na vangine change chini.

5. Valibaki na mavadho, vangine kuchunduvaa
Kadhi vadhifanyadho, hadhi vamalidhi ndaa
Hachuvoni muongodho, sirikali kuchufaa.

6. Kiswa hichi ni kirefu, siṯokimaliza sasa
Vala siṯoikashifu, sirikali mepukusa
Ṯavalipiya Raufu, kuvakusisha mikasa.

## HISṮORIYA

***Mzee Athman Shee***

1. Nimekuya nivambiye, nambe nalokusudiya
Nambe nivachasuliye, maovu valoafanya
Ulimi vachukasiye, na madhila kueneya.

2. Ulimi vachukasiye, hiyo nda kwanda hiyana
Madhara vachuaṯiye, siri hachunavo ṯena
Dha kwavo vadhisuṯiye, dhavo siri huyivana.

3. Amechuvumba Manani, makabila chuyivane
Kwa rangi enye samani, na ulimi chuyivane
Na kwa umbile la shani, si veusi si wanene.

4. Meṯuvumba Rahamani, ṯafauṯi dhechu ndrimi
Makabila duniyani, chuyivane kwa ulimi
Huvaye kwa mbajuni, kwa luga haisimami?

5. Sio la kwanda aridhi, hiyana kuchufanyiya
Valikuchana vayudhi, luga kuchuharibiya
Vakachuvaṯa wadhi, kwa aṯakavo kungiya.

6. Chuṯakuvaye ni vachu, kabila chusisikiye
Chusiyo ulimi vechu, siri chuṯahifadhiye?
Enga na mila dha vachu, dhavo ndrimi wasiṯiye.

## Hadithi ya Kibajuni

***Hassan Msham Mahmoud***

1. Huvaṯoleya hadiṯhi, mupache kupumbadhika
Hadiṯhi ya uwiraṯhi, muwedhe kunufaika
Ili ibaki ṯuraṯhi, kwa veneve vahusika

2. Baada kupicha nyaka, changu mwando wa duniya
Vachu valiṯavanyika, kwa raha na kukimbiya
Ndipo juba kuinyuka, kwa kuandiya Shungwaya

3. Bajuni huuvikana, kwandia hoko dhamani
Na jimbo lake ni pana, kwa bahari na madini
Ni hakika sio dhana, asili ake ni pwani

4. Bajuni imeenea, kwene fukwe dha bahari
Pia bara imedhaa, na imeaṯa aṯhari
Ilikuveko haṯaa, changu vageni kujiri

5. Bajuni iliinyuka, kwa kupichia khilafa
Ikakuwa kwa haraka, kwa nguvu na maarifa
Hadiṯhi hini hakika, ndio imepacha sifa

6. Mwisho nikimalidhiya, hadiṯhi ya Kibajuni
Ni udhuri kuvambiya, ina langu. muiveni
Ni mwana awaeleya, Bini Mshamu Hassani

## Bajuni

*Hassan Msham Mahmoud*

1. Kwanḏa ṯaanda hondeni, nikachie makulima
   Nivalinde na dhijuni, vasinilie nchama
   Ukichukana Bajuni, ichukane kwa kusoma

2. Pili ṯashukia pwani, nende na chambo kuṯoma
   Kisha nenende imboni, vendapo vachu vadhima
   Ukikashifu Bajuni, ikashifu kwa kusoma

3. Chachu ṯanenda dhidhini, niṯunge siku ndhima
   Niṯedhe na hayavani, ninwe madhiwa na nama
   Ukidharau Bajuni, idharau kwa kusoma

4. Iṉe ndao baradhani, nende kasikie mema
   Nikeṯi paka iyoni, pindi yuwa likidhama
   Ukibomowa Bajuni, ibomowe kwa kusoma

5. Ṯanu ṯanenda ngomani, nikachike kila ngoma
   Na niimbe nimbo hini, japo kuva na. koroma
   Ukidhiisha Bajuni, idhiishe kwa kusoma

6. Siṯa ṯanenda chuvoni, nende kaishe. kusoma
   Na mwisho nie n'umbani, nimalidhie hiṯima
   Ukisodhesha Bajuni, isodheshe kwa kusoma

## HISṮORIYA

*S.A. Bin Abeid*

1. Naṯaka kuṯakalamu
nieledhe kwa undrani
huku nishike kalamu
na kuandika bukuni
walivokuwa kaumu
waloishi Ṯikuuni

2. Ṯarihi nimenukuu
kuṯoka kwa vabajuni
ina la upandre huu
laliloveko ndrimini
valiliiṯa Ṯikuu
si eo changu dhamani

3. Yali ni bahari kuu
Hindi ni lakubandikwa
na vachu ni vaṯikuu
ndrivo valochambulika
bara nalo ni Ṯikuu
halikuva Afirika

4. Kaṯu halikusikika
ṯoka dha nima qarini
ina hili Afirika
halikuva kwa bajuni
wala havakuhusika
ni ṯili dhavo vageni

5. Pulikani valimwengu
eo wadhi naṯamka
nieledhe kwa ufungu
mambo enye uhakika
ina hili ni vadhungu
ndrio valichubandrika

6. Ingava chwachambulika
vakadhi hapa barani
nasi chungafarijika
kuichwa afirikani
ina valochubaandrika
ni vadhungu vakoloni

7. Lau chukiṯaamali
kwa makini pasi pupa
si la kwechu ina hili
ṯimbuko lake si hapa
na valio chusajili
wachu kuṯoka uropa

8. Ṯarehe ilivosema
na dhiṯabu kadhalika
kwamba dhilo picha dhama
kamwe halikuchumika
walipokuya varoma
ndrio valochubaandrika

## Mbajuni

### S.A. Bin Abeid

1. Ilahi Mola nkwasi
nipa jaha na imani
niifunguwe kamusi
nisomeshe vabajuni
aive aso kaisi
aelewe kwa undrani

2. Kifumba kupacha resi
hunyuka usindidhini
hutanga angu nafusi
kwa kuvadha ubajuni
valokuva maraisi
kwa kadhi a baharini

3. Si habari dha chechesi
dhitokao ulimini
kwa kasikadhi na kusi
havakuketi miyini
valikuva havakosi
kichoveo cha numbani

4. Katu havakucha kusi
kupundruka mikaoni
vakitoma darakasi
pima mia udhivani
hurudi kwa talibisi
shehena dhimbo dhimboni

5. Na pandre dha mafufusi
hekwa na mbwaragurani
valikitoma kwa misi
a kwa inde na kwa ndrani
mbali vashukao pesi
nyambani na mayavani

6. Hoko pandre dha Ilisi
kiomoni dhigomeni
maleleji vakikisi
matilahi dheituni
vakidhitoma geusi
imbo vakidhisamini

7. Kula aina ya isi
akingiya udhioni
maimbeimbe na tasi
tangu pono vaiveni
vakitoma kwa mayasi
nyambani na mavukoni

8. Eo vana havaisi
kadhi avo a dhamani
mwambie lake upesi
kukimbilia sokoni
hwendra kupimiwa kusi
huchiliwa kikapuni

## Ṯarihi A Kibajuni

***S.A. Abeid***

1. Mwando wake ṯaamali
ṯarihi dhaeledheya
ni qarini dha awali
ndripo chulipoandiya
ṯimbuko lechu asili
liloṯimbuka Shungwaya

2. Si eo changu dhamani
isi chwalichanguliya
chwalikuya kusakini
bara na dhisiwa piya
ṯoka yaa saba qarini
ṯarihi yaa miladiya

3. Na kiwango muafaka
naṯaka kueledheya
ni ṯarihi dhiso shaka
ndripo nikahadisiya
nyaka miya kupunguka
ṯarihi ya hijiriya

4. Hapo chukaṯavanyika
kula pembe chukangiya
ubajuni kupanuka
kidhadhi kikaeneya
na barani chukafika
la kuṯwa na kwava piya

5. Kwa usemi chuna huja
kwa bajuni si mapiya
ṯafauṯi ni lahaja
eṉe ulimi mmoya
kimviṯa kiunguja
na kiamu huchweleya

6. Dhiṯengemene asili
dhalidhoṯoka asiya
makabila mbali mbali
yalishukiya shungwaya
lugha echu kiswahili
na dini echu ni moya

7. Mewapa muhṯasari
apache kuwaeleya
haya naloakariri
nadhani mumesikiya
muhimu hini habari
ipache kuwafikiya

# Nlango a Ṯisa: Uṯamaduni

## Mabarobaro na Jamii

*Mohamed M. Kombo*

1. Ubarobaro ni kiungo muhimu
Hili chwataka nno chulifahamu
Ndrio eo ndrudha kuniladhimu
Kuvapasa habari dha muhimu

2. In'i ndrin'i muchumiwavo
Kuivesha mikao ake nguvo
Kwa ukali wenyu wa mbuvo
Hukosa kujali mambo avavo

3. Yivani ndrini tuka na mwambo
Vakulipa ipaa lilo nalo vumbo
Ivapo basi mutaichia Kh'ombo
Ni kuipondra jamii kwa simbo

4. In'i ndrin'i nchi wanyongo
Usimamishao echu shingo
Na akachaao hili ni irengo
Bila iyo nvili hauna mpango

5. Ndrio siasani mukachumiwa
Nao mikaoni mukatugidhiwa
Musaid'ie uvund'ifu kukuwa
Maisha mupache kuharibiwa

6. Isi haa pia alichusikilia
Kwa kukosa kudhingatia
Ubarobaro chukaumbiria
Ili upudhi kuupondrania

7. Nnenao isi hachukueledhewa
In'i muna bahati eo huambiwa
Ambeleni akikosa kufikiriwa
Uchudhima huya ukayutiwa

8. Pesa dhenyu dha udheeni
Hulia marungi faid’a nigani?
Hutakia bugidhi kupacha nini?
Haa mabarobaro adhingatieni

9. Hwendra kusumbuka kutafudha ipeni
Ukilipacha umpe akh’etidhiyeo n’yini
Akupe uchafune dhijichi na mayani
Huu mabarobaro niuwinga kiasi gani?

10. Ama ni ng’ombe arud’io malisoni
Afunguliwe irimba angie idhidhini
Akamwe madhiva apekwe sokoni
Annufaishe kivumbe hayawani?

11. Haa huvaomba siapudheni
Kwa uchulivu nno apimeni
Muketi hili muvulidhanyeni
Muwashirikio ana faid’a gani?

12. Vahishimuni vadhee venyu
Muchunge hishima dhenyu
Mujali na kupend’a mila enyu
Mukanye aso na faid’a kwenyu

13. Jamii hulindrwa na mabarobaro
Mashujaha akilini nyoyo n’eroro
Vayidhao miyini kuechewa kero
Sivaechavo uvundro na kasoro

14. Siveni vachumwa va marungi Faru
Miyini mwenyu mukaecha en’e ruru
Mai kifuma kafukuwa ishimo kh’ururu
Akiyaa akayalia mad’od’i na makuru

15. Siveni vachumwa vavunga na ch’embe
Afia dhenyu mukadhichofa kwa dhembe
Na maneno akufuru nkudhia musambe
Rud’ini kwa Mola nsamaha mukaombe

16. Musive vachumwa va udhembe
Mukachiwa magambari ng'ombe
Yivani kuva likivaangukia iyombe
Litakosekana lakuvafukuwa yembe

17. Musichumiwe mukambiriwa
Mwen'e kichi akisha kutukuwa
Kwenyu miyini mukadharauliwa
Kwa vana siasa mukasahauliwa

18. Simamani jamii ifaid'ike
Miyini kwenyu mutukuke
Haki dhenyu dhihifadhike
Ukiya udhee musisumbuke

19. Jamii dhenyu dhipend'eni
Shetwani kitoto simpeni
Avadhee venyu sikidhani
Mujenge kwenyu miyini

20. Liepukeni kila la uhuni
Muipe nguvu enyu d'ini
Uwaibike ote ushetwani
Ugure kwechu kote miyini

21. Nchu nsawa hutaba mema
Alee en'e kunufaisha umma
Akuvasaid'ia baba na mama
Sikutaba kila ayao aujoma

22. Nchu kwavo huchengedha
Havund'i, upudhi huvodha
Huvaomba haa kuwavadha
Na mutake kuachungudha

23. Mvund'a kwavo golo ni nlanisi
Afadhali ulee uvodheeo uyusi
Taushikia ph'uwa upiche basi
Mvund'ati ni kama pwapwasi

24. Mvund'a kwavo udhidhie
Vadhee vachwambidhie
Akuvund'a musiakubalie
Miyini kwechu achutapie

25. In'i ndrin'i mabarobaro
Kugumu hufanya kweroro
Musikubali kupokea kero
Miyini likaecha kasoro

26. Ndrin'i valind'i vamiyini
Kuvund'a basi sikubalini
Akuecha aibu akachaeni
Akuecha sifa akaribisheni

27. Shikanani na pend'anani
Akuvachesa apingeni
Akuvaunganisha aungeni
Kupache nguvu Bajunini

28. Kwa mavadho madhuri said'ianani
Mavadho maovu asipiche milangoni
Akuchupend'edha akumbachieni
Na akuchutukidha basi afukudheni

29. Na ijengeeni ngome hishima
Muvatukudhe vachu vadhima
Vadhee kwa wema vakiterema
Maishani vana huvayia nema

30. Sitanena mangi ela kuvausia
Haa mupache kuwadhingatia
Na amwisho th'akao kuvaatia
Muwapime sana nakuwafikiria

31. Ubasho wa mwisho upulikeni
Maneno muwachie nno akilini
Nd'ia dha sawa chudhivoneni
Kulipo mochoni kuve ph'eponi

32. Kongo hwambiwa kongoni, kongoni kaecha kongo
Lakini th'ongo jamani havoni, na avonao sitongo
Urongo ungafanywa shani, ukweli hauvi urongo
Hunena maneno pulikani, siavekei dhilingo

33. Nani bikwe kwa simbo, na hata kwa dhigungo
Th'aiyosa angu bongo, isiveko moyoni n'ongo
Usive ukweli urongo, ukweli ukava ushingo
Hunena mambo alivo, siavekei dhilingo

34. Huwanena ahitajiwavo, wala sinyamisi shingo
Vulevule niavonavo, huwavona siyava th'ongo
Urongo upend'elewavo, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, siavekei dhilingo

35. Kin'ime cha tamu ilivo, utungu ni ushingo
Ni anenao atukiwavo, sitaafungia nlango
Urongo ukubaliwavo, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, siavekei dhilingo

36. Ungava n'dhuri ulivo, hauyawi hondreni mpingo
Lakini kumea umeavo, nao hwand'ama miongo
Urongo unyamaliwavo, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, katu siavekei dhilingo

37. Nyongo itukuwavo, uwamudhi mbwake bongo
Maumudhi amuevoevo, sisawa na kwen'e pango
Urongo upend'edhwavo, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, katu siavekei dhilingo

38. Chwengeni pan'a ajengavo, ishimo pia n'jengo
Kichundru kichengedhwavo, n'on'i una malengo
Urongo namuna upangwavo, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, katu siavekei dhilingo

39. Majukwaa chujengavo, hutabwa wechu ulingo
Simichi ikorogwavo, ni nkandro wa uvuongo
Urongo utukudhwavo, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, katu siavekei dhilingo

40. Na vuso sikishogo, kifuwa hakivi nyongo
Kudhia sikusuluhia, udhivu haudhui mpango
Urongo kuubarikia, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, siavekei dhilingo

41. Usafishwao ni upovu, nkuchema kukacha gongo
Na kuhad’aa siwerevu, kokodhimba siung’ongo
Urongo kipacha nguvu, ukweli hauvi urongo
Hunena mambo alivo, siavekei dhilingo.

## Chuhifadhini Ṯuraṯhi

***Yusuf Kassim***

1. Awali nawabuṯadi, kwa ina lake Jalia,
Ni pweke mwene ahadi, vaja kuchuṯimidhia,
Eo nami sina budi, ṯamasha kuichangia,
Chuhifadhini ṯuraṯhi, mwaṯa mila ni nchumwa.

2. Chuhifadhini ṯuraṯhi, chudumishe ṯamaduni,
Chuhimidhane vanaṯi, chusipwedhe kuva duni,
Chudhike mihadharaṯi, dhijana muwaauni,
Chuhifadhini ṯuraṯhi, mwaṯa mila ni nchumwa.

3. Uṯamaduni hadhina, bajuni chwaivunia,
Akina mama kwa hina, baba kandu na kofia,
Aura kwechu ni bina, umagharibi susia,
Chuhifadhini ṯuraṯhi, mwaṯa Mila ni nchumwa.

4. Amu mui wa adhali, majengo ake ajabu,
Amepangwa maṯufali, waashi wa kiarabu,
kuna vaṯokao mbali, Amu huya kuiṯibu,
Chuhifadhini ṯuraṯhi, mwaṯa Mila ni nchumwa.

5. Punda Amu mesheheni, ṯena kuṯoka kichambo,
Ndugu navahusieni, musiaṯe haya mambo,
Chukia na baharini, majahadhi mashindano,
Chuhifadhini ṯuraṯhi, mwaṯa Mila ni nchumwa.

6. Lahaja echu vaamu, nsamiaṯi adhali,
Miundo ake adhimu, muinenapo asali,
Kisha kuna ukarimu, Chukicheledha ajali,
Chuhifadhini ṯuraṯhi, mwaṯa Mila ni nchumwa.

## Chuṯayapo Maadili

***Quswai Sufiyani***

1. Bismillahi Manani, naanda angu kauli
Swala dhende kwa Amini, swahaba na vake ali
Na jamii wa-umini, walofuacha Rasuli
Chuṯayapo maadili, wavele chwawaṯamani

2. Ninenapo a dhamani, si hadisi ni ukweli
Ungiapo mchaani, kuna mema maadili
Angiyao haṯiani, uma ukimkabili
Chuṯayapo maadili, wavele chwawaṯamani

3. Wanuna kwavo numbani, havaṯoi ufidhuli
Wakiomba samahani, baba awapo mkali
Iliao ṯamaduni, kudhungumudha ukweli
Chuṯayapo maadili, wavele chwawaṯamani

4. Kama ndugu majirani, kipendana kwelikweli
Hawashikiani kani, ṯabia dhao jamili
Eo nasi chwaṯamani, chumedhiṯupia mbali
Chuṯayapo maadili, wavele chwawaṯamani

5. Ṯunu ṯamasha yakini, dhisahani dhibakuli
Dhaṯembea michaani, numba huchii kufuli
Alokuva masikini, kaṯu hakuva jangili
Chuṯayapo maadili, wavele chwawaṯamani

6. Ṯama niko kikomoni, bajuni meṯoka mbali
Wafanyalo namba wani, hawakuwahi kufeli
Hela nasi chwamkeni, chusiwe moyo jabali
Chuṯayapo maadili, wavele chwawaṯamani

## ṮANABUHI

*Quswai Sufiyani*

1. Moyo umefanya kicho, kwa uṯungu huniṯoma
   Yalioko si machocho, haṯa hujera kusema
   Kuchenda kilicho sicho, vana na vachu vadhima
   Chwaenda vapi Bajuni, mbona ṯwadhidi kudhama?

2. Dawa dhoṯe dha kulewa, dhiko kwechu mayumbani
   Sidhiṯai mwadhiyua, mechuchia hasarani
   Uchumi mechukamua, chumebaki masikini
   Chwaenda vapi Bajuni, mbona ṯwadhidi kudhama?

3. Meecha mbovu asari, hachuna la kuivuna
   Yambo hili sio siri, kula mmoya huvona
   Imesimama haṯari, kwa dhisu chunaṯindana
   Chwaenda vapi Bajuni, mbona ṯwadhidi kudhama?

4. Haṯa kwa venye mashamba, havaivi vachendani
   Si minazi si migomba, henda kujepa wahuni
   Kula kichu vakaramba, ni haki hii jamani?
   Chwaenda vapi Bajuni, mbona ṯwadhidi kudhama?

5. Dini chulipoiyaṯa, ndio haa a kangiya
   Chumebakiwa kuyuṯa, kumi hachupachi moya
   Yoṯe haa kuchupacha, Bajuni hana umoya
   Chwaenda vapi Bajuni, mbona ṯwadhidi kudhama?

6. Chushikaneni masombo, kwa pamoya chushikane
   Usokushika ulimbo, mapema usiivone
   Ṯakunasa si kichambo, hii dunia ingine
   Chwaenda vapi Bajuni, mbona ṯwadhidi kudhama?

## Dhama Dhechu

*Omar M. Maulana*

1. Nikumbukapo ujana, ruhu angu huumiya
   Pwani chukikusanyana, dhidau kudhiṯedheya
   Akiya Shali wa Mbwana, karara akichuchiya
   Vala hachukuchukana, hishima chulimwekeya

2. Chukikimbiya chuvoni, mwichuni chukaekeya
   Chukadhiinda dhijuni, ulimbo kuvashikiya
   Na dhigwe dha michamboni, dhoṯe chukidhichumiya
   Eo hayavonekani, hulivoni haṯa moya

3. Chulikilima hondeni, babe kunsaidiya,
   Kifusiya ishimoni, mbeu kudhilimbikiya
   Na kukweya ulingoni, cheu chukidhichumiya
   Ako kwapi siyavoni, vana havakupichiya

4. Kwa mambo a baharini, haa chulikusudiya
   Ndiyo kadhi a mbeeni, isi chuṯaifanyiya
   Mayongoo bei peni, chukidhanya bahariya
   Eo vako darasani, a kidhungu husomeya

5. Yuwa kuvucha maini, paka uive koveya
   Likishika magomeni, mbidhi chukilidhamiya
   Nsiṯi iyu na ṯini, chukivucha kwa pamoya
   Ukikosa kee vaṯakubikiya

6. Chukiichosa mwambani, mai pima miya moya
   Kamba hunṯowa ndani, ishimoni alongiya
   Pumudhi yavuyavuni, udhuke dhimikwishiya
   Kina papa mavindoni, hukuvira kuchishiya

7. Na nyavu dha ufuoni, mikidhi chukiindiya
   Dhishikapo mashuuni, henda kudhiṯambuliya
   Chukivucha kwa makini, isi kuṯowambiriya
   Eo dhikwadho dha pwani, imechubana shariya

8. Madofe sufuriyani, huchensha kuiliya
Bodo mocho machumboni, huchiya bila udhiya
Ṯasi, ngisi nṯudhini, huliwa kuṯobakiya
Chai kavu ndomoni, huchoma kuṯosikiya

9. Dhali dhama dha amani, mangi chumeyapichiya
Chukiṯanga baharini, uhuru chwalidhoweya
Bori hadi Kiyamboni, Kuṯoma chukiyendeya
Dhikwadho dha baharini Hii eo dhimekuya

## A Kwapi Maina Echu?

***Omar M. Maulana***

1. Sio ṯena maina alee, maina ndabadilika,
Sio ṯena yavalee, dhijana dha kadhalika,
Sio ṯena yavelee, maina a kuṯukuka,
Sasa yandabadilishwa, maina sio alee

2. Hakuna ṯena Alale, Mwanapembe nsifika,
Hakuna ṯena Bakale, kina Ṯora vachaika,
Hakuna ṯena Nyakale, a Ṯima na Mwanaika,
Sasa yandabadilishwa, Maina sio alee

3. Maina a kina kale, sasa chundaambiriya,
Maina a Barkale, ako kwapi kusikiya?
Maina echu a Ile, na Aroi mepoṯeya
Sasa yandabadilishwa, maina sio alee.

4. Isi suṯe ni varabu, ubajuni hukimbiya
Isi chwaṯaka sawabu, kwa maina kuichiya,
A maswahaba si ṯabu, maina yandaeneya,
Sasa yandabadilishwa, Maina sio alee.

5. Mbwarafaki halifai, ina hili huchukera,
Mbwaramadi hulichai, kwa kuikosa busara,
Mbwarausi hako hai, na kwa ina undagura,
Sasa yandabadilishwa, maina sio alee.

6. Kumwicha mwana Famau, sasa hachuwedhi ṯena,
Kumwicha ni madharau, ishe hilo ṯalikana,
Kumwicha wako Malau, henda likakosekana,
Sasa yandabadilishwa, maina Sio alee.

7. Vako kwapi kina Mbwara, Shembwende na Ishemwana,?
Vako kwapi valo bara, maina a kiungwana,?
Vako kwapi vandavira, Sivaoni kina Nana,
Sasa yandabadilishwa, Maina sio alee.

## Uganga

***Omar M. Maulana***

1. Ruhu dhimebadilika, sio ṯena dha dhamani
Nyoyo dhimegafilika, dhimwendeme Shaiṯwani
Imani dhimechuṯoka, ndudho hamuelevani

2. Hurogana kwa sihiri, na chego dha kuchambika
Mambo alo na haṯwari, kufanya ruhu kuṯoka
Yamekuva si a siri, chumedhiye kuumbuka

3. Kwa vaganga hachuṯoki, kambi kwavo chumebika
La haki hachuliṯaki, chumikwenda kuchambika
Ili chuvapoke haki, mayaṯima kucheseka

4. Nganga kiṯaki haki, isi ṯayari kulipa
Chuyapoṯedhe malaki, huduma ake kuchupa
Chunroge alobaki, kwa midhi na kwa dhiṯupa

5. Muṯafudhe kila rangi, mbudhi, kondoo na kuku
Hapo aṯafanywa mangi, yalopijwa marufuku
Yavundwe ṯena maingi, kuwafunga vasishuku

6. Muchiwe ndani pangoni, kwene lana ya midhimu
Munshiriki Manani, na oṯe mwayafahamu
Mwachiya jiwe chumboni, Mume ave marehemu

7. Vaganga huvasamini, hachwendi bila ya wao
Vanenalo chwaamini, yoṯe vaṯakao ao
Mwana huvekwa kichini, vayapache mambo ao

8. Mashindano a jahadhi, mambo haa havakosi
Kisicho mwendo kwa ṯedhi, kipiche mbiyo kwa kasi
Vashindwe valo vayudhi, na vaganga va nuhusi

9. Na punda aso kawedhi, huva farasi kwa kweli
Aṯavishwa mahiridhi, apijiwe na ranli
Akiṯoka humuedhi, aṯakushinda kwa mbali

10. Nganga aṯakwambiya, kaiyale kaburini
Uṯajiri uṯakuya, uve na mamilioni
Huna budi kuridhiya, kwa ṯamaa ya moyoni

11. Harusi bila ranli, hili halivedhekani
Nganga alo nkali, unṯafudhe n̠yini
Avambiye sikubali, nke huu kisirani

12. Chuṯubuni kwa Ilahi, mambo haa chuvaṯeni
Chufanye na masilahi, chulodhulumu kadhini
Kwa mapema chuyawahi, hachuyenda kaburini

## Maledhi A Kibajuni

***Mzee Athman Shee***

1. Mwana ndhaye mwichuni, uyive la kumueya
Ṯena ṯapacha makini, mambo aṯamuweleya
Usidhandame fafani, ndiya dhiṯakupoṯeya.

2. Mwana ndhaye ndiyani, usimpe madhoveya
Umuwanike yuvani, pepo dhikimpepeya
Usidhandame fafani, ndiya uṯaidhengeya.

3. Mwana ndhaye barani, bugeni likinyesheya
Umuaṯe pagachini, kalaha aṯadhidhoveya
Usidhandame fafani, mwisho huṯasikiliya.

4. Mwana ndhaye ṯangini, maṯo akiangaliya
Usimuaṯe chunguni, dira dhiṯanpoṯeya
Usidhandame fafani, uṯakuya kuyuṯiya.

5. Mwana ndhaye sagoni, ṯevu vakinkiliya
Aṯoke usingidhini, vaume ṯankimbiya
Usidhandame fafani, bahaṯi haiṯakuya.

6. Mwana ndhaye kondreni, ayive kupaliliya
Unchiye dharubuni, apache kusuluhiya
Usidhandame fafani, safari iṯakupoṯeya.

## Dhama Hidho

***Zuwena Ahmed Mohamed***

1. A sasa si a dhamani, ana ṯafauṯi sana.
Hapo kwalina imani, vaja valikipendana.
Baraka dha Rahmani, ndripo dhikapachikana.
Madhicho a Mwanamina, huva nda nyi ndhima.

2. Ilikuva nchaani, vachu vakikusanyana.
Kupanga vafanye nini, kwene kusaidiana.
Vakipandra na kidhani, mapaa kudhimbiana.
Kaṯu havakuaṯana, vana kwa vachu vadhima.

3. Dhikiandikwa mochoni, kundre muye kuchafuna.
Vakishuka ipaani, mule muvapo husona.
Chai a ndalasini, mushushie hidho ṯena.
Sasa kiva pesa huna, ako hukalia nima.

4. Basi nasi hachuvoni, mamboe chukaapima?
Huchoka na hachusoni, la shubiri hwendra pima.
Vachu maṯo upaani, vako mbioni daima.
Chudhipachepi neema, madhuri kiasukuma?

5. Enga chuko machachani, hali kwa sasa si njema.
Na hachusaidiani, kusaidia ni kwema.
Ruhu hadhina amani, dhiki dhimechuegema.
Huchelewa si mapema, ni kheri badilikani.

6. Hapa niko kikomoni, hut̲osa nit̲aikoma.
Mat̲odhi t̲ele mat̲oni, moyo kwa shaki huhema.
Hela ndrudhangu ndooni, chuufufueni wema.
Chufaidi kila lema, chuishi kama mwandoni.

## Jamii

***Hassan Msham Mahmoud***

1. Kusudi la chungo hii, t̲aeledha sivafit̲i
Nachunga kuhusu mii, na menendo ya umat̲i
Ladhima kwene jamii, ibuniwe harakat̲i

2. Sineni kwa usanii, kufurahisha baradha
Na wala sivat̲adhii, mukamba navaapidha
Ladhima kwene jamii, vachu vaat̲e kut̲edha

3. Na eo sivakanii, kachika haa maneno
Navaomba mut̲walii, kwa ibara na mifano
Ladhima kwene jamii, kuve na nshikamano

4. Chwendeni chukat̲alii, kachika it̲i dha vachu
Kwa heri hachuvangii, vako mbee kila kichu
Ladhima kwene jamii, chut̲hamini sana uchu

5. Dhicha dhechu hadhisii, kila siku chwapondana
Na vakuru vako dhii, vameikosa namuna
Ladhima kwene jamii, chuve venye kupendana

6. Mwisho chwandeni kut̲wii, kwa hakina kwa ruhuma
Chuit̲abeni kisii, kwa kadhi dha ukulima
Ladhima kwene jamii, vachu vadhidi kusoma

## Kiswahili

*Hassan Msham Mahmoud*

1. Bahari ni va vaṯonyi, vanavoṯoma maini
A kina moni na mwinyi, vakeṯio ufuoni
Na Kiswahili cha nyanyi, kama si cha Mbajuni?

2. Chuandameni usuli, ili chupache bayani
Hili yambo chujadili, kwa usawa na maṯini
Ni cha nyanyi Kiswahili, kama si cha mbajuni?

3. Eo chwambidhane kweli, kwa ina la Rwahamani
Chuṯoleane dalili, hukumu a kesi hini
Ni cha nyanyi Kiswahili, kama si cha Mbajuni?

4. Chusichaeni mavili, kwene imoya vendani
Haki nda kuikabili, ingava ni ṯafashani
Ni cha nyanyi Kiswahili, kama si cha Mbajuni?

5. Chusiaṯeni halali, kwa dhihi dha duniani
Hafaulu baradhuli, angava ana makini
Ni cha nyanyi Kiswahili, kama si cha Mbajuni?

6. Mwisho wa shairi hili, mwene kesi muiveni
Ni mbwa Nshamu rijali, aviliwae Hassani
Huvavudha Kiswahili, mwenewe si Mbajuni?

## Harusi dha Vabajuni

*Abubaker Mohamed Khuchi*

1. Ni mbili dhilo muhimu, harusi dha Vabajuni
Harusi dhilidho tamu, harusi dhilo na dini
Hili ni yambo muhimu, kwechu ni utamaduni
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

2. Harusi dha kutahiri, vana vechu va kiume
Dhilo yaa n'ingi heri, kwa baraka dha Nchume
Akibikwa na matari, vakachikapo vaume
Bakiwa na mila echu, hoo ndio nsimamo

3. Chukitedha mudhidile, chukiiyala chineni
Chukiyala chineni, kwa furaha na amani
Chukiyala majambini, chukiva hapo chineni
Bajuni ni valevale, si Vabajuini vangine
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

4. Hutahiriwa kwa kigwe, cha udhi ulo imara
Kila mwana hula kigwe, ugwe ulo barabara
Vachu hutufia wembe, na duwa dhilidho bora
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

5. Harusi a kuolewa, nao pia ni fahari
Bwanarusi hunyolewa, kwa gungu ao kwa tari
Kwa nyimbo dha kuongoa, na nyimbo na mashairi
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

6. Usiku hutedhwa ngoma, kuna ndongwe na nsondro
Vachu vote huterema, vana vote vako kandro
Vaume vamesimama, vaufueche nsondro
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

7. Ama harusi a pili, ni ile akuvakana
Ndrio arusi a kweli, mana vachiu hudhaana
Hata kama huavatana, kidhadhi hupachikana
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

8. Mungu atachuhifadhi, na balaa dha dunia
Achupe na dhake radhi, na peponi kuchuchia
Achwepushe na maradhi, maovu alo ingia
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

9. Madirasa na Sikuli, vana chuvasomesheni
Dini chushikeni kweli, chukifa chwende peponi
Tena chuve na ukweli, urongo chuuvateni
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

10. Hoo ni wasia wangu, nnavapa ushikeni
Namuomba Bwana Mungu, achuhivadhi Bajuni
Hapa kwene ulimwengu, ahera chwendre peponi
Bakiwa na mila echu, hoo ndrio nsimamo

# Nlango a Kumi: Madhingira

## Kulindra Madhingira

***Quswai Sufiyani***

1. Naipiga a ngambo, navudhia ṯarumbeṯa
   Mambo ameanda kombo, kisha chusiye kuyuṯa
   Madhingira ya kichambo, hung’ara chuliyapacha
   Ya eo hunuka shombo, ni wapi chulipobecha?

2. Ṯukifahamu dhamani, madhingira alisafi
   Chaka kiṯupwa yaani, kihalifu vala kofi
   Mbona chmekuva duni, kwa uchafu ni walafi?
   Shime suṯe chufanyeni, yapokuva ṯakilifu

3. Siṯa dhoṯe dhiking’ara, upichapo kula kona
   Punda havakudhurura, mabandani huvabana
   Eo vamekuva hura, si usiku si nṯana
   Madhingira medorora, uchafu meṯapakana

4. Dhimeyaa pempasi, hunuka kula mahali
   Na vachu havaikisi, huṯupa kula mahali
   Haṯa kaweka nochisi, hilo kwavo havajali
   Nasi haraka upesi, nyendo dhechu chubadili

5. Baharini chuvuako, dhimipoṯea neema
   Ṯafikiri huko siko, mambo endee nrama
   Chwapaṯa makombomwiko, isi chwendao kuṯoma
   Chubadili miondoko, chusiwangojeni NEMA

6. Hapa napiga bureki, nilioamba yaṯosha
   Usafi chupige jeki, mii echu kusafisha
   Hami haivi kaniki, musiande kupochosha
   Miṯi kupanda huṯaki, ukombee kuyangusha

## Kuhifadhi Madhingira ni Ada

*Swaleh Omar Mohamed*

1. Kuhifadhi madhingira, ni ada kwa vabajuni
   Hupea kwa makarara, kukang’ara michaani
   Ungiapo ni ṯwahara, haṯa kwechu mahondeni.

2. Chukiimedha na michi, a mivinje na minadhi
   Na mingine kachi kachi, a dhivuli dhipumbadhi
   Chukichengedha makuchi, chukadhimba kwene wadhi.

3. Chaka chukidhikusanya, kisha hudhisumba mocho
   Ng’ombe na mbudhi vakinya, samadi hufanya hicho
   Usafi chukiufanya, bila kuvona udhicho.

4. Dhisima na majabia, usafi ulichupasa
   Madawa chukiachia, kusudi kuachakasa
   Mai chukiachumia, kwa kunwa na kuiyosa.

5. Vanyama kihifadhiwa, kila nchu banda lake
   Chakula vakichiliwa, kila nchu dumu lake
   Kwa dawa vakiṯibiwa, maradhi asivashike.

6. Ṯama ahiri shairi, nndafika kikomoni
   Na usafi wa bahari, hufagia ufuoni
   Kwa suṯe chukahiyari, kung’arisha dhijijini.

## Madhingira

*Khalid Omar Kanjenje*

1. Kwa kulinda madhingira, ni mweṉewe Mbajuni
   Huyafanya kwa busara, ṉumbani na michaani
   Ṯena hulinda kwa ghera, kukanawiri numbani.

2. Huasumua upesi, magugu oṯe myini
   Ṯena bila wasiwasi, husafisha kwa yakini
   Hoo ndio ufanisi, kwa usafi namba wani.

3. Mashimo huasafisha, na dhisima kadhalika
   Na uchafu kuondosha, wa kinyesi bila shaka
   Na dhoo hudhidumisha, kuwa safi kadhalika.

4. Na piya hupanda michi, hilo kwechu ni muhimu
   Kwa midhuri mikakachi, nasi hangacha jukumu
   Hachutaki achiachi, kuwajibika chwadumu.

5. Huondoa chakachaka, dhilo koṯe mayumbani
   Na vachu huyumuika, wakava voṯe miini
   Madhingira husafika, koṯe miini jamani.

6. Ṯama hapa nimependa, kusimama ndrudhanguni
   Wabajuni huipinda, kuyalinda kwa makini
   Madhingira kuyalinda, bajuni ni namba wani.

## Kulindra Madhingira

***Zuwena Ahmed Mohamed***

1. Chualindre maeneo, ambao ndrani chwakaa
   Madhingira chupecheo, kwa sana anochufaa
   Asive na halagao, na magugu asofaa
   Na hii vua inyao, mai asipache kaa

2. Mambo aṯakikanao, ndrudhangu ni kama haa
   Chusafishe kwa upeo, na kusumua hufaa
   Ndripo chupache pumbao, uwee kuṯosambaa
   Vana vaendrapo mbio, vasipache kukuvaa

3. Na mabusiṯani nao, a machundra na maua
   Aveko kila kuchao, awedhe na kufumbua
   Nguvo chudhichumiao, chuiṯahidi kufua
   Chuṯafaidi kwa hao, nadho ruhu dhiṯachua

4. Dhichu chudhichumiao, chukisha kudhifungua
   Chuaṯe chuafanyao, chaka popoṯe kusua
   Chudhipeke maeneo, chudhisumbe kimurua
   Usivaudhi vendio, kwa uvundro kuvuvua

5. Kwene miṯaro mekuwa, uchafu humbirilia
Kisha inyeshapo vuwa, ṯabu dhikachungilia
Mai kupacha haṯuwa, hushindrwa hela sikia
Kifanyeni kibaruwa, cha kuṯokuchudhibia

6. Ṯamaṯi hapa ṯachua, huṯosa nalovambia
Isive huvasumbua, mambo kivadhidishia
Mola kushusha afua, ni chukiisaidia
Ṯena bila kubagua, usafi kuifanyia

# Nlango a Kumi na Moja: Maisha a Ugenini

## Maisha a Ugenini

*Famau Ali Famau*

1. Huvaeledha dhilivo, mambo a dunia echu
   Emame nchu nkwavo, imi kasa sina kwechu
   Huenenda ndivo sivo, kana ngeni kwa vachu.

2. Ngeni hachundi nguvo, ugenini hana kichu
   Huivelea ni mbovu, hasali hushinda chuchu
   Mwisho hukosa ubavo, ungaumiliki mwichu.

3. Ugeni ni kama chuvo, humfunda kila nchu
   Na vachu vakuivavo, vakakuvona si kichu
   Dhienge ṯabia dhavo, vangine havana uchu.

4. Maisha akenda ndivo, a ugenini mwenechu
   Hili ni rahisi kwavo, kukuomba vachu vechu
   Na ndivo mambo alivo, hondoo na imbwamwichu.

5. Ugenini sio kwavo, hunkoṯa kila nchu
   Chambo ungachia sivo, ṯanshika pono mwichu
   Hukimu vengi vendavo, vala havarudi kwechu.

6. Ugenini a Kosovo, bado kuna vachu vechu
   Havarudi venendavo, havaṯamani makwechu
   Mungu ṯavaafu navo, vasisavadhwe na dhichu.

7. Ṯamaṯi nivambiavo, ni ugenini si kwechu
   Hulingana uṯakavo, mambo huva ni machachu
   Ima kubakia kwavo, kaivelea kiachu.

## Maisha Ugenini

*Khalid Omar Kanjenje*

1. Baada ya kuṯolewa, hakika kwechu miini
Isi chukashambuliwa, na maharamia miṯeni
Ndio chukakimbilia, kuekea ugenini.

2. Bajuni kila mahali, vangi wamechapakaa
Wengine nṯi za mbali, Bajuni wameenea
Vanavake kwa rijali, ndio walochokomea.

3. Vangine vakenda Shanga, na vangine wako Amu
Vangi kwa kuṯangaṯanga, wakafikia Waṯamu
Na vangine vako Ṯanga, vangine Daresalamu.

4. Na vangine Marekani, na Ulaya vamengia
Koṯe vako Vabajuni, kwa shida zilowangia
Ni maisha ugenini, sasa wameyadhowea.

5. Wamedhowea maisha, a ugenini hakika
Hawawedhi kuyepusha, mizizi ao meshika
Vao vamefurahisha, wendhao kujumuika.

6. Hapa sasa ni ṯamaṯi, kalamu naeka ṯini
Hakika voṯe umaṯi, jamii a Vabajuni
Waliyaweza kwa dhaṯi, maisha a ugenini.

# Nlango a Kumi na Mbili: Ushirikishwaji

## Nyukani Vana Nyukani

*Jamila Ali Haji*

1. Nyukani vana nyukani, nyukani chwendeni pwani
Pwani chukimbilieni, chukapokee vageni
Vandaṯolewa barani, kwechu chuvapokeeni

2. Chukapokea vageni, numbani chukavachia
Ivo pweke masikini, bila nguvo haṯa moya
Valikimbilia pwani, madauni vakangia

3. Kae dhaliko imani, na huruma ṯeleṯele
Haya ndudhechu sonani, dhishindo dha vasomale
Hiki chakula ilani, na majumba muiyale

4. Kwa ufupi kifunua, mambo aliopichika
Va barani veṯolewa, miyi avo vakaṯoka
Mabara akimbiriwa, kwa kukimbiwa shifuṯa

5. Meṯolewa maskini, na haramii shefuṯe
Kuandia Ishakani, na dhigambogambo dhoṯe
Vakangia dhisiwani, vakahora mali oṯe

6. Nina ineno akali, nikeṯipo hushangaa
Vachu vako mbalimbali, kwa maisha huṯaaṯaa
Huiomba sirikali, ivape navo ridhaa

7. Hupacha nyaka siṯini, changu kuṯolewa kwavo
Ni vakimbidhi va ndani, hufaa kuengwa navo
Varudi kwavo vabuni, vaishi na vana vavo

## Hupachikanae furaha?

*Mohamed M. Kombo*

1. Kwand'a huvudha habari
Kwa mila echu ni udhuri
Hamuyambo in'i maamiri
Mad'i D'ad'i nind'avayia

2. Nind'avayia na isuwali
Kunijibu mukikubali
Huvaomba tafadhali
Faid'a kuchupachia

3. Raha ndrio Furaha
Ama Furaha ni Raha?
Lipi ndrilo lenye Jaha
Uko wakuchwambia?

4. Furaha ni afiya nd'uri?
Ama ni nrefu umuri?
Kama ukipawa hiyari
Nilipi taichagulia?

5. Ote anao nsimamo
Angava na kikomo
Furaha ingavemo
Hudhuni huitapia

6. Kama nikupacha Raha
Ndrio kuva na Furaha
Ikikosekana Naswaha
Jee Furaha hukuyia?

7. Naikiva ni Naswaha
En'e kukupa Furaha
Huvaye bora Raha
Ikaya kuivamia?

8. Furaha nimali na utajiri
Ama nikuva jamad'ari
Ukidheeka wako umuri
Hudhuni dhikakuchia?

9. Furaha ni sitarehe
Nikufana sherehe
Ama nikutaka ushehe
Ubora kuipend'elea?

10. Furaha nikupend'wa
Na nyud'i ukafukidhwa
Sabuleni ukapembwa
Asikutose maridhia?

11. Furaha ni umaarufu
Kukuechea utukufu
Ayapo wakukukashifu
Hasira akakuchia?

12. Kama ni Raha kuleva
Hukuchiyae hangiova
Furaha nikutaka kueva
Sinti kudhimbiria?

13. Huvaye kuva ni Furaha
Kunchia ndruo Jaraha
Likakuvelea Karaha
N'ngine kikufanyia?

14. Hupachae Naswaha
Kulifanya la Karaha
Likakuvelea Furaha
Ndruo kumfanyia?

15. Hutafudhwa Furaha
Kwa kuand'amwa Raha
Kikosekana Naswaha
Raha ikava hatia

16. Huvona vaand'amao
Ote alee vaapachao
Huva havatoseki nao
Furahani angavachia

17. Ndripo kuyiva kh'ataka
Wake Furaha uhakika
Kiipacha kuto kutoseka
Kiikosa hudhuni kakuchia

18. Furaha ukikachaliwa
Maudhiko ukachiwa
Raha taichambuwa
Itakavo kukuyia?

19. Ndrio kuvudha niambiwe
Tena kwaudhuri nieledhewe
Kweli a Furaha faid'awe
Nimambo akid'unia?

20. Furaha niyambo gani
Muyivao chueledheni
Atosekao nadho n'nyani
Ipachikanavo kachwambia?

21. Mwisho,lilo bora ni Raha?
Kushindra kuva na Furaha?
Ama nikuva na Naswaha?
Haa mavili kupachikana?

## Kuveeye mbona huvaye?

*Mohamed M. Kombo*

1. Bisumila chwambe
Mungu chumuombe
Achwapuse naudhembe
Simwema kwadhivumbe

2. Chuombe kwa ina lake
Mvumba nvuli na nke
Kudhaa vana vatake
Id'ad'i iyongedheke

3. Mmoya,kumi na mia
Maalifu chukitimia
Jamii kuidhingatia
Nijukumu huchuyia

4. Imi kh'ava ndruo
Shemeji ni nkeo
Vana vadhawao
Niundrugu ukuwao

5. Akendra atakikanavo
N'oki asiifanye mbuvo
Mambo chuapend'eleavo
Haavi chuwavonavo sivo

6. Endrapo kh'ombo
Huya n'dhimbodhimbo
Chukitamani urembo
Chukaangalia ng'ambo

7. Ng'ambo kuna mapicho
Kusikilia niuvuke ncho
Usiche kulivacha ch'ocho
Nahatari dhenye udhicho

8. Kiisitiecho kitofe
Uombe kisikuchofe
Yeda niheri nchafe
Usalama kwa dofe

9. Nd'ia nimbili avu
Audhaifu ni twevu
Tafauti na ushupavu
Hudhifahamu nchulivu

10. Apichao uwamudhie
Nd'ia moya uikubalie
Ima tavulidha huvaye
Ama taajabu kuveeye?

11. Yiva ushupavu singuvu
Wala panga kuchia kh'ovu
Bali nikupend'elea werevu
Ukweli ukapawa nguvu

12. Ivapo utachia tabu
Huvaye ive matulubu
Kupachikana jawabu
Niukweli uve wajibu

13. Huvaye isive nidhana
Wala pia kushindrana
Jawabu kupachikana
Nisababu kuyivikana

14. Huvaye ave ni fulani
Haa nd'a midomoni
Ama hutoka dhitwani
Dhana ndrio sukani?

15. Huvae huvudhwa nyani?
Niyivavo imi th'aabaini
Silammoya chukubalini
Chwalivudhwa vabajuni

16. Huvaye chulioko miyini
Chwalivudhwa chujibuni
Mangine chusiongedheni
Udhicho kavund'a midhani

17. Vachu huvashika vavo
Ndrivo ubinad'amu ulivo
Kama ndrivo chutakavo
N'oki hupendae ambuvo?

18. Vachu huvashika vavo
Mana vavo kuvahora sivo
Ndrivo vachu vachendravo
Kwechu sivo chufanyavo

19. Isi vechu huvahora
Chungayiva nihasara
Huwand'ama aujura
Chukidhani nibusara

20. Niiye haa avao kuva
Kh'uku kuva nambava
Kaukh'a kama kudukuva
Hachutaki hili kuliyiva?

21. Ndrudha nambiani kuveeye
Mbona huvudhwa huvaye?
Nachwambiwe ayieo ayieye
Achangadhwao mamboye?

22. Th'avambia musikie
Kidhani chusitungie
Unvonao ndrie sie
Unvonao sie ndrie

23. Dhana hadhivi ukweli
Asokutamukwa sikauli
Nimavili mbali mbali
Chukubali chusikubali

24. Huvaye nisive ndrimi
Nd'a utamukao ulimi
Upachikanapo uvumi
Ndripo ulipo usemi

25. Hii imi ilidhawa
Na vavili ikaewa
Pweke nikuhad'awa
Kukosa kuichambuwa

26. Wingi mbwamanufaa
Uimi wingi huukachaa
Ikuchi halidhimbi ipaa
Makuchi ipaa hulifaa

27. Mwen'e kuwayiva haa
Ubinafusi huukachaa
Ishimo kamwatia kh'aa
Kidhani asokahitaji taa

28. Asokavoni kidhani
Hamwelei aishimoni
Gorowa simwend'ani
Ake taa chusimpokeni

29. Samaki huoweya baharini
Kwadhiyapa nkiya nsukani
N'on'i nae huuka angani
Kwambava kisusu nsukani

30. Jahadhi husafiri maini
Kwa changa lilo angani
Huongodhwa nasukani
Turusini kana nkononi

31. Api mangine chunene
    Dhamira dhiyivikane
    Ubora uchambulikane
    Sinyendro dhakh’unene

32. Hapa utand’uni th’achuwa
    Nipache nami kupumuwa
    Mbava alonadho n’on’i alipawa
    Sikuipa ndrivo alivo dhawa.

## Kauli A Mafundisho

*Jamila Ali Haji*

1. Sivabiki maṯoṯomo, huvafunda fahamuni
   Kuva nkuru sio kimo, fundi akili kiṯwani
   Mayi a ṯedhi na omo, hudirikana ngamani

2. Muvuavo na kuvumba, kwa mikono na mashini
   Dhiṯimbi mkidhiṯimba, verevu kumbusanani
   Makali menyo a imbwa, lakini haaumani

3. Dhisasi dha baharini, malidhani dhipuluni
   Siyeni nadho miyini, kudhilipa majumbani
   Hadhichakasi sabuni, nyoyo dhikishika kani

4. Muswaliavo sanamu, dhibulani kwa sipika
   Majungu enyu a sumu, pimani mukiapika
   Damu haiosi damu, udhidie kuipaka

5. Vapungufu va fahamu, mwambavo na kungnong’ona
   Mungachupukia sumu, chupache kufarikana
   Yivani kisu cha damu, ulimwenguni hakuna

6. Hondoo vaṯedha ngoma, huilogi maguguni
   Vavudheni valosoma, vachungudhe dhiṯabuni
   Mwanaharamu wa mama, uko vapi simvoni?

## Mwanasimba

*Hassam Msham Mahmoud*

1. Mwana wa simba unani, mbona umeyala sana?
   Huyanenda mavindoni, bado umekuṯumana
   Nyuka venende mwichuni, udhivu si wa maana

2. Mwanasimba usiyale, si wakaṯi wakuyala
   Ṯoka wenende ukale, ndani huṯopacha kula
   Usishiriki uwele, udhivu mbwa mwene ila

3. Mwanasimba iṯaṯudhe, kuṯaṯuka ni faida
   Usiregee ikadhe, iva huna ṯena muda
   Simama uiṯokedhe, udhivu huecha shida

4. Mwanasimba uka uka, kuidhiisha si dawa
   Ukivona undachoka, usiisumbuwe chuwa
   Chunga usive ndhuka, ukangoja kuechewa

5. Mwanasimba nisikiya, awae mwema hadhii
   Uendapo kudhengeya, isome kaida
   Hii avindae huocheya, mwando kwenda hakimbii

6. Mwanasimba uṯaṯufu, kwako uwe ni ladhima
   Si kwamba nakukashifu, kikuambia nguruma
   Mwisho iva mwangalifu, wangalifu ni hikima

## Fumbo

***S.A. Bin Abeid***

1. Imi la kweli siidhi
kiambiwa husikiya
na la sawa silipudhi
hukubali mara moya
simba na ṯuvi na mbudhi
huvuswae dau moya

2. Huvavulidha vayudhi
mwalio nichanguliya
munijudhe wadhi wadhi
apache kunieleya
simba na ṯuvi na mbudhi
huvuswae dau moya?

3. Nimekosa usindidhi
wa leli na nahariya
hubaki na uvuvudhi
kwa hili kufikiriya
simba na ṯuvi na mbudhi
huvuswae dau moya?

4. Malenga valo na hadhi
va kenya na somaliya
chuma chaṯaka mfudhi
ninyoshewe mara moya
simba na ṯuvi na mbudhi
huvuswae dau moya?

5. Sili ḵashusha pumudhi
nami nikalimachiya
lanichiya kikohodhi
hisabu sipachi moya
ni kweli simba na mbudhi
huvusika dau moya?

6. Cẖungo dhaṯaka nyudhi
na manju aloṯimiya
asive na kikohodhi
nshindro unapoliya
vapokedhi kwa henedhi
vapache kudhipokeya
simba na ṯuvi na mbudhi
huvuswae dau moya?

7. Mwisho ṯashusha pumudhi
nipache kulimachiya
ṯena munivee radhi
vashairi kwa pamoya
na jibu la kuniridhi
kwenyu ninalingojeya
simba na ṯuvi na mbudhi
huvuswae dau moya?

## Risala Nda Veṉe Pwani

***S.A. Bin Abeid***

1. Isomeni kwa uchuvu
risala nda veṉe pwani
valoifanya verevu
vaṯengao vabajuni
Kiswahili ni kipevu
chalibuniwa dhamani
mukumbuke kina veṉe
ambao ni maaluma

2. Navapa kwa ṯaawili
mulo mwambao va pwani
musome muṯaamali
na muive kwa undrani
muṯapacha ukamili
muive uṯamaduni
kuva hichi kiswahili
ndricho hichi kibajuni

3. Kiswahili kina kwao
kina na vachẖu venewe
changu dhamani si eo
ṯimbuko mulielewe
lugha ndavo ya mwambao
wala si a mwengineo
Kiswahili kina vene
ambao ni maaluma

4. Chimbuko ni Somalia
kiswahili huwafumbi
Kenya na Ṯanzaniya
hoko bara hawachambi
kilizaliwa shungwaya
husomwae Nairobi
Kiswahili kina veṉe
ambao ni maaluma

5. Ṯoka hoko Banadiri
swahili hadi Sofala
mui na kila bandari
pwani oṯe kwa jumula
kwa lugha vaifahiri
shungwaya ndrio aula
Kiswahili kina veṉe
ambao ni maaluma

6. Bajuni ni suluṯwani
angavundiwa hishima
angaṯolewa samani
kwa ṯurathi aloṯuma
lugha ndake masikini
eo angavekwa ṉima
Kiswahili kina veṉe
ambao ni maaluma

## Hii Shungwaya ni Kwechu Huṯawalie Vageni?

***S.A. Bin Abeid***

1. Hushindrwa kuadhiviya
kuaveka machumboni
kooni mesikiliya
yameniyaa kanwani
huṯafudha kula ndiya
nisaili vabajuni
hii shungwaya ni kwechu
huṯawalie vageni?

2. Vamepichia dhivumbe
kiwandeo milimani
valokuva ni vayumbe
na vaomwe vaiveni
valochumiya dhikombe
dha dhifuvu maishani
hii shungwaya ni kwechu
huṯawalie vageni?

3. Ushahidi ni wa kale
ulokuva kamba mbovu
ukienda waravole
veku nkono va ndovu
magofu a vile vile
yapo kucha ni ṯakavu
hii shungwaya ni kwechu
huṯawalie vageni?

4. Haṯi dhechu ni dha kale
dhilioko dhiṯabuni
aridhi nda vadaile
ṯa kwa na va uṯanuni
valolimiya mawele
na kuyala saririni
hii shungwaya ni kwechu
huṯawalie vageni?

5. Kunako na vachandraa
ndau valiosakini
valochumia kiamban
kwa ngodhi dha hayawani
hukosae manufaa
vakaṯolewa funguni
hii shungwaya ni kwechu
huṯawalie vageni?

6. Ṯoka dhama dhilopicha
dha Nabii Selemani
valikuwa vaokwacha
ṯayari vamesakini
na Mombasa chika sicha
umo ṯele ubajuni
hii shungwaya ni kwechu
huṯawalie vageni?

## Sivone Dhombo Kupicha Ungama Ulini Mui

*S.A. Bin Abeid*

1. Uli biladi na sicha
madhiva ali ni mai
na kufuru dhikachacha
vasive na ṯanabui
sivone dhombo kupicha
ungama uli ni mui

2. Vali vamejenga ḵucha
buyuṯi mbali na mai
kwa adhabu vakaḵucha
dhiloṯokea samai
sivone dhombo kupicha
ungama uli ni mui

3. Numba dhalimecha mecha
maisha haasumbui
sheṯwani akavapacha
voṯe kwa amali sui
sivone dhombo kupicha
ungama uli ni mui

4. Bahari ake huchacha
pepo dhikivamba mai
ukiambiwa ṯachecha
kuva ulikuva mui
sivone dhombo kupicha
ungama uli ni mui

5. Na mayi ake huvucha
kama nlango va kui
ulo na wingi machacha
uambiwao mbwa mai
sivone dhombo kupicha
ungama uli ni mui

6. Mwamba dhibori kupicha
usiku aṯaka rai
ela ṉyudhi wa nocha
mwene hisabu amai
sivone dhombo kupicha
ungama uli ni mui

## Kufukuliwa mafucha

*Hassan Shee*

1. Kivuwaniwacho kichu
Vene haki nacho ndisi
Eo vamedhuka vachu
Vaṯokapo hachuyisi
Hili ni eneo lechu
Lenye dhisima dha gesi
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

2. Si upande wa kusini
Maeneo a Mviṯa
Wala si rasi hafuni
Kueledha siṯoaṯa
Huku kwechu bajunini
Ndipo alipo mafucha
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

3. Mipaka a baharini
Hapo pawaniwanapo
Shakani na Kiamboni
Fahamu si kwenginepo
Eneo lechu bajuni
Ndipo mafucha alipo
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

4. Kuṯoka Kisimaiu
Manda hadi Kipungani
Paṯe Rasini na Ndau
Mpaka Mpekeṯoni
Ni iṯi dha vaṯikuu
Si eo changu dhamani
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

5. Ṯarihi huchuambiya
Makadhi avabajuni
Kwamba valichanguliya
Ndio avo masikani
Eneo hili shungwaya
Si eo changu dhamani
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

6. Ndisi vachu va awali
Ukweli haupingiki
Ṯena venyeji asili
Vanaṯi kindakindaki
Iṯi enye paṯiroli
Ni Bajuni mwene haki
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

7. Ṯoka endhi dha qadimu
Dha Nabi Sulemani
Vakimina valokimu
Mwambao hu wa pwani
Nivaṯikuu fahamu
Vana nṯi namba wani
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

8. Inenavo ṯarihiya
Mwambao hu wa pwani
si Kenya si Somaliya
Sehemu dha mipakani
Ni eneo la shungwaya
Lilo ki ichwa dhamani
Kifukuliwa mafucha
Vanaṯi chuṯafaidi?

9. La mwisho sambi kwa kucha
Lilo wadhi nabaini
Hudhidi kula kukicha
Haki dhechu kuchuhini
Eneo lenye mafucha
Ni it̲i dhechu bajuni
Kifukuliwa mafucha
Vanat̲i chut̲afaidi?

## Chuamke Vabajuni

***S.A. Bin Abeid***

1. Ilahi Mola wa haki
Huomba kwako manani
Dhiondroshe dhechu chuki
Chusive na ushindrani
Uchupe na it̲ifaki
Chushikamane bajuni
Churudi kama dhamani

2. Ubajuni una cheo
Na ina ulimwenguni
Chuvudheni vaivao
T̲arihi dha kidhamani
Lakini vana va eo
Vameut̲owa samani
Sababu ni k̲ichu gani?

3. T̲oka dha mwando karini
T̲arihi dhaeledheya
Ut̲ikuu ubajuni
Ndripo ulipoandiya
Huikosae samani
Na ina likapot̲eya?
Luga chukaimbiriya

4. Chusiifanye vageni
Vakimina va shungwaya
Kwa pukuchu nlimani
T̲anga na bubushi piya
Hut̲olewae samani
Nasi chukayaridhiya?
Ukongwe ukapot̲eya

5. Sasa chujumuikeni
Chuveni k̲ichu kimoya
Chusit̲abe a miyini
Usuli umepot̲eya
Akili churudisheni
Chungieni namba moya
Kama chwalivoandiya

6. Chwaliambiwa kichambo
Chuisikidhapo mbiya
Ikiliya ina yambo
Ndrivo chwalivosikiya
Chuibikeni dhibombo
Ubajuni kuchecheya
La kwava na kut̲wa piya